# Nipashe

Jumatano Novemba 2, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581117

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKAME,

**Wadau wanapokumbusha ukaribu serikali, wananchi**

• Mmoja ahoji mradi visima Kimbiji, Mpera vipi?

UKURASA 13


SUPA JACKPOT

TZS.1,046,433,814

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Zumaridi** adai kuibwa mil.19/- na askari polisi wakati akikamatwa

UKURASA 5



BUNGE LAAGIZA...

# Waliokosa mikopo wakaripoti vyuoni

• **HESLB** yaitwa ikajieleze kulikoni... *Endelea ukurasa 2*

**"Nimeunda kamati ya wataalamu kuchunguza mifumo ya bodi, lakini ninapata upinzani mkali sana mpaka ninashangaa.**



Prof. Adolf Mkenda

**"Wanaopata daraja la kwanza kidato cha sita, wasomeshwe bure na wale wengine wakopeshwe.**



Ester Matiko

**"Mfumo uliopo utazaa matabaka, wanafunzi waliokosa mikopo licha ya kuwa na sifa, wapate mikopo.**



Ezra Chiwelesa

## YALIYOMO

UKURASA WA 11

**VIKOSI VYA JWTZ VYAONGEZA NGUVU KUZIMA MOTO K'NJARO**



SIKU mbili baada ya Mkuu wa Majeshi mstaafu, Jenerali George Waitara, kuzuru...

# Achoma moto wanawe kisa kula kwa jirani

UKURASA 3




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza wakati akifungua Mkutano wa 6 wa Chama cha Wanasheria wa Mabunge ya Afrika wilayani Magharibi "B", Zanzibar jana. **Habari Ukurasa 23**. **PICHA: IKULU**

# Rais Samia: Ondoeni vizuizi vinavyoleta tabu Mto Ruvu

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA, WATUNISIA DK. 90 ZA JASHO LEO** UK.32 **KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akihutubia viongozi pamoja na wananchi waliohudhuria kwenye Kongamano la Kitaifa kuhusu Nishati Safi ya Kupikia, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Samia: Ondoeni vizuizi Mto Ruvu

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewaagiza wakuu wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani pamoja na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuhakikisha vizuizi vyote vya maji kwenye Mto Ruvu vinaondolewa mara moja ili maji ya mto huo yakachangie upatikanaji wa nishati hiyo.

Aliagiza hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa Mjadala wa Kitaifa wa Nishati Safi ulioandaliwa na Wizara ya Nishati na kuhudhuriwa na washiriki zaidi ya 3,000 ikiwamo mikoa ya Morogoro, Shinyanga, Iringa, Dodoma na Tabora.

Rais Samia alisema suala la uhaba wa upatikanaji wa maji Mkoa wa Dar es Salaam lina sura mbili - za asili na zinazosababishwa na wanadamu.

"Kwa kiasi kikubwa kupungua maji Mto Ruvu ni matendo yetu wenyewe, tumeambiwa hapa mkoa ule unakata miti kwa kiasi kikubwa, ardhi inakauka. Vyanzo vidogo vinakauka, maji hayaendi, na yale yanayokwenda unakuta njiani watu wameweka vizuizi maji hayawezi kwenda," "Unakuta mashine kubwa zimewekwa, 'wanapampu' maji kwenda kwenye mashamba, mashamba ya wageni wala siyo mashamba ya wenyeji wa eneo lile, unakuta vizuizi kadhaa watu wamejenga mabwawa humo ndani wanafuga samaki humo," alisema.

Kutokana na kadhia hiyo, Rais Samia aliwaagiza wakuu hao wa mikoa Dar es Salaam na Pwani pamoja na DAWASA kuhakikisha wanakwenda kuondoa vizuizi vyote Mto Ruvu.

"Nilizungumza na DAWASA wakasema wamefanya operesheni mwezi uliopita, binadamu ni mzito sana inawezekana mmepita mwezi uliopita mlipoondoka tayari wameweka vizuizi, ninaomba mwende kuzunguka, kama ni kupita kwa helkopta au miguu kama mtakwenda kwa magari yenu, ninataka msafishe mto maji yaende yakachangie upatikanaji wa maji," aliagiza.

Rais Samia pia alimtaka Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwenda kuhakikisha maagizo aliyotoa ya kuunganisha lita 70,000 za maji kutoka Kigamboni kwenda Dar es Salaam yanafanyiwa kazi kwa kuwa fedha tayari zimeshatoka ili kupunguza makali ya uhaba wa maji uliopo.

Alisema Dar es Salaam ina miundombinu mikongwe ya usambazaji maji na mingine ilijengwa wakati mkoa huo ukiwa na watu milioni tatu lakini sasa una wakazi milioni tano.

"Wanaohusika na maji, DAWASA na Wizara ya Maji waangalie pia muunganisho wa maji ndani ya jiji hili kwa sababu ukisoma kazi iliyofanywa, Dar es Salaam ina uwezo wa kupata maji kwa asilimia 100 kuanzia mwaka 2023 lakini bado maeneo mengine wanalia.

"Sababu nyingine ni ujenzi holela, ndani ya Dar es Salaam watu wamejijengea tu kiasi ambacho mabomba hayawezi kupita, mfumo wowote hauwezi, bali ni kuchimba tu visima na kutoa maji kwa watu. Mkuu wa Mkoa wa sekta husika ninataka myasimamie hayo na Waziri Mkuu atawasimamia," aliagiza.

Mkuu wa Nchi alisema utatuzi wa muda mrefu wa uhaba wa maji mkoani humo ni kujenga Bwawa la Kidunda ambalo mkataba wake ulitiwa saini juzi na serikali imeshatenga fedha za kuanza ujenzi wake.

Alisema bwana hilo litachukua muda mrefu kukamilika na itachukua miaka miwili kujaa maji kutegemea mvua itakavyonyesha.

"Lakini, miaka minne mitano, sita mbele Dar es Salaam itakuwa na akiba kubwa ya maji ya kutosha," Rais Samia alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, akitoa salamu za mkoa huo, alimweleza Rais kazi ambayo walielekezwa kuhusu Kigamboni wameitekeleza.


DANISH REFUGEE COUNCIL

## TANGAZO LA ZABUNI

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUINGIA MKATABA WA VIFAA VYA UJENZI, VIFAA KWA AJILI YA MSAADA WA DHARURA NA VIFAA VYA MAJUMBANI.

HIVYO SHIRIKA LA DANISHI LINATANGAZA ZABUNI TAJWA HAPO JUU NA WAZABUNI WAFUATE MAELEKEZO YAFUATAYO.

- USIFUTE KWENYE BEI
- USITUMIE WINO WA MAJI KUSAHIHISHA UNAPOFANYA KOSA.TUMIA KARATASI MPYA
- USIBADILISHE KARATASI ZA ZABUNI KWENDA KWENYE MFUMO WORD/EXCEL,
- ZINGATIA SEHEMU ZA KUSAINI NA KUGONGA MUHURI AMBAZO NI LAZIMA
- USISAHAU KUAMBATANISHA NYARAKA ZINAZOHITAJIKA KAMA VILE KIAMBATISHO A.1, KIAMBATISHO A.2, CHETI CHA KUKUBALI TUZO YA ZABUNI NA KANDARASI, WASIFU WA MUUZAJI NA FOMU YA USAJILI, HALI YA MKATABA WA JUMLA WA DRC, MAELEZO YA KAMPUNI, KANUNI YA MWENENDO WA WASAMBAZAJI WA DRC BAADA YA KUMALIZA SEHEMU ZOTE KAMILI, SAINI, GONGA MUHURI, WEKA TAREHE.

KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAARIKA WAZABUNI KULETA BEI ZAO.

NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA TAREHE 2.11.2022 HADI TAREHE 15.11.2022 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA 0625482649 au BARUA PEPE sadock.kabuko@drc.ngo
ZABUNI ZITAFUNGULIWA HADHARANI TAREHE 17.11.2022 SAA 4:00 ASUBUHI OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI.

UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA RFQ.TZA@DRC.NGO AU KULETA MOJAKWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI.

217126902


# 'Waliokosa mkopo waripoti vyuoni'

**Na Richard Makore,** DODOMA

BUNGE limeagiza serikali kuwarudisha vyuoni wanafunzi wote wenye sifa za kupata mikopo, lakini hawakupata ili waendelee na masomo wakati serikali ikitafuta fedha za ziada kwa ajili yao.

Vilevile, limeagiza uongozi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kufika mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ili kuhojiwa "kwanini inakuwa na kiburi?"

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alitangaza maazimio hayo jana bungeni jijini hapo baada ya wabunge kujadili hoja ya Mbunge wa Biharamulo, Ezra Chiwelesa aliyoiwasilisha baada ya kumalizika kipindi cha 'Maswali'.

Mbunge huyo, katika kujenga hoja yake hiyo, alisema serikali imetenga bajeti kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, lakini anashangaa kuona wanafunzi wengi hawajapata fedha mpaka sasa huku kukiwa na kundi la wanafunzi wenye sifa za kupewa mkopo huo, lakini hawajapangiwa mkopo.

Alibainisha kuna mwanafunzi amesoma Shule ya Sekondari ya Wasichana Msalato, akiwa na ufaulu wa daraja la kwanza kidato cha nne na sita, lakini amenyimwa mkopo wa elimu ya juu.

"Mfumo uliopo utazaa matabaka na ili kuondoa hili, utengenezwe utaratibu wa haraka ili wanafunzi waliokosa mikopo licha ya kuwa na sifa, wapate mikopo," alisema.

Mbunge huyo pia alipendekeza serikali kufumua mfumo uliopo kwa sasa kuhusu mikopo ya elimu ya juu kwa kuwa umekosa tija.

Hoja hiyo ilichangiwa na wabunge 16 kwa rukhsa ya Spika Tulia huku wengi wao wakiinyooshea vidole HESLB kutokana na shida zilizoibuka.

Mbunge wa Viti Maalum, Judith Kapinga, aliitaka serikali iongeze bajeti ya HESLB ili kuwanusuru wananchi maskini ambao wako hatarini kukosa elimu ya juu.

Mbunge wa Nzega Vijijini, Dk. Khamis Kigwangalla, alisema suala la mwanafunzi kupata mikopo ni haki yao, akitaka serikali kutekeleza dhana ya utawala bora kwa kutoa haki hiyo kwa wanafunzi.

Aliitaka serikali kufumua mfumo wa utoaji mikopo ili iwe haki ya kila mtoto aliyesoma na kufaulu vizuri kukopeshwa fedha.

Mbunge wa Geita Mjini, Constantine Kanyasu, akichangia hoja hiyo ya dharura, alitaka serikali kufumua mfumo wa utoaji mikopo ili wanafunzi wenye sifa waipate bila kuzungushwa.

"Nashindwa kuelewa huu mkopo ni huruma, hisani ama ni kitu gani, maana sielewi! Kama mtoto anafaulu kwenda chuo kikuu, lakini anakosa, huu mfumo ni lazima ufumuliwe," Kanyasu alisema huku Mbunge wa Vvawa, Japhet Hasunga akiitaka serikali itoe majibu "ni kwanini wanafunzi wanakosa mikopo ya elimu ya juu?" Na itoe fedha za dharura ili kutatua tatizo hilo.

Mbunge wa Korogwe Vijijini, Timotheo Mzava, alisema katika bajeti ya mwaka huu, wanafunzi 30,000 watakosa mikopo na kuomba ufanyike uchunguzi ili kubaini sababu.

Mbunge wa Viti Maalum, Ester Matiko aliitaka serikali kuwekeza katika elimu na kuwe na chanzo maalum cha fedha kama ilivyo kwa Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Ester alisema wanafunzi wanaopata daraja la kwanza kidato cha sita, wasomeshwe bure na wale wengine wakopeshwe, akisisitiza kuwa suala hilo linawezekana kwa kuwa wazazi wao walisoma bure.

Mbunge wa Mbulu Vijijini, Flatei Massay alisema kwa sasa hali ni mbaya HESLB, hivyo kuna haja bodi hiyo ivunjwe kwa kuwa imeshindwa kufanya kazi yake vizuri kwa kipindi kirefu tangu ilipoundwa.

Akihitimisha hoja yake, Mbunge Chiwelesa aliitaka serikali kutoa tamko ili wanafunzi waliokosa mikopo, warudi vyuoni wakati serikali inatafuta fedha.

Pia aliitaka serikali kupeleka bungeni bajeti ifanyiwe mapitio ili kuongeza bajeti kwa kuwa inaonekana shida ni fedha na kuundwe kamati teule ya Bunge ili kuichunguza HESLB kwa kuwa malalamiko yamekuwa mengi.

### MAAZIMIO YA BUNGE

Kutokana na hoja hiyo, Spika Tulia alisema Bunge kwa kauli moja linaitaka serikali kuwasiliana na vyuo ya serikali na binafsi kuwapokea wanafunzi hao.

Spika Tulia pia aliagiza uongozi wa HESLB ufike mbele ya Kamati ya Bunge ili kuzungumza nayo, akitamka: "Ninataka bodi hii ifike mbele ya kamati hii Ijumaa hii ili tuone kama ni kiburi inafanya ama ni kitu gani".

Uamuzi wa kuitwa kwa uongozi wa HESLB ulitokana na kauli ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda kwamba bodi hiyo imekuwa na kiburi, ilipowagomea wataalamu aliowatuma kuichunguza, ikiwazuia kufanye kazi yao.

"Nimeunda kamati ya wataalamu kuchunguza mifumo ya bodi, lakini ninapata upinzani mkali sana mpaka ninashangaa," Prof. Mkenda alisema.

Katika kujibu hoja ya dharura ya Mbunge Chiwelesa, Waziri Mkenda serikali inafanya mazungumzo na Hazina ili kupata fedha kwa ajili ya kuwapa mikopo wanafunzi waliokosa mwaka huu.

Katika mwaka wa masomo 2022/23, serikali imetenga bajeti ya Sh. bilioni 573 kwa ajili ya kutoa mikopo na ufadhili kwa wanafunzi wa elimu ya juu nchini.

HABARI KITAIFA

# Bei ya mafuta yashuka tena

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imetangaza kushuka tena bei ya petroli na dizeli kutokana na serikali kuendelea kuweka ruzuku.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na EWURA, bei ya rejareja ya mafuta ya petroli kwa Bandari ya Dar es Salaam ingeongezeka kwa Sh. 110 kwa lita na kwamba ruzuku ya Oktoba iliyopo imesaidia bei zisipande.

"Bei ya mafuta ya rejareja ya dizeli kwa Dar es Salaam na Tanga kwa Novemba mwaka huu imepungua kwa Sh. 31 na 34 kwa lita kulinganishwa na Oktoba 2022. Kwa Mtwara hakuna meli imehusishwa kwenye bei kwa Novemba mwaka huu na mafuta yake yatatumika Desemba," EWURA ilifafanua kupitia taarifa hiyo iliyotiwa saini na Mkurugenzi Mkuu, Modestus Lumato.

Alisema mabadiliko ya bei kwa mwezi huu kwa Mtwara ni kwa ajili ya kuhuisha taarifa sahihi ya meli husika iliyotumika kwenye bei za Oktoba.

Kwa upande wa mafuta ya taa na ya petroli kwa Tanga imepungua kwa Sh. 164 na Sh. 118 kwa lita kulinganishwa na zilizopita kwa sababu ya wastani wa bei ndogo zaidi ya mafuta yaliyosafirishwa katika soko la dunia na gharama za usafirishaji kwa Bandari ya Tanga.

Kutokana na kushuka kwa bei hizo, Dar es Salaam yatauzwa Sh. 2,889 kutoka Sh. 2,996 huku dizeli ikiuzwa Sh. 3,052 kutoka Sh. 3,197 kwa lita.

Lumato alisema ruzuku kwenye kila lita ni Sh. 110 kwa petroli na Sh. 145 kwa dizeli.

Kwa Tanga, lita moja ya petroli itauzwa kwa Sh. 2,806 na dizeli Sh. 3,074 huku Mtwara ikiwa ni Sh. 2,917 na 3,096.

"Wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa rejareja na jumla wanatakiwa kuuza kwa bei yenye ruzuku, hatua kali zitachukuliwa kwa atakayekiuka," alionya.

Kwa mabadiliko hayo, Wilaya ya Kyerwa (Ruberwa) mkoani Kagera iliyokuwa inanunua mafuta kwa Sh. 3,234 kwa lita ya petroli, sasa itanunua kwa Sh. 3,290, huku dizeli iliyokuwa Sh. 3,435 kwa lita, sasa itauzwa Sh. 3,290.

# Samia ataka kikosi kazi nishati safi ya kupikia

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameagiza kuanzishwa kwa kikosi kazi cha taifa kitakachochakata sera na kuja na afua ya nishati safi ya kupikia na kulitoa taifa kwenye matumizi ya sasa ya nishati zisizo safi na salama.

Aliagiza hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa Mjadala wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia ulioandaliwa na Wizara ya Nishati na kuhudhuriwa na washiriki zaidi ya 3,000.

Akifungua kongamano hilo la siku mbili lililokutanisha wadau wa sekta hiyo, Rais alitaka kikosi kazi hicho kihusishe watu kutoka serikalini, sekta binafsi na wadau wa maendeleo na kichambue sera za serikali na mapendekezo ya wadau.

Aliagiza kikosi kazi hicho kiongozwe na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na kuratibiwa na Wizara ya Nishati ambayo Waziri wake ni January Makamba.

Rais alisema kikosi kazi hicho kitakuja na mpango mkakati ambao utaiongoza serikali, sekta binafsi na wadau wa maendeleo kutafuta suluhu ya nishati safi na endelevu ya kupikia.

"Mkachakate sera zetu, mje na afua zitakazotekelezeka, kuliko kila mmoja kufanya lake, takwimu zinaonyesha kaya zinazopikia kwa kutumia mitungi ya gesi ni asilimia tano, umeme asilimia tatu na nishati nyingine safi asilimia 2.2. Bado tuna kazi ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi na salama," aliagiza.

Rais Samia alisema wanapaswa kuwa na mkakati wa kisera na kibajeti pamoja na kuweka mazingira wezeshi katika kutatua shida katika upatikanaji wa nishati safi kwa kushirikiana na sekta binafsi.

**MFUKO NISHATI SAFI**

Rais Samia pia alisema serikali imejipanga kutenga fedha kwa ajili ya uanzishwaji wa mfuko maalum kwa ajili nishati safi ya kupikia ambazo zitaanza kutengwa katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha kwa lengo la kumtua mama mzigo wa kuni kichwani.

Alibainisha kuwa wakati akiwa Makamu wa Rais, aliweka lengo la kumtua mama ndoo kichwani ambalo amelitimiza kwa asilimia 80, licha ya kuwapo kikwazo cha mabadiliko ya tabianchi unaosababisha upatikanaji wa maji kushuka.

"Nitajisikia fahari ikifika 2032 Tanzania hii iwe na nishati ya kupikia kwa asilimia hizo 80 au 90 kama sio zote," alisema.

Waziri wa Nishati, January Makamba aliwaeleezea mabinti wawili Juliana (11) na Joyce (13) wa familia moja wanaoishi na baba yao namna wanavyotumia muda wao mwingi kuokota kuni kwa matumizi ya nyumbani na kuuza mzigo mmoja kwa Sh. 1,000 ili kujipatia fedha za chakula.

Katika mdahalo huo wa kitaifa Rais alishuhudia majadiliano yaliyoendeshwa na Waziri Makamba, yakihusisha hali ya sasa ya nishati ya kupikia ambapo Waziri mstaafu, Prof. Anna Tibaijuka alisema ili kukabiliana na gharama ya nishati safi, serikali ihakikishe inaweka sera na sheria itakayosimamia bei za nishati hizo kuwa himilivu sokoni.

Alisema bei ya mitungi midogo ya gesi imepanda kutoka Sh. 18,000 mpaka Sh. 24,000.

Daktari wa Magonjwa ya Mapafu kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Pauline Chale, alitoa ushuhuda namna wanawake wenye umri wa miaka 66, mmoja akipoteza maisha mwezi uliopita, waliokuwa wamelazwa hospitalini huko kwa matibabu baada ya kupata maradhi ya kushindwa kupumua kutoka na kutumia kwa muda mrefu nishati isiyo safi huku gharama ya matibabu zikiwa kubwa.

# Mama adaiwa kuchoma moto wanawe kisa kula kwa jirani

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKAZI wa Kijiji cha Nyombo wilayani Njombe, Adelina Ngolo (36), anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kuwachoma moto watoto wake wawili, wanaodaiwa kwenda kutafuta chakula kwa majirani.

Imedaiwa kuwa aliwachoma watoto wenye umri wa miaka saba na minne sehemu mbalimbali za mwili na mikono.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 28, mwaka huu, majira ya saa nne usiku.

Alisema, chanzo cha watoto hao kuchomwa moto ni kuzunguka kwa majirani kutafuta chakula.

"Majirani walimuita huyu mama na kumwambia malezi ya watoto sio haya, watoto wamekua ombaomba, yeye akayaweka moyoni alipofika nyumbani kwake usiku aliwaamsha na kuwachoma moto alioutoa kwenye jiko la kuni. Watoto hao wameungua vibaya mikononi na sehemu nyingine za mwili," alisema Kamanda Issah.

Kamanda alisema, walipomuhoji mama huyo alijitetea kuwa amewachoma kwa sababu wameshindwa kumlea mdogo wao mwenye umri wa mwaka mmoja.

"Jaribu kufikiri kweli watoto wenye miaka saba na miaka minne wanaweza kumlea mtoto wa mwaka mmoja ambaye mama mwenye watoto watatu yeye ameshindwa kuwalea na kuwaacha wanakua ombaomba," alihoji.

Alisema jambo hilo linasikitisha na halikubaliki. "Wananchi wa Njombe amkeni muache kuwaachia watoto walee watoto wenzao, haitawezekana kwa sababu mnaweza mkasababisha ukatili dhidi yao, mama amefanya ukatili kitendo hiki hakikubaliki," alisema.

Kamanda alisema, wanakijiji wamejitolea kuwalea watoto hao ili mama huyo achukuliwe hatua za kisheria. "Viongozi wa vijiji, vitongoji leteni taarifa za ukatili ili tuweze kuchukua hatua zinazostahili mfano huyu mama baada ya kuwachoma aliwafungia katika chumba mpaka mwananchi aliyesikia uchungu alitoa taarifa na wamekutwa watoto wakiwa taabani wameungua, sijui alitaka wapoteze maisha," alihoji Kamanda Issah.



## SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
## MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF)

# Miaka miwili ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi madarakani na mafanikio ZSSF

NDANI ya miaka miwili ya uongozi wa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) umefanikiwa kukusanya Sh. 10,911,476,425.56 zinazotokana na miradi mbalimbali iliyonayo ikiwamo kiwanja cha kufurahishia watoto Kariakoo.

Pia mfuko huo umefanikiwa kupata wanachama wapya 8,625 ambao wamejiunga na mfuko huo kutoka wanachama 104,837 ambao walikuwa nao kabla ya miaka miwili ya uongozi wa Dk. Mwinyi na kufikisha idadi ya kuwa na wanachama 113,463.

Katika mazungumzo na Nipashe ofisini kwake Kilimani mjini Unguja, Mkurugenzi Mipango na Uwekezaji wa ZSSF, Khamis Filfil Thani anasema mafanikio hayo yanatokana na juhudi za viongozi wa serikali na watendaji wa mfuko huo.

Anasema kazi za msingi za mfuko huo ni kuihifadhi jamii ambayo imeajiriwa katika ajira rasmi iwe ya taasisi za serikali au taasisi binafsi ili kuikinga kutokana na majanga yatakayosababishwa na shughuli za kikazi yakapelekea mwajiriwa kutoweza kufanya tena shughuli za kazi na ikamsababishia kutopata kipato au ikampunguzia uwezo wa kufanya kazi. "Yawezekana asiweze kufanya shughuli zake za kazi kutokana na kupata maradhi, kuzeeka, kifo au ikimpunguzia uwezo wake wa kufanya kazi kwa kupata ujauzito," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema ZSSF ina mafao manne ambayo ni ya: Uzee; kifo; uzazi; na fao ambalo mtumishi hawezi kufanya tena kazi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo maradhi kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Vilevile, anasema katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Dk. Mwinyi, kuna mambo ambayo wameainishiwa katika ibara ya 220 ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuhakikisha wanasimamia shughuli za hifadhi ya jamii kwa manufaa ya wanachama wote na taifa kwa ujumla.

Mkurugenzi huyo anasema katika ibara hiyo, pia wameainishiwa kufuata sheria na panapokuwa na tatizo la kisheria kufanya marekebisho ili kukidhi haja ya wananchi na wanachama kwa ujumla.
Anasema mwaka jana walifanya mapitio ya marekebisho ya sheria ya kutoa mafao mapya na mwaka huu pia wamefanya marekebisho ya sheria na sera za hifadhi ya jamii ili kuendelea kuwahudumia vizuri zaidi wananchi na wanachama wa mfuko huo.

Anaeleza mafanikio mengine yaliopatikana ndani ya miaka miwili ya uongozi wa Dk. Mwinyi, ni kujenga majengo ya makazi na biashara katika eneo la Mombasa Unguja ambapo hivi sasa wapo katika hatua ya kuandaa mkataba na kumweka mkandarasi .

"Tayari tumeshapata mshauri elekezi wa kuchora mchoro wa majengo hayo na umeshathibitishwa kwa ajili ya kutumika na tayari tumeshatoa zabuni ya ujenzi na kwa sasa tupo katika hatua ya mwisho za kutia saini mkataba na kuwa na mkandarasi," anasema.

Anaongeza kuwa lengo ni kuwa na makazi bora na kwamba majengo hayo yatakuwa ya bei nafuu ili wanachama wa ZSSF na wananchi waweze kununua nyumba hizo.

Anasema malengo yaliowekwa katika ilani ni kuongeza wigo wa wanachama wao kwa asilimia 50 kwa muda wa miaka mitano na kwa sasa katika miaka miwili hii wamefanikiwa kusajili wanachama wapya kwa asilimia 70.

Anasema usajili wa wanachama wapya kwa mwaka huu umezidi kuongezeka baada ya kupungua kwa janga la maradhi ya UVIKO-19 kutokana na wanachama wao wengi hasa katika sekta ya utalii kupoteza ajira.

Anasema wamefanikiwa kufungua ofisi katika mikoa minne ya Unguja na Pemba ili kuwarahisishia wanachama na wananchi kupata huduma kwa haraka na wamefanikiwa kuazisha mafao mawili mapya hasa kwa wale wanachama wao wanaopoteza ajira kupata mafao yao na fao la fidia kwa wafanyakazi wanaoumia kutokana na kazi.

Mkurugenzi huyo anasema tayari sheria sasa imeshatambua kuwapo kwa mafao hayo ambayo yatatumika kwa wanachama wa mfuko huo.

Akizungumzia fao la uzazi, mkurugenzi huyo anasema wanufaika wake ni kinamama wanaojifungua na mwitiko ni mkubwa na wamevuka malengo waliyoyaweka katika fao hilo na kuna wimbi kubwa la wanachama wao waliopata fao hilo.

"Kwa mwanachama anayejifungua anapata fao la wastani wa Sh. 180,000 na anayejifungua pacha hupata mara mbili yake," anasema.

Akizungumzia vikwazo vinavyowakabili, mkurugenzi huyo anasema waajiri na wajiriwa hawataki kukatwa mafao kwa sababu hawajui manufaa yake baada ya kumaliza muda wa utumishi na ndio maana kuwapo kwa ZSSF ni suala la kisheria na ambaye hataki huchukuliwa hatua za kisheria kwa lengo la kulinda maslahi ya wanachama.

Anasema pia wanakabiliwa na shida ya uelewa kwa wanachama na wananchi kuhusu mfuko huo lakini wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi kukabiliana na kikwazo hicho.

Hata hivyo, mkurugenzi huyo anawataka wale wote ambao hawajajiunga na mfuko huo kujiunga na wale ambao waliojiunga kufuatilia taarifa zao ili kujua kuwa zinafika kwa manufaa yao ya baadaye kwa sasabu ZSSF imejipanga kulipa mafao mapema baada ya mwanachama wa mfuko huo kustaafu kazi ama kupatwa na janga lolote lililomo ndani ya Sheria ya Mfuko.

# SALAMU ZA PONGEZI

KISHINDO CHA
MIAKA
**OFISINI** **2**

**Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa**
**MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF)**
**wanaungana na Watanzania wote kumpongeza**
**Mheshimiwa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutimiza miaka miwili ofisini kwa mafanikio Makubwa .**
**Hongera sana.**



Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi

# Zumaridi adai kuibwa milioni 19/- na askari polisi wakati akikamatwa

**Na Pelucy Yohana,** SAUT

MSHTAKIWA Diana Bundala (40), maarufu Mfalme Zumaridi, amedai katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza kuwa wakati wa ukamataji wa askari katika chumba chake, zimeibwa Sh. milioni 19.5 na simu mbili baada ya yeye kutolewa nje.

Alidai hayo mahakamani huko jana alipowasilisha utetezi wake katika kesi inayomkabili na wenzake 83, kuhusu utata wa saini yake katika maelezo ya onyo.

Zumaridi alidai kuwa siku ya tukio hilo, alivamiwa na askari waliokuwa hawajavalia sare za polisi kinyume cha maelezo yaliyowasilishwa mahakamani.

Mshatikiwa huyo namba moja alidai kuwa kipindi cha ukamataji Februari 26 mwaka huu, askari walimvamia katika chumba chake na kumtoa nje huku wao wakiendelea kukagua chumbani huko bila kuwapo kwake.

Alidai askari hao hawakusema sababu ya ukaguzi huo pamoja na kutolewa nje, hatua iliyosababisha askari hao kuchangia upotevu wa fedha hizo na mali zake nyingine ndani ya chumba chake.

Shahidi mwingine katika kesi hiyo, Neema Julian (36) alidai askari walipofika eneo hilo, walivamia nyumba hiyo na kupiga mabomu ya machozi pamoja na kupiga watu waliokuwamo kwenye ngome hiyo, kitendo kilichozua taharuki kwa waumini hao.

Shahidi mwingine, Diana Michael (26) alidai wakati anafika katika eneo hilo, alikuta askari hao wameishavamia eneo hivyo naye alianza kushambuliwa na askari hao baada ya kujulikana kuwa ni miongoni mwa waumini.

Kesi hiyo iko chini ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Clescensia Mushi ambaye anatarajiwa Novemba 9 mwaka huu kutoa uamuzi kuhusu utata ulioibuka ili kuendelea na ushahidi wa kesi ya msingi.


SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI ZANZIBAR

SALAMU ZA PONGEZI

KISHINDO CHA MIAKA 2 OFISINI

Uongozi na wafanyakazi wa WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI ZANZIBAR wanaungana na Watanzania wote kumpongeza Mheshimiwa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutimiza miaka miwili ofisini kwa mafanikio Makubwa. Hongera sana.



Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi

S.L.P 394 Mazizini, Zanzibar, SIMU: +255 24 223 2827
TOVUTI: info@moez.go.tz

17128702



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI

TANGAZO

USAJILI WA TAASISI, KAMPUNI NA WATAALAM BINAFSI WANAOFANYA KAZI ZA UTAFITI NA UCHIMBAJI WA VISIMA VYA MAJI CHINI YA ARDHI KWA MUJIBU WA SHERIA YA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA MAJI NA.11 YA MWAKA 2009 PAMOJA NA MAREKEBISHO YAKE NA. 8 YA MWAKA 2022

Wizara ya Maji inazitaka Taasisi, Kampuni na Watu binafsi wanaofanya kazi za utafiti na Uchimbaji wa maji chini ya ardhi ambao bado hawajajisajili, kuhakikisha wanajisajili ndani ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya tangazo hili.

Kufanya kazi za utafiti na uchimbaji wa visima vya maji chini ya ardhi bila ya kusajiliwa na Wizara ya Maji ni kosa linalopaswa kuadhibiwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2022.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa simu nambari: **+255 713 396 591** au kwa barua pepe: **dwr@maji.go.tz**, au fika katika ofisi za Idara ya Rasilimali za Maji zilizopo Barabara ya Ali Hassan Mwinyi karibu na Ofisi za Makao Makuu ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA). Pia unaweza kufika kwenye Ofisi za Bodi za Maji za Mabonde na Ofisi ndogo za Bodi za Maji za Mabonde zilizopo katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Dkt. George V. Lugomela
**MKURUGENZI**
**IDARA YA RASILIMALI ZA MAJI**
**Wizara ta Maji,**

**Idara ya Rasilimali za Maji,**
**Makao Makuu Dodoma,**
**41104 Tambukareli, DODOMA**

www.maji.go.tz
dwr@maji.go.tz

17128102

**Nipashe** MWANGA WA JAMII

# Takwimu za sensa zitumike vizuri kulisaidia taifa

**IDADI** ya watu nchini sasa imejulikana baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, juzi kutangaza matokeo ya mwanzo ya Sensa ya Watu na Makazi, iliyofanyika mwezi Agosti, mwaka huu.

Sensa hufanyika nchi nyingi duniani ili kupata idadi kamili ya watu na kuisaidia serikali kujua namna ya kupanga bajeti kwa ajili ya maendeleo ya nchi husika.

Kwa mujibu wa Rais Samia, wakati akizindua matokeo hayo juzi, idadi ya watu milioni 61.7 kwa nchi ni mzigo mkubwa unaohitaji mikakati na mipango ya maendeleo ya kuwahudumia.

Umuhimu wa kufanyika kwa sensa hiyo sasa umeanza kuonekana kwa kuwa idadi ya watu walioko ni kuonesha ipo kazi kubwa ya kupanga mipango ya kuwahudumia na vile vile kuhakikisha ustawi wa maendeleo yao.

Serikali sasa itakuwa na uwezo wa kupanga bajeti yake kwa kutambua kulingana na idadi ya watu walioko ili kujua ni vituo vingapi vya afya vinavyohitajika, shule, huduma za kijamii kama masoko na shughuli zingine zinazohusu maisha ya watu.

Kwa mujibu wa sensa hiyo, idadi ya wanawake ni 31,687,990 na wanaume ni 30,053,130.

Idadi ya watu inapoongezeka kuna faida na hasara. Faida huja kwasababu nguvukazi ya uzalishaji mali huongezeka na uchumi wa nchi hukua.

Lakini ongezeko hilo pia linaweza kuwa mzigo kwa sababu serikali inabidi iongeze bajeti kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma zote muhimu ikiwamo ya afya, elimu, makazi, umeme na maji.

Watu wanapoongezeka na makazi hupanuka kwa kuwa watu huongeza maeneo ya kuishi. Ndio maana katika baadhi ya sehemu, kwa mfano mkoa wa Pwani na Dar es Salaam kwa sasa huwezi kukuta misitu mikubwa kwa sababu wananchi wanaendelea kujenga na kulima na hatimaye kuunganisha mikoa hiyo.

Wataalamu wanasema idadi ya watu inapoongezeka kwa asilimia 3.2 kwa kipindi cha miaka 10 tangu sensa ya mwaka 2012 ilipofanyika, kunatakiwa kuhakikishwa kuwa barabara zinaongezeka kwa angalau asilimia tatu, shule, vituo vya afya vyote viongezeke kulingana na idadi ya watu watakavyokuwa wameongezeka.

Mtaalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Pius Yanda, anasema ongezeko hilo la watu litasababisha uhitaji mkubwa wa huduma za kijamii ikiwamo maji, ardhi na chakula ambavyo upatikanaji wake umeshaanza kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

Anasema kutokana na ongezeko hilo la watu, ni wazi sehemu kubwa ya ardhi itatumika kwa ajili ya kilimo, ikizingatiwa kuwa asili ya kilimo nchini imejikita zaidi kwenye ardhi kwa kuwa jamii haina uwezo wa kulima kisasa.


Ukirudi katika sekta ya afya, daktari katika kituo cha afya, Daudi Zimulinda, anasema ongezeko hilo la watu linachangia gharama za utoaji wa huduma za afya na bajeti ya serikali kwenye sekta hiyo itolewe kwa wingi ili kupunguza magonjwa ya mlipuko na mengine ili kusaidia vituo visizidiwe na wagonjwa.

Vivyo hivyo, katika elimu majengo ya shule lazima yaongezeke kulingana na idadi ya watu walioko ili kuhakikisha hakuna anayebaki na ujinga wa kukosa elimu.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com


## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Mbinu za kidijitali ziokoe wanafunzi

**RUSHWA** ya ngono imekuwa ikitajwa kushamiri katika shule za msingi, sekondari na vyuo na kusababisha baadhi ya wanafunzi wa kike kushindwa kutimiza ndoto zao walizojiwekea kupitia elimu.

Kushamiri kwa rushwa hiyo kunawafanya wadau wanaoipiga vita wanaungana na serikali katika harakati za kuikomesha, kwa kuja na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha wanafunzi wanasoma na kuhitimu masomo yao bila usumbufu.

Miongoni mwa wadau hao, ni shirika lisilo la kiserikali la C-SEMA ambalo linawaelekeza wanafunzi kupiga vita rushwa hiyo kidigitali kwa kutumia simu kutoa taarifa za matukio hayo ya ukatili ili zifikishwe mahali husika haraka.

Ni katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike yaliyofanyika viwanja vya Shule ya Sekondari Makumbusho Dar es Salaam wiki iliyopita, mwezeshaji kutoka shirika hilo, Dominic Vitus anasema hayo.

Anaelekeza wanafunzi kutumia namba 116 kutoa taarifa zote za ukatili wa kijinsia ikiwamo rushwa ya ngono, ili shirika hilo liwaunganishe na wadau kama ustawi wa jamii na polisi kwa ajili ya kuchukua hatua sheria.

Wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, hawaruhusiwi kumiliki simu, lakini wanaelekezwa kutoa taarifa za rushwa hiyo kwa wazazi, walezi au ndugu zao wa karibu, wapige namba hiyo waunganishwe ili zichukuliwe haraka.

Si kwa hao tu bali wanafunzi pia wanaweza kutoa taarifa za rushwa hiyo kwa walimu wao ili wapige namba hiyo, kwani hatua hiyo ya kupaza sauti inaweza kuwaokoa dhidi ya rushwa hiyo ambayo inadaiwa kushamiri.

Ikumbukwe kuwa ukimya unaweza kuchangia kuendelea kuwapo kwa rushwa hiyo miongoni mwao, kwa kuwa wamepewa namba ya kupiga ili kuwaripoti wanaoashiria kuwafanyia ukatili huo, basi hiyo ni fursa nzuri waitumie. Pamoja na hayo, ni vyema pia wanafunzi wakaungana kama mabinti shuleni vyuoni waongelee changamoto wanazokumbana nazo, kwani kwa njia hiyo wanaweza kugundua kuwa wanapitia mambo yanayofanana.

> **Vyombo vya sheria vipo, vinawalinda dhidi ya ukatili huo wa rushwa ya ngono, hivyo ingependeza kama wanafunzi wa kike kwa umoja wao watapaza sauti badala ya kuumia kimya kimya na kujihisi hawana msaada.**

Kwa njia hiyo, ninaamini kuwa wao wenyewe wanaweza kujiwekea mikakati ya pamoja ambayo itawasaidia kushinda kirahisi vita hiyo, hasa kwa kuzingatia kwamba umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Vyombo vya sheria vipo, vinawalinda dhidi ya ukatili huo wa rushwa ya ngono, hivyo ingependeza kama wanafunzi wa kike kwa umoja wao watapaza sauti badala ya kuumia kimya kimya na kujihisi hawana msaada.

Kimsingi, njia zipo nyingi za kupambana na rushwa hiyo ikiwamo ya kidigitali ya kupiga simu namba 116, ili kuunganishwa na taasisi za serikali, kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria, ninadhani ni vyema wanafunzi kuchukua hatua.

Lakini, waandaaji wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike ambao ni Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), wanapongeza hatua ya vita ya rushwa ya ngono kufanyika kidigitali.

Ninadhani pamoja na pongezi hizo, walengwa nao wangechangamkia fursa hiyo na kuitumia kwa usahihi ili iweze kuleta matokeo chanya na siyo watu kukwaruzana kwa mambo mengine anasingiziwa rushwa ya ngono.

Iwapo chuki binafsi hazitaingizwa kwenye vita hiyo, ninaamini wanaotaka rushwa ya ngono kwa wanafunzi wanaweza kukamatwa kirahisi na kuchukuliwa hatua za kisheria hatimaye kutokomeza ukatili huo kwao.

Kama ilivyo kaulimbiu ya WAJIKI katika vita hiyo kwamba; 'Safari salama bila rushwa ya ngono inawezena', ninaamini pia kwamba vita ya rushwa kidigitali inaweza kuzaa matunda ikitumika inavyotakiwa.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

# MWITO WA KUTOA MAONI

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.**

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Dalasho Enterprises Limited – Del Oil, S. L. P 32164, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 541, Kitalu 'A' Eneo la Ipazi, Nzega, Tabora. | Ibrahim Mohamed Bashe (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 2. | Nicholaus George Ngassa T/A Galaxy Petroleum, S.L.P 19, Igunga. | Kiwanja No.236, Kitalu "B', Eneo la Hanihani, Igunga, Tabora. | Nicholaus George Ngassa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 3. | Gobsan Campany Limited Itobo, S.L.P 32164, Dar es Salaam. | Kiwanja No.1, Kitalu "X', Eneo la Itobo, Nzega, Tabora. | Ibrahim Mohamed Bashe (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 4. | Majid Masoud Ally, S.L.P 1061, Tabora. | Kiwanja No.501, Kitalu "D", Eneo la Ipuli, Tabora. | Majid Masoud Ally (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 5. | Gobsan Company Limited, S. L. P 32164, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 541, Kitalu "D" Eneo la Ipazi, Nzega, Tabora | Ibrahim Mohamed Bashe (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 6. | CG Traders, S. L. P 2207, Tabora. | Mtaa wa Sokoni, Kata ya Gongoni, Tabora. | Charles George (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa gesi ya kupikia (LPG) |
| 7. | JM Couriers (T) Limited Petrol Station Ikungi, S.L.P 42051, Dar es Salaam. | Kiwanja No.65, Kitalu "C", Eneo la Ikungi, Singida. | Msafiri Rashid Kitemangu (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 8. | FAB International Limited-Rungwa, S.L.P 70419, Dar es Salaam. | Kijiji cha Rungwa, Manyoni, Singida | Farid Ahmed Bazar (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 9. | Puma Kisasa Service Station, S.L.P 9043, Dar es Salaam. | Kiwanja No.59, Kitalu "E', Eneo la Kisasa, Dodoma. | Lameck Hiliyai (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 10. | Puma Hazina Service Station, S.L.P 9043, Dar es Salaam. | Kiwanja No.260, Kitalu "27', Eneo la Hazina, Dodoma. | Lameck Hiliyai (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 11. | Total Energies Marketing Tanzania Limited, S.L.P 1503, Dar es Salaam | Kiwanja No.342, Kitalu "X', Eneo la Hazina, Dodoma. | Jean Francois Schoepp (Mbelgiji) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 12. | Ibrahim Mohamed Ibrahim – Mambo Mazuri Petrol Station, S.L.P 95, Tunduru. | Kiwanja Na. 1, Kitalu, "P", Nakayaya Mashariki, Tunduru, Ruvuma | Ibrahim Mohamed Ibrahim (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 13. | Cross Road Filling Station, S.L.P 230, Tunduru. | Kiwanja Na. 122, Kitalu "A", Tunduru, Ruvuma. | Saleh Tawred Ahmed (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 14. | PetroAfrica (T) Limited – Makambako Service Station, S.L.P 4878, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.7, Kitalu "H", Ubena – Makambako, Njombe | Yassin Hersi Warsame (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 15. | Joseph Faustin Kawogo, S.L.P 174, Njombe. | Kijiji cha Madobole, Njombe | Joseph Faustin Kawogo (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 16. | Ntanyinya Filling Station – Mkwajuni, S.L.P 101, Chunya. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "Y", Mkwajuni, Songwe. | Fidelis Ntanyinya (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 17. | AFM HASHI Company Limited, S.L.P 256, Sumbawanga. | Kiwanja Na. 422 & 423, Kizwite, Sumbawanga, Rukwa. | Abdi Mohamed (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 18. | Fredrick Kijana Tweve, S.L.P 13440, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1004, Kitalu "D", Mbalizi, Mbeya. | Fredrick Kijana Tweve (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 19. | Canuck Company Limited, S. L. P. 472, Shinyanga. | Kijiji cha Magung'humwa, Msalala, Shinyanga. | Chad David Beattie (Muafrika Kusini) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 20. | Jambo Petroleum Products Limited, S.L.P 71, Shinyanga. | Kiwanja Na. 91C, Kitalu 'S', Uzunguni, Shinyanga | Seleman Khamis Al-Amri (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 21. | New Javas Oil and Tours Tanzania Limited, S.L.P. 112, Karagwe. | Kijiji cha Kihanga, Karagwe, Kagera. | Jamal Tindamanyile Chamani (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 22. | Nekemia Phillimon Tiigwera, S.L.P. 61, Karagwe. | Kijiji cha Kihanga, Karagwe, Kagera. | Nekemia Phillimon Tiigwera (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 23. | Samira Khalfan Amour, S.L.P. 70, Biharamulo. | Kijiji cha Kikoma, Biharamulo, Kagera. | Samira Khalfan Amour (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 24. | Mipawa Kasiga Lukamaja T/A Gaha Oil, S.L.P. 11156, Mwanza. | Kijiji cha Busolwa, Nyang'hwale, Geita. | Mipawa Kasiga Lukamaja (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 25. | Domician Nyambi Mkufu, S. L. P. 139, Geita | Kijiji cha Ntinachi, Nyamilimilwa, Geita. | Domician Nyambi Mkufu (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 26. | Kayonza Limited, S.L.P. 972, Mwanza. | Kiwanja Na.229, Kitalu "B", Eneo la Nyegezi, Mwanza. | Oliver James Kashaga (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya Kupikia ya LPG |
| 27. | Pius Felix Sizza, S.L.P. 1081, Musoma. | Kijiji cha Nyamuswa, Bunda, Mara. | Pius Felix Sizza (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 28. | Leonia Joseph Makubi, S. L. P. 281, Busega. | Kijiji cha Kabita, Busega, Simiyu. | Leonia Joseph Makubi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 29. | Kitema Oil Investment, S.L.P. 280, Kasulu. | Kijiji cha Nyanga-Muyama, Buhigwe, Kigoma. | Emmanuel Joas Gwisembeza (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 30. | Sayona Chemicals Limited, S.L.P 5478, Tanga. | Kiwanja Na. 24, Kitalu "F", Eneo la Viwandani Amboni, Tanga. | Kumar Vinodrai Pujara (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 31. | GBP (T) Limited – KIA Service Station, S.L.P 3728, Dar es salaam. | Kiwanja Na. 690 na 691, Kitalu "E", Bomang'ombe, Hai, Kilimanjaro. | Badar Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 32. | China Railway Seventh Group Co. Limited, S.L.P. 23480, Dar Es Salaam. | Eneo la Visiga, Kibaha, Pwani. | Xuanyao Xu (Raia wa China) | Leseni ya Mafuta kwa matumizi binafsi |
| 33. | Gp Global Energy Services (T) Limited, S.L.P. 7387, Pwani. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "T", Eneo la Visiga, Kibaha, Pwani. | Manan Goel (Raia wa India) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 34. | Msuri Petroleum Tanzania Limited, S.L.P 474, Chemba. | Kiwanja No. 5, Kitalu "H', Eneo la Chamakweza, Chalinze, Pwani. | Sanda H. Sanda (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 35. | GBP (T) Ltd – Kibaha Service Station, S.L.P 3728, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 50, Eneo la Mkuza, Kibaha, Pwani. | Badar Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 36. | Ahmed Abdallah Bakhamis T/A Happy Oil, S.L.P 20, Morogoro. | Kiwanja Na.13, Kitalu "A", Eneo la Ngugu, Kisarawe, Pwani. | Ahmed Abdallah Bakhamis (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 37. | Abdulqadir Ally Qullaten T/A Tash Oil Kilindoni, S.L.P 10731, Dar es Salaam. | Kijiji cha Kilindoni, Mafia, Pwani. | Abdulqadir Ally Qullaten (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 38. | Difre and Associates Limited, S.L.P 3633, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 190, Mikocheni, Kinondoni, Dar es Salaam. | Lusekelo Mwandemange (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya mafuta |
| 39. | Aim Steel Limited, S.L.P 60693, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 4, Eneo la Mbezi Juu, Kinondoni, Dar es Salaam. | Nikhil Patel (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 40. | Top Oil Petroleum Limited - Mbezi Luis, S.L.P. 42445, Dar es Salaam | Kiwanja Na.422 na 424, Kitalu "A", Eneo la Mbezi Luis, Ubungo, Dar es Salaam. | Mbaraka Sakim Bawazir (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 41. | Uno Petroleum Tanzania Limited, S.L.P 14113, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P20509, Eneo la Kunduchi Mtongani, Kinondoni, Dar es Salaam. | Ravilal Devji Vekaria (Raia wa India) | Leseni ya kituo ya mafuta |
| 42. | Uno Petroleum Tanzania Limited, S.L.P 2860, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P707, Eneo la Yombo Vituka, Temeke, Dar es Salaam | Ravilal Devji Vekaria (Raia wa India) | Leseni ya kituo ya mafuta |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Barua Pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: www.ewura.go.tz**

**Namba ya Bure 0800110030**

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**EWURA**

# Wachangia huduma ya choo na wanafunzi

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WANAFUNZI wa shule za sekondari za Tumo na Roo zilizoko wilayani Hai mkoani Kilimanjaro, wanapanga foleni kupata huduma ya choo na kuchangia na walimu wao kutokana na shule hiyo kukosa choo cha walimu.

Vilevile, walimu wa kike wa Shule ya Msingi Usari, Kata ya Narumu wilayani hapo hawana vyoo na wanalazimika kuomba huduma hiyo katika vyoo vya watawa wa Kanisa Katoliki.

Pia walimu wa Shule ya Msingi Narumu nao wanachangia choo na wanafunzi wao mlangoni kutokana na shule hiyo kutokuwa na shule hiyo kutokuwa na choo cha walimu.

Akizungumzia kadhia hiyo na namna asivyopendezwa na hali hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Juma Irando alisema: "Nimezitembelea hizo shule mwenyewe, ni aibu na inasikitisha sana. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri na Mwenyekiti wa Halmashauri, kwa kupitia mapato ya ndani, tengeni fedha kwa ajili ya vyoo hivi vya walimu. Ninaagiza kwa kuanza, mwanze na shule hizi mbili za Roo na Tumo, ambazo binafsi nimeziona, ili walimu wafanye shughuli zao bila kuwa na wasiwasi au fedheha."

Alipoulizwa kuhusu kero hiyo, Diwani wa Narumu (CCM), John Lengai, alisema mkuu wa wilaya hajapata taarifa kamili na inayojitosheleza kwa kuwa amesahau kuzitaja shule zingine ambazo hazina vyoo na walimu wake wanasubiriana kwenye mlango wa choo na wanafunzi ili kujisaidia.

"Ni kweli Shule ya Sekondari Tumo imebainika kuwa ni miongoni mwa shule ambazo walimu wake hawana vyoo kabisa. Lakini kuna shule zingine za msingi zimesahaulika kama Shule ya Msingi Narumu na Shule ya Msingi Usari.

"Kwenye hizo shule, walimu hawana vyoo kabisa na wanalazimika kujisaidia kwenye vyoo vya wanafunzi. Shule hizi, walimu wanapata shida sana. Kwa mfano, katika Shule ya Msingi Usari, walimu wa kike wanajisaidia kwa Masista wa Roman Catholic (watawa wa Kanisa Katoliki), tena kwenye choo kilichoko karibu na shule hiyo.

"Vivyo hivyo, walimu wa Shule ya Msingi Narumu, wao wanajisaidia katika vyoo vya wanafunzi. Yaani mwanafunzi yupo nje, anamsubiri mwalimu atoke. Hili siyo jambo zuri kwenye jamii yetu, tutafute namna bora wajisitiri," alishauri.

Kutokana na uhitaji huo wa dharura, diwani huyo aliiomba Halmashauri ya Wilaya ya Hai itakapokuwa imeomba kutumia za fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vya Shule ya Sekondari Tumo, isizisahau Shule za Msingi Usari na Narumu.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, David Lekei, alisema tayari wamepokea maelekezo ya mkuu wa wilaya hiyo na wanajipanga kutatua kero hiyo wakati wowote kuanzia sasa.

Uhaba wa matundu ya vyoo ni tatizo linalozikabili shule nyingi za msingi nchini, hali inayosababisha wanafunzi katika baadhi ya shule, kujisaidia kwa kupanga foleni, huku baadhi ya shule zikiwa hazina kabisa huduma ya choo.

Akizungumzia kero hiyo, Fadhila Omari, mkazi wa Kijiji cha Usari, alisema hali hiyo inawaweka hatarini wanafunzi kupata magonjwa ya mlipuko, ikiwamo kipindupindu. Alisema mlipuko huo iwapo utajitokeza unaweza kusababisha wanafunzi kutokuhudhuria darasani na kufanya vibaya kwenye masomo yao.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 inaelekeza uwiano unaofaa ni tundu moja la choo litumiwe na wanafunzi 20 wa kike au wanafunzi 25 wa kiume. Pia kila shule iwe na choo kwa ajili ya walimu.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi na Biashara za Kati wa Benki ya Exim Tanzania, Andrew Lyimo (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kampeni maalum ya "Chanja Kijanja, Kimasta Zaidi", inayolenga kuwashawishi wateja wake wanaomiliki kadi za MasterCard kufanya miamala zaidi kwa kutumia kadi hizo badala ya malipo ya fedha taslimu. Kushoto ni Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano, Stanley Kafu na Mkuu wa Idara ya Huduma Mbadala Kupitia Mifumo ya Kidigitali, Silas Matoi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walazimika kuhamisha mifugo kusaka chakula

**Na Jenifer Gilla**

BAADHI ya wafugaji katika Kijiji cha Sindeni, Kata ya Sindeni, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, wamehamishia mifugo yao katika vijiji vya jirani kutokana na ukame uliokithiri na kusababisha uhaba wa chakula na maji kijijini hapo.

Mmoja wa wafugaji hao, Joshua Godliver, alisema amelazimika kuhamisha mifugo yake katika kijiji cha Kingoma kwa sababu hakuna majani ya kulisha mifugo kijijini hapo.

Joshua mwenye ng'ombe 100 na mbuzi 70, alisema kabla ya kuwahamisha alikuwa analazimika kutembea umbali wa saa mbili na mifugo hiyo ili kufikia maeneo yenye malisho hali iliyokuwa inazorotesha afya yao.

"Kutokana na kutembea mwendo mrefu sisi wenyewe tulikuwa tunachoka na kumwa kwa sasababu jua linatupiga siku nzima, lakini pia mifugo ilikuwa inakonda kwa sababu ya kushinda juani siku nzima, sasa hivi tunashukuru afya zao zimeanza kuimarika.

Naye Zubeda Ndimwe, alisema kuwa amehamisha mifugo yake katika kijiji cha Mswaha baada ya kuona mifugo yake inakonda na kukosa soko anapokwenda kuiuza.

"Ilifika mahali ng'ombe niliyekuwa namuuza Sh. 300,000 nikawa namuuza bei ya hasara ya Sh. 150,000 kwa sababu walikuwa wamekonda ukilinganisha na ng'ombe wanaotoka maeneo yenye malisho," alisema.

Alisema japokuwa kijiji hicho kina majani, lakini inamlazimu kutumia fedha kulipia eneo ambalo mifugo hiyo itakula kwa sababu wenye maeneo yao wanatumia fursa hiyo kujinufaisha kiuchumi.

"Kuhusu maji kule kuna afadhali kidogo kwa kuwa kuna Ruvu (Mto Pangani) ingawa changamoto iliyopo ni umbali kwani inatulazimu kutembea masaa mawili na nusu kufika eneo hilo, hivyo tunalazimika kwenda kila baada ya siku moja ili kuwapumzisha." alisema.

Naye Mollel Lolusu alisema kuwa kabla ya kuhamisha mifugo yake katika kijiji hicho, alipoteza ng'ombe watano waliokufa kutokana na njaa na kukosa maji ya kunywa ya kutosha.

Aidha, alisema wanyama hao pia wanasumbuliwa na ugonjwa unaoitwa ndigana ambao umekuwa ukiathiri mapafu ya wanyama hao na kusababisha kufa.

Kutokana na hali hiyo, mkazi wa eneo hilo, Mwanahawa Omari, aliiomba serikali iwaruhusu kulisha mifugo yao katika ranchi za serikali zilizopo Kijiji cha Nzeli, kuepuka kukamatwa wanapokutwa wanalisha katika maeneo hayo.

"Sisi hatutaki kupewa bure, watupe vitalu vya kulipia ilimradi mifugo yetu ipate sehemu ya kula kwa sababu hata huko tulikohamishia mifugo pia tunalipia na ni mbali inatulazimu kuamka asubuhi kwenda kulisha mifugo," alisema.

Ofisa Mifugo wa Kata ya Sindeni, Dotto Deus, alisema kuwa tangu mwaka huu uanze wametoa vibali 100 vya kuhamisha mifugo kwa wafugaji hao na bado wanaendelea kupokea maombi.

"Tumetoa vibali 100, lakini wafugaji waliohamisha mifugo ni zaidi kwa sababu wengine wanaungana wawili hadi wanne na kuomba kibali kimoja. Kwa ufupi ni kuwa wafugaji wenye mifugo zaidi ya 50 wote wamehamisha mifugo kwa sababu ya ukame," alisema.

Kwa mujibu wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Jamii (UNDP), Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoendelea kukumbwa na athari za mabadiliko ya tabianchi, zinazosababisha majanga ya mafuriko na ukame na kuathiri kwa kiasi kikubwa shughuli za kiuchumi na kurudisha nyuma juhudi za kupunguza umaskini.

# Bilioni 5.8/- kujenga madarasa 290 ya kidato cha kwanza

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI imeupatia Mkoa wa Singida Sh. bilioni 5.8 zitakazotumika kujenga vyumba vya madarasa 290 kwa ajili ya wanafunzi watakaojiunga na kidato cha kwanza kuanzia Januari mwakani.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alibainisha hayo juzi wakati wa kuwekwa wakfu Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kati, Askofu Dk. Syprian Hilinti.

Aliwaagiza wazazi na walezi kuhakikisha wanafanya maandalizi ya kuwapeleka watoto wao shuleni watakaoanza darasa la kwanza na wale wa kidato cha kwanza kwa kuwa serikali imeweka mazingira mazuri ya kumwezesha kila mtoto kupata elimu.

Serukamba ambaye alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika hafla hiyo, alisena serikali inatambua na kuthamini mchango wa Kanisa la KKKT katika huduma ya kiroho na kuhubiri injili ya amani, umoja, upendo na katika kulea na kukuza vipawa mbalimbali.

"Kanisa la KKKT Dayosisi ya Kati pia linatoa huduma mbalimbali za kijamii kama elimu na afya kwa kushirikiana na serikali. Mfano mmojawapo ni Hospitali ya Iambi iliyoko Wilaya ya Mkalama ambayo inamilikiwa na kanisa hilo ambayo serikali inalipa mishahara ya watumishi 31 ili kuyawezesha malengo ya kanisa katika utoaji huduma kwa wananchi," alisema.

Kuhusu kufunguliwa njia ya reli ya kutoka Manyoni - Singida, Serukamba alisema serikali ya mkoa ilishawasilisha ombi hilo kwa Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa ajili ya kufufua njia hiyo na shirika limeahidi kushughulikia.

**HABARI KITAIFA**

## Ndalichako apongeza wamiliki wa viwanda kutoa ajira maelfu

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, amewapongeza wamiliki wa viwanda wa mikoa ya Pwani na Dar es Salaam kwa kutoa ajira kwa maelfu ya Watanzania kupitia uzalishaji wa bidhaa zinazouzwa ndani na nje ya nchi.

Alitoa pongezi hizo juzi alipohitimisha ziara yake ya siku mbili katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ambako alitembelea viwanda na maeneo ya kazi sita yanayozalisha bidhaa mbalimbali vikiwamo vifungashio, vyombo vya majumbani, mabomba, vinywaji, taulo za kike na nyama.

Maeneo yaliyotembelewa na Waziri Ndalichako ni pamoja na Lake Oil Group, Tanzania Ruidar Co. Ltd vya Kigamboni pamoja na Tanchoice Limited, U-fresh Food Limited, Keds Tanzania Ltd na Global Packaging Limited.

"Nimehitimisha ziara yangu ya siku mbili katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Lengo la ziara hii ilikuwa ni kupata mrejesho wa utekelezaji wa Sheria za Kazi ikiwamo kuangalia ajira zinazozalishwa na wawekezaji wetu. Jambo la kufurahisha ni kwamba katika maeneo yote sita niliyotembelea, nimeona zaidi ya ajira 3,000 zimezalishwa," alisema.

Prof. Ndalichako alisema wengi wao kati ya idadi hiyo yote ni vijana, jambo ambalo linadhihirisha serikali inatekeleza ipasavyo wajibu wake wa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji nchini.

Hata hivyo, pamoja na pongezi hizo kwa wawekezaji, Prof. Ndalichako alibainisha kumekuwa na dosari ndogo katika maeneo ya kazi aliyoyatembelea ikiwamo baadhi ya waajiri kutotoa mikataba ya ajira kwa wafanyakazi, kutowasilisha michango katika mifuko ya hifadhi kwa jamii na baadhi ya maeneo kutokuwa na mifumo madhubuti ya usalama na afya mahali pa kazi.

Katika ziara hiyo, Waziri Ndalichako aliongozana na Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Sarah Msafiri, Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Fatma Nyangasa, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usalama na Afya (OSHA), Khadija Mwenda, Kamishna wa Kazi, Suzan Mkangwa, watendaji wengine wa taasisi zilizoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) na wilaya za Kigamboni na Kibaha.

Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Sarah Msafiri, alimshukuru Waziri Ndalichako kwa kufanya ziara katika wilaya yake na kuwakumbusha waajiri kuzingatia sheria za kazi, akiahidi kushirikiana na wawekezaji katika kutekeleza maagizo yaliyotolewa na waziri huyo.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, aliwataka wawekezaji kushirikiana kwa karibu na ofisi yake katika kuboresha mazingira ya kazi.

# Wafanyakazi wa NMB wasaidia watoto JKCI

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhitimisha Mwezi wa Huduma kwa Wateja, wafanyakazi wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam wamejitolea sehemu ya mishahara yao na kukabidhi Sh. milioni 10 na kuchangia damu salama kwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na Kituo cha Tulee Yatima Tanzania (TUYATA) cha Magomeni.

Kupitia Programu ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR), wafanyakazi wa kanda hiyo (mikoa ya Dar es Salaam na Pwani), juzi walikabidhi Sh. milioni tano kusaidia gharama za matibabu ya watoto wanaotibiwa JKCI, walikochangia pia damu za kuwezesha upasuaji, huku wakitoa Sh. milioni tano za kulipia bima za afya kwa watoto 100 wanaolelewa TUYATA.

Makabidhiano hayo yalifanyika JKCI, Muhimbili jijini Dar es Salaam ambako wafanyakazi hao waliongozwa na Meneja wa NMB Kanda, Donatus Richard aliyekabidhi misaada hiyo kwa Mkurugenzi wa Upasuaji JKCI, Angela Muhozya na Mwasisi wa TUYATA, Faudhia Katundu.

Akizungumza wakati akikabidhi misaada hiyo iliyotanguliwa na ushiriki wa wafanyakazi hao katika usafi wa mazingira ulioongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, Donatus alisema kiasi walichotoa kimetoka mifukoni mwa wafanyakazi, lengo likiwa kuchagiza wadau kujitoa kusaidi wenye uhitaji. "Tulizindua Mwezi wa Huduma kwa Wateja pale Mlimani City na sasa tunaelekea kuufunga rasmi, ndipo sisi wafanyakazi wa NMB mikoa ya Dar na Pwani, tukajichanga kwa kile tunacholipwa na mwajiri wetu, tukatafakari cha kufanya, tukaona tuelekeze kidogo tulichopata kwenye sekta ya afya.

"Sekta ya afya ni pana na ina uhitaji mkubwa, nasi tukachagua kuja JKCI kusaidia gharama za matibabu ya watoto wanaotibiwa hapa, sambamba na kuchangia damu kwa ajili ya upasuaji wao. Kingine cha ziada tukaona tukielekeze TUYATA, kulipia bima za afya za NHIF kwa watoto 100 wa kituo hicho," alisema Donatus.

Muhozya aliwashukuru wafanyakazi wa NMB kwa moyo wa kujali uliowasukuma kusaidia gharama za matibabu na kufafanua kwamba kwa mwaka taasisi yake inajikuta ikihitaji zaidi ya Sh. milioni 800 za kusaidia gharama za watoto wasio na uwezo, hivyo wanahitaji wadau kama NMB kufanikisha huduma hiyo.

"Tunapata sapoti kubwa kutoka serikalini, lakini uhitaji ni mkubwa ndiyo maana tunafurahi tunapopata uungwaji mkono kama huu uliofanywa na NMB. Mmeonyesha moyo wa kizalendo na wito wangu kwa Watanzania wajitokeze kusaidia gharama za matibabu na damu kwa ajili ya upasuaji.

"JKCI tuna takribani watoto 500 kutoka mikoa mbalimbali nchini wanaohitaji matibabu ya moyo na mahitaji nayo ni mengi. Kwa takwimu zilizopo, kwa mwaka tunasamehe zaidi ya Sh. milioni 800 ambazo nasi tunategemea kuzipata kwa serikali. Kwa hiyo, sapoti ya wadau inahitajika sana hapa," alisisitiza Muhozya.

Faudhia ambaye ni mwasisi wa TUYATA, alishukuru kwa uzalendo na utu wa wafanyakazi wa NMB kwa kujitoa kulipia gharama za bima za afya na kuomba taasisi zingine na Watanzania kuiga kilichofanywa na benki hiyo, ambayo inakwenda kumaliza shida ya matibabu kwa watoto 100 wa kituo chake.




Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard (katikati), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 5 kwa Mkurugenzi wa Upasuaji Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Angela Muhozya, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Meneja wa NMB Muhimbili, Frank Makungu, Meneja Uhusiano Biashara na Huduma za Serikali, Irene Masaki (wa pili kushoto) na Mhasibu Mapato JKCI, Reuben Nyiti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania yawezeshwa ufuatiliaji magonjwa kwenye maeneo mipakani

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imepatiwa msaada wa vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) vyenye thamani ya Sh. milioni 181.1 kwa ajili ya kufuatilia magonjwa ya kuambukiza kwenye mipaka ya nchini.

Msaada huo umetolewa na serikali ya Marekani kupitia Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) na Shirika la Usimamizi na Uboreshaji wa Huduma za Afya (MDH) uliikabidhi serikali.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa MDH, Dk. David Sando, wakati akikabidhi vifaa hivyo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Prof. Said Aboud.

Dk. Sando alisema msaada huo ni kwa ajili ya kutambua mapema magonjwa kwa wasafiri wote wa ndani na nje ya nchi ili watambulike.

Alisema tangu mwaka 2015 serikali ya Marekani imekuwa ikishirikiana na Tanzania katika kuboresha afya za mpakani ili kukabiliana na magonjwa ya milipuko.

Prof. Aboud alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizo katika hatari ya kupata magonjwa ya milipuko kutokana na nchi ilizopakana nazo kupitia maziwa na bahari.

Alisema vifaa watavitoa katika mipaka saba ikiwamo Namanga, Horohoro, Rusumo, Kabanga, Murongo na Bahari ya Dar es Salaam.

Aidha, alisema msaada mwingine wa dharura ni kuongeza usaidizi wa wafanyakazi 40 katika viwanja vya ndege vya kimataifa kwa ajili ya uchunguzi na kutoa mafunzo ya ziada kwa wafanyakazi 86 wa afya na wasio wa afya.

Prof. Aboud alisema wamekuwa wakishirikiana na MDH kupata msaada wa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano kuhakikisha kwamba wanakwenda sambamba na mikataba ya kimataifa.

Alisema watakuwa wanafuatilia wagonjwa na kukusanya taarifa zao lengo likiwa ni kuzuia magonjwa yasiingie nchini.

"Tumetengeneza mfumo wa TEHAMA tumesimika katika mipaka yetu ili wageni wanapoingia na kutoka tunacheki taarifa zao kama mnavyofahamu saivi kuna mlipuko wa ugonjwa wa ebola lakini tunaendelea na mapambano ya Uviko-19," alisema.

Alisema wanashukuru Shirika la DMH kwa msaada huo ambao utaleta chachu kwa watendaji kuhakikisha wanafikia malengo ambayo wizara imejipangia.

# Serikali yafanya tathmini kuboresha shule za msingi

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inakamilisha tathmini ya upembuzi yakinifu wa shule zote za msingi kupitia mradi wa Boost ili kuandaa mpango endelevu wa uboreshaji wa elimu nchini.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, David Silinde alibainisha hayo jana bungeni alipojibu swali la msingi la Mbunge wa Sikonge (CCM), Joseph Kakunda.

Mbunge huyo alitaka kujua lini serikali itajenga shule mpya za msingi katika maeneo ya Mbirani, Makibo, Kiyombo na Tutuo huko Sikonge mkoani Tabora.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema tathmini hiyo inalenga kubaini taarifa za eneo shule ilipo, hali ya mazingira shule ilipo na umbali kutoka shule moja hadi nyingine.

Pia alisema Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inaangalia umbali kati ya shule na makazi ya watu na idadi ya watu.

Silinde alibainisha kuwa mwaka wa fedha 2022/23, kupitia mradi wa Boost, serikali imetenga Sh. bilioni 230 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi katika halmashauri zote 184 nchini.

Silinde alisema mradi huo ni wa miaka mitano na ujenzi huo pia utahusisha shule za maeneo ya Sikonge.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (wa pili kulia), akijadiliana jambo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene (kulia), Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (wa pili kushoto) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Eliezer Feleshi, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Adhabu tatu kwa madereva bodaboda wanaong'oa vioo

SERIKALI imetaja adhabu tatu zinazowakabili madereva wa bodaboda wanaotoa vioo (sight mirror) kwenye vyombo vyao vya usafiri na kusababisha ajali za barabarani.

Vilevile, imewaonya viongozi wa kisiasa wanaowatetea madereva wasiovaa kofia ngumu pindi askari wa usalama wa barabarani wanapochukua hatua kwa kuwa wanachangia uvunjifu wa sheria.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, alibainisha hayo bungeni jana alipojibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fakharia Shomar Khamis.

Mbunge huyo alitaka kauli ya serikali kuhusu ajali zinazosababishwa na bodaboda kwa kutoa 'sight mirror'.

Akijibu swali hilo, Sagini alisema Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 ya Mwaka 1973 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002, kifungu 39 (1) inayotumika Tanzania Bara na Sheria ya Usafiri Barabarani Sura ya 7 ya Mwaka 2003, kifungu cha 22 inayotumika Zanzibar, zinatamka kuwa ni kosa kisheria kwa mtu yeyote kuendesha chombo cha moto barabarani ikiwamo gari na pikipiki bila kuwa na vifaa kamili ikiwamo sight mirror kwa kuwa chombo hicho kitahesabika kuwa ni kibovu.

Alisema serikali inatoa wito mtu yeyote anayeendesha chombo cha moto, zikiwamo bodaboda, kufuata sheria na kutotoa sight mirror kwenye pikipiki.

Alisema kitendo cha kutoa sight mirror ni kukiuka sheria na dereva wa bodaboda atapaswa kukamatwa na kutozwa faini ya papo kwa papo au kufikishwa mahakamani na chombo chake kuzuiwa mpaka akirekebishe kwa kuweka sight mirror kwa mujibu wa sheria.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alitaka hatua za serikali kwa madereva bodaboda ambao hawavai kofia ngumu.

Sagini, akijibu swali hilo, alisema pamoja na adhabu zilizoko, wamekuwa wakiwaelimisha kuhusu kuheshimu sheria, pamoja na kuvaa kofia ngumu.

Katika swali la nyongeza la Mbunge wa Kinondoni (CCM), Abass Tarimba, aliyetaka serikali kutoa tamko kwa madereva wa bodaboda wanaopita kwenye taa nyekundu, Naibu Waziri Sagini alisema viongozi wa kisiasa wamekuwa wakiwatetea madereva hao na kuwaomba washirikiane kutoa elimu.

"Pamoja na sheria zinachukuliwa lakini tuwe na utashi wa kisiasa wote, madiwani na viongozi wote ili wote tuwe na lugha moja kwa ajili ya usalama wa barabarani, hususani hawa vijana wa bodaboda," alisema.

Sagini alisema kutovaa kofia ngumu kwa madereva bodaboda ni chanzo kikubwa cha vifo kwa madereva hao kwa kuwa kichwa kinapogonga barabara ya lami au chombo kingine cha moto hupasuka.

## Serikali kuongeza kasi na ubora wa intaneti

SERIKALI ina mpango wa kuongeza kiwango cha kasi na ubora cha intaneti kinachotumiwa na taasisi za serikali 312 na taasisi za elimu ya juu kutoka 2.1G kwenda 20G ili kupunguza gharama za intaneti kwa taasisi hizo.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, aliyasema hayo jana bungeni alipojibu swali la msingi la Mbunge wa Vunjo (CCM), Dk. Charles Kimei.

Mbunge huyo alitaka kujua mkakati wa kuwezesha Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) kuunganisha wateja wengi kwenye Mkongo wa Taifa kwa kupunguza gharama za kuunganisha.

Nape alisema serikali inaongeza uwezo wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kutoka kiwango cha sasa cha 200G hadi 800G.

"Kuongezeka kwa kiwango hiki kutasaidia kupunguza gharama, hali itakayofanya kuwaunganisha wateja wengi zaidi, mkakati mwingine wa serikali ni kuondoa wizarani shughuli zote za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kupeleka TTCL," alisema.

Nape alisema uamuzi huo utawezesha TTCL kuwa na uwezo wa kufanya uamuzi wa kibiashara kwa haraka zaidi, ikijumuisha masuala ya kuwaunganisha wateja kwenye mkongo huo.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Sikonge (CCM), Joseph Kakunda, alitaka TTCL iwezeshwe pindi Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) itakapotoa 5G.

Waziri Nape, akijibu swali hilo, alisema licha ya 5G kuingia nchini, serikali haina mpango wa kuipa TTCL upendeleo bali itatakiwa ifuate taratibu zote na kutakuwa na usawa kwenye kampuni za simu.

Alisema mkakati wa serikali kuwezesha TTCL kuunganisha wateja wengi kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ni kupanua wigo na uwezo wa miundombinu ya mawasiliano ukiwamo Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kufika katika maeneo mbalimbali nchini.

Septemba 2021 wizara hiyo iliingia mkataba wa ushirikiano na Shirika la Umeme (TANESCO) katika matumizi ya pamoja ya miundombinu inayojengwa. Kupitia mkataba huo miundombinu inayojengwa kwenye nguzo za TANESCO nchi nzima, nyaya za mawasiliano zinatumiwa kwa pamoja, hivyo ushirikiano huo utaiwezesha TTCL kuunganisha wateja maeneo ya biashara na nyumbani kwenye mkongo huo kwa gharama nafuu kwa kuwa gharama za uwekezaji zitapungua.







# Vikosi JWTZ vyaongeza nguvu uzimaji moto hifadhi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SIKU mbili baada ya Mkuu wa Majeshi mstaafu, Jenerali George Waitara, kuzuru Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA), kufuatilia vikosi mbalimbali vinavyoendelea na operesheni ya kuuzima moto uliozuka ndani ya hifadhi hiyo siku 11 zilizopita, serikali imepeleka mamia ya vikosi vya askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kuukabili.

Waitara ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Shirika la Hifadhi ya Taifa (TANAPA), alikwenda kuongeza nguvu ya usimamizi wa operesheni hiyo iliyoanza Oktoba 22, mwaka huu.

Alipofika katika hifadhi hiyo, Waitara, alipokewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Eliamani Sedoyeka.

"Kwanza niwapongeze wote wanaoendelea na jitihada za kuuzima moto huu uliozuka Oktoba 21, mwaka huu. Tuna kazi moja tu ya kuhakikisha moto huu hauendelei kusababisha hasara na kuathiri shughuli za utalii katika hifadhi yetu.

"Lakini pia niwasihi sana wapambanaji wetu kwamba, ni vyema kila mmoja akahakikisha moto haufiki katika eneo la msitu ndani ya hifadhi hii."

Aidha, Mkurugenzi wa Wanyamapori nchini, Dk. Maurus Msuha, aliitaka TANAPA kuishauri kitaalam serikali kununua helikopta mpya za Wizara ya Maliasili na Utalii ili zisaidie yanapotekea majanga kama ya moto.

Mara ya mwisho moto kama huo ulizuka na kuteketeza sehemu ya hifadhi hiyo, Oktoba 11, 2020 katika eneo la Whona, ambacho ni kituo cha kupumzikia wageni wanaotumia njia ya Mandara na Horombo.

Kanzidata ya Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro, inaonyesha kuwa mwaka 2015/16 eneo lililoteketea kwa moto ni hekta 49.13, mwaka 2016/17 (hekta 17), 2017/18 (82), 2018/19 (72.3), 2020 (22.05).

Kwa kipindi kisichozidi miaka mitano mpaka kufikia mwaka 2020, jumla ya hekta ambazo ziliteketea kwa moto katika hifadhi hiyo zinatajwa kufikia 242.48.

Sababu kubwa ya kuzuka kwa mioto katika eneo hilo ikielezwa uvunaji mbaya wa asali, ujangili na njia mbaya za kilimo.

Katika ripoti yake ya ukaguzi ya mwaka 2020/21 iliyotolewa Machi 30, mwaka huu na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, alisema amefanya uchunguzi kuhusu ripoti ya tukio la moto la KINAPA la Desemba 2020 na kutoa mapendekezo manne kwa mamlaka husika.

CAG Kichere, alisema moto huo ulisababisha hasara ya jumla ya Sh. bilioni 1.214 na kubainisha kuwa mamlaka za hifadhi za taifa hazina uwezo wa vifaa na maandalizi ya kupambana na majanga ya asili.



Baadhi ya madiwani wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, wakimsikiliza Mwenyekiti wa CCM wa wilaya hiyo, Kiria Laizer (hayupo pichani), akitoa maelekezo ya chama kwa viongozi wa serikali jana. **PICHA: GIFT THADEY**

## Watendaji Simanjiro kupimwa utendaji kupitia mikataba lishe

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WATENDAJI wa kata na vijiji katika Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, wamewekwa 'mtegoni' baada ya Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Suleiman Serera, kuahidi kuwapima utendaji wao kupitia mikataba ya lishe.

Kipimo hicho, kitaanza kwa kutazama kama wamefanya suala hilo la lishe ni ajenda ya kudumu katika vikao vya kishe-ria ili kuboresha hali ya lishe na kupunguza athari za utapiamlo katika jamii. Dk. Serera, alikuwa jana na watendaji hao, wakati alipokutana nao na kutoa maelekezo ya utekelezaji vipaumbele vya lishe ngazi ya jamii.

"Mikutano hiyo itachochea na kuibua fursa za lishe, matatizo na suluhu za kutatua matatizo ya lishe, yaliyopo kwenye jamii na kwenye kata," alisema Dk. Serera.

Alisema watendaji hao wanapaswa kuhakikisha lishe inakuwa ajenda ya kudumu katika vikao vya kisheria vya kamati ya maendeleo ya kata.

Alisema mikutano hiyo itahakikisha mpango kazi wa lishe unajumuisha afua za chakula na lishe, afya, majisafi, usafi wa mazingira na uchangamshi kwa watoto.

Aidha, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Simanjiro, Samwel Warioba, alizipongeza kata za Mirerani na Emboreet kwa kuongoza kwa lishe bora kwa jamii katika wilaya hiyo.

Kwa upande wake, Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alisema wajawazito wanapaswa kupewa lishe bora, ili afya ya mtoto iwe nzuri na uwezo bora wa kufikiri.

Naye, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Simanjiro, Kiria Laizer, alisema jamii inapaswa kupewa elimu ya kuhakikisha lishe inapatikana kwa wakati hasa kwa watoto.

## TCCIA yashauri wigo malighafi ya madini upanuliwe

**Na Jaliwason Jasson,** HANANG'

CHAMA cha Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA), kimeshauri kuwa kutokana na malighafi ya madini yanayozalisha chokaa kupatikana kwa asilimia 90 Wilaya ya Hanan'g, mkoani Manyara, ni vizuri wawekezaji wa ndani na wa kigeni, wakatanua wigo kwa kuelekeza nguvu kwenye eneo hilo.

Jana, Katibu wa TCCIA mkoani humo, Mwanahamisi Hussein, alisema wanaona ni vyema kuishauri serikali na Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC), kuwasukuma wawekezaji wa viwanda vinavyotumia malighafi hiyo kuchangamkia fursa.

"Katika Wilaya ya Hanan'g sio chokaa tu inayopatikana bali kunapatikana chumvi hivyo iwapo wawekezaji wakiingia eneo hilo wananchi watanufaika na kupata fursa za kiuchumi.

Mwanahamisi, alisema fursa za uwekezaji katika mkoa huo ni nyingi, akitolea mfano Wilaya ya Simanjiro, kwamba kuna utajiri mkubwa wa zao la ngozi za wanyama, lakini hakuna wanunuzi.


Zao la ngozi, lina faida kubwa kwa taifa na duniani kote, kwa kuwa imegundulika kuwa chujio zuri linalofaa kwenye kuchujia mafuta ya ndege ni chuji la ngozi.

Pia, alisema Wilaya ya Babati, kuna uhakika wa kilimo cha alizeti, mtu anayewekeza kwenye eneo hilo, atasaidia kujengwa kwa viwanda na kuzalisha ajira.

Akizungumzia fursa hizo, Mwekezaji mzawa na Mkurugenzi wa Kiwanda cha Mati Super Brands Limited, David Mulokozi, alisema Mkoa wa Manyara umeshafunguka kiuchumi, mtu anayewekeza mkoa huo ni lazima akumbane na fursa za kibiashara.

Mulokozi, alisema kiwanda chake kimeajiri wafanyakazi 305 na wengi wao ni wakazi wa Babati isipokuwa wachache ambao ni wataalamu waliochukuliwa katika maeneo mengine ya nchi.

**"Katika Wilaya ya Hanan'g sio chokaa tu inayopatikana bali kunapatikana chumvi hivyo iwapo wawekezaji wakiingia eneo hilo wananchi watanufaika na kupata fursa za kiuchumi.**



## Halmashauri Arusha yapokea bilioni 3.27/- miradi ya maendeleo

**Na Allan Isack,** ARUMERU

HALMASHAURI ya Arusha kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imepokea Sh. bilioni 3.27 kutoka serikali kuu, kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Lengo la serikali kutoa fedha hizo ni kuendelea kuimarisha upatikanaji na utoaji wa huduma kwa wananchi, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka huo.

Akitoa taarifa hiyo jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, alisema fedha hizo zinatumika kufanya shughuli mbalimbali za miradi ya maendeleo kwa robo ya kwanza ya Julai hadi Septemba.

Msumi alisema kati ya fedha hizo Sh. milioni 95.2 zimetokana na mapato ya ndani ya halmashauri kukamilika.

Akitoa mchanganuo, alisema Sh. milioni 658.4 ni fedha za elimu bila malipo kwa idara ya msingi na sekondari, Sh. milioni 227.9 za elimu msingi, Sh. milioni 430 zitakuwa za elimu sekondari, Sh. milioni 589.5 zikitumika katika ujenzi wa miundombinu ya shule na Sh. milioni 187.8 zitakuwa za kuendesha shughuli za mitihani ya taifa.

Pia alisema sekta ya afya serikali imetoa Sh. milioni 502.6, kwa mchanganuo wa Sh. milioni 52 kwa ajili ya chanjo, Sh. milioni 50.6 za Mpango wa Kudhibiti UKIMWI, Sh. milioni 50 ujenzi na ukamilishaji wa zahanati ya Mirongoine na Sh. milioni 350 kwa kununua vifaa tiba.

Aidha, alisema serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), kwenye halmashauri hiyo, imepokea Sh. milioni 602, zitatumiwa kwa walengwa 13,920 walio kwenye mpango wa kunusuru kaya maskini.

Mkurugenzi huyo, alisema serikali imetoa Sh. milioni 760 nje ya bajeti kwa kujenga vyumba 38 vya madarasa kwa shule 15 za sekondari ikiwa ni maandalizi ya kuwapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza wanaotegemewa kupangiwa kwenye shule za serikali kwa mwaka wa masomo 2023.

"Fedha hizi zote tayari zimefanya kazi kulingana na zilivyopangiwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo umetumia mafundi jamii 'Force Akaunti' chini ya usimamizi wa kamati za ujenzi zilizoundwa kisheria na wananchi wa maeneo husika," alisema Mkurugenzi Msumi.

# Kituo cha Sayansi kuwaibua wanafunzi 800 pembezoni

**Na Oscar Asaenga,** TANGA

KITUO cha Sayansi jijini Tanga, kinakusudia kuwaibua wanafunzi zaidi ya 800 wa pembezoni, kufikia ndoto zao za kusoma masomo ya sayansi kwa vitendo, baada ya idadi kubwa ya wanaoishi mazingira hayo kukosa maabara za kujifunzia.

Kwa mujibu wa Meneja wa Kituo hicho kilichoko eneo Kisosora, Max George, utekelezaji wa mpango huo, utaanza rasmi Novemba 5, mwaka huu.

"Ni kweli tumepanga kuzindua mradi wa kuangalia namna ya kuweza kuwafikia wanafunzi waliopo umbali wa kilomita tano, ili kuhakikisha nao wananufaika na mafunzo ya sayansi kwa vitendo.

"Tutakuwa tukiwafuata shuleni na kimsingi tutatembelea shule zote na kuwafikia wanafunzi hao kwa kipindi cha wiki nne na watakuwa wakienda kunolewa kwenye madarasa yetu kila Jumamosi.

"Lengo letu hili ni kuhakikisha wanafunzi wanaokaa umbali wa huo kutoka eneo la kituo, tuweze kuwafikia. Humo tutazihusisha pia na shule za binafsi na tumetembelea shule 20 mpaka sasa."

Alisema katika kituo hicho wanahakikisha wanafunzi wanasoma masomo ya sayansi kwa vitendo na wanafanya kazi moja kwa moja walimu na maofisa kwa kuangalia namna ambao unarahisisha ufundishaji walimu kwa kutoa namna mbalimbali ufundishaji wa masomo hayo unakuwa rahisi.

"Watawasaidia walimu na wanafunzi namna mtaala unavyohitaji kwa kuanzisha mfumo ambao walimu na wataalamu wa kituo cha sayansi tunamwandalia mazoezi kwa vitendo ili kumrahisishia anapomaliza inakuwa ni rahisi watoto kuelewa wanachofundishwa na inakwenda ngazi ya msingi mpaka sekondari," alisema.

Alisema mfumo huo waliouanzisha unawezesha watoto kuanza kupenda masomo ya sayansi kabla hata ya kuanza kutumia maabara na kujifunza kwa tija na mafanikio makubwa.



Watu wakikusanyika kushuhudia ajali baada ya pikipiki mbili kugongana katika eneo la daraja la Amtico, Muheza Mjini, mkoani Tanga jana, ambapo madereva wa vyombo hivyo walijeruhiwa na kukimbizwa katika Hospitali Teule Muheza. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Sababu ongezeko la vifo Mkinga zatajwa

**Na Dege Masoli,** MKINGA

WAKAZI wa Maramba, Wilaya ya Mkinga, mkoani Tanga, wametaja miongoni mwa sababu zinazochangia ongezeko la vifo kwa wananchi kuwa ni ukosefu wa vipimo katika vituo vya afya na upungufu wa wataalamu.

Hayo yalielezwa na wananchi wa kata hiyo jana, wakati wa mkutano wa kuutambulisha mradi wa kuijengea uelewa jamii iweze kushiriki katika usimamizi wa rasilimali za umma katika sekta ya afya unaoendeshwa na Asasi ya TAWSEI, inayofadhiliwa na Shirika la Foundation for Civil Society.

Wananchi hao walitoa mfano katika Kituo cha Afya cha Maramba kwamba baadhi ya vipimo vya magonjwa kama ya moyo na mifumo ya kupumua havipo na wagonjwa wanashindwa kwenda hospitali za rufani kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo ukosefu wa fedha.

Asifiwe Paulo, mkazi wa Maramba B, alisema licha ya ukosefu wa vipimo vikubwa na upungufu wa wataalamu, gharama za kuwaona madaktari na kitanda kwa wanaolazwa ni kubwa na wengi wanashindwa kumudu.

Catherine Kopwe (29), alisema kukosekana kwa vipimo katika kituo cha afya cha Maramba kulisababisha mtoto wake, Faythaly Thomas, mwenye miaka minne na nusu kudhaniwa kuwa anasumbuliwa na ugonjwa wa kupungua damu mara kwa mara Cythocel, "lakini alipokwenda Hospitali ya Rufani ya Bombo na kupimwa hakuonekana na maradhi hayo, alitibiwa na sasa amepona.

Kopwe alieleza kuwa hali hiyo imekuwa ikihatarisha maisha ya wagonjwa kwa kutibu tatizo ambalo halipo kwa anayeugua. "Kituo cha Afya cha Maramba walisema anasikoseli, lakini Bombo walimfanyia vipimo vikubwa akaonekana hana tatizo hilo. Kama ningeamua kwenda kwa waganga wa kienyeji angekuwa amekufa," alisema Catherine.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Maramba, Dk. Josephat Mapunda, alisema mahitaji ya watumishi ni 105 wakati waliopo idadi yao ni 32.

Mkurugenzi wa TAWSEI, Bernadeta Choma, alisema mradi huo ulizinduliwa wiki iliyopita na Mkuu wa Wilaya ya Mkinga, Hassan Maulidi Sulumbu, lengo likiwa ni kupata matokeo tarajiwa ya kuimarika huduma za afya ifikapo Desemba 2023.

Alisema Wilaya ya Mkinga ina kata 22, vijiji 85 ikiwa na zahanati 29 na vituo vya afya vitatu wakati sera inaelekeza kila kijiji kiwe na zahanati.

James Chemanjagaa, Mkazi wa Maramba A, alisema kunahitajika jitihada kubwa kutekeleza sera ya afya kwa sababu vituo vina mashuka machafu, tozo ya kitanda kwa anayelazwa ni Sh. 3,000 kwa siku, dawa hazipatikani, wazee hawana vitambulisho na huduma si rafiki.

Ukurasa 15



Harakati za wasomi wa vyuo vikuu katika siasa zilianza enzi za uhuru hadi mageuzi

Ukurasa 16



Miaka miwili ya Dk. Mwinyi Zanzibar yang'ara kidemokrasia na kiuchumi

Ukurasa 19



GIORGIA MELONI Waziri Mkuu mwenye mengi, akianzia kazi baa hadi uyaya

siasa

JUMATANO NOVEMBA 2, 2022

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

UKAME,

# Wadau wanapokumbusha ukaribu serikali, wananchi

- Mmoja ahoji mradi visima Kimbiji, Mpera vipi?

**Na Sabato Kasika**

KUWAPO ukame katika maeneo mbalimbali kunazua taharuki inayotokana na mgawo wa maji kwa wateja, uwezekano wa njaa, mabonde na mito kukauka na kukwamisha kilimo cha mboga na cha umwagiliaji kwa wakulima wengi, mazao kama migomba , mihogo na hata mbaazi kukauka. Hayo ni miongoni mwa mengi yanayotokana na athari za ukame, yanayowaibua wanasiasa na wadau wengine wakitaka kauli ya serikali na hakikisho kwa wananchi la namna ya kukabiliana na hali ngumu.

Ukame huo unaoweza kutishia maisha ya binadamu, mifugo na viumbepori kama wanyama kwenye hifadhi unaelezwa kuwa haufai kunyamaziwa ni vyema kuwapo na mipango mbadala kuukabili na taarifa zijulikane kwa wananchi, mwanasiasa aliyehudumu katika serikali za awamu mbalimbali, Stephen Wasira, anakumbushia.

Anaeleza umuhimu wa wananchi kufahamu hatua za dharura za kuwapatia maji ikiwa ni pamoja na kuchimba visima, mabwawa hasa kwa ajili ya kuwa na maji ya uhakika katika maeneo mbalimbali yanayotishiwa na ukame.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili, Wasira anasema kulikuwapo na mradi wa kuchimba visima kwa lengo la kukabiliana na uhaba wa maji ingawa hafahamu mipango hiyo imeishia wapi na sasa hali ya ukame inaongeza wasiwasi zaidi.



Moja ya kisima eneo la Mpera na Kimbiji kilichofunguliwa kuangalia hali ya msukumo wa maji. Visima hivyo vilitegemewa kupunguza uhaba wa maji Dar. **PICHA: MAKTABA**

Anatolea mfano eneo la Kimbiji na Mpera Dar es Salaam kwamba, lina maji mengi ambayo yanaweza kusambazwa hadi Mto Ruvu ili kuhudumia watu wengi zaidi wa mkoa huo na Pwani , mambo kama hayo yanatakiwa kufahamika kwa wananchi na kauli ya serikali ni muhimu ikatolewa.

"Kulikuwa na mradi wa kuchimba visima kwa ajili ya maji hayo, ninadhani kuna haja ya kuupanua zaidi mradi ili uwe mojawapo na mipango ya muda mrefu ya kukabiliana na ukame, Dar es Salaam na Pwani," anasema Wassira akiongeza kuwa kazi imeshaanza kinachohitajika ni kuikamilisha na kwamba tumaini lililotolewa kwa visima hivyo, lilitakiwa kumaliza shida ya maji Dar na Pwani

"Yaani maajabu kuna mwamba mkuu wa maji 'aquifer' maji hayo yapo karibu na Bahari ya Hindi, lakini hayana chumvi, ni safi na salama, hivyo ni vyema kuendeleza mradi wa kuchumba visima na kuyasambaza zaidi," anasema Wasira.

Anafafanua kuwa kwa wale wanaoishi kando kando ya ziwa, hawana budi kutumia maji ya ziwa, kwa kuwa hayakauki na kwamba wale waonaishi mbali na vyanzo vya maji wachimbiwe visima na mabwawa makubwa ya maji.

Wasira pia anaongeza kwamba, wananchi hawana budi kuaachana na mtindo wa kukata miti ovyo kwenye vyanzo vya maji na katika sehemu zote kwenye makazi yao , misitu na mashambani kwa kuwa unachangia kuwapo kwa ukame na uharibifu wa mazingira na hilo halinabudi kutolewa kauli kila mara ili kulizingatia.

"Kimsingi, tuwe na utaratibu wa kuchimba mabwawa makubwa na kuweka akiba ya maji kwa kukinga na kuhifadhi maji ya mvua, ili nayo yawe chanzo cha maji, lakini pia kuchimba maji ardhini na kuyasambaza maeneo mbalimbali," anasema.

Anasema anaamini kwamba, kukiwa na mipango ya muda mrefu na mfupi ya kukabiliana na ukame na kuitekeleza nchi inaweza kufanikiwa kwa njia hizo za kujenga mabwawa, kuchimba visima na kutokata miti ovyo.

VYANZO VIPYA

Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Hellen Kijo-

INAENDELEA UK. 20

## SAMIA CHINA

# Ni safari nyeti inayoainisha uhusiano mahsusi na Tanzania




Marais Samia Suluhu Hassan na Xi Jinping wa China. **PICHA: MAKTABA**

**Na Anil Kija**

RAIS Samia Suluhu Hassan anatazamiwa kuwasili Beijing China wakati wowote kuanzia sasa kwa ziara ya kiserikali ambako eneo linalotajwa zaidi la mazungumzo yake na mwenyeji wake, Rais Xi Jinping ni biashara. Baadhi ya vianzio vya habari vinataja maeneo muhimu kuwa yatagusa kilimo na miundombinu lakini pia wapo wenye matumaini ya kufufuliwa mradi wa bandari ya Bagamoyo ambako kampuni zilizotaka kupata zabuni ya ujenzi wake zilijitoa miezi michache iliyopita.

Ni safari inayoanza Novemba 2 hadi 4, ni kwa mara nyingine tena Tanzania inachukua nafasi muhimu katika utambulisho wa sera za nje za China. Wakati alipoingia madarakani mwaka 2013, Rais Xi Jinping alifika Tanzania kama ziara yake ya kwanza ya nje, na sasa wakati anaanza muhula wa tatu , ambao unabishaniwa na kujadiliwa sehemu kadhaa duniani, Rais Samia anakaribishwa kuwa kiongozi wa kwanza wa nje kuitembelea China. Ni kielelezo kuwa nchi hizi zinaendelea kuhitajiana kwa masuala ya kimkakati.

Mwaka jana serikali ya China ilitoa tuzo kwa Waziri Mkuu mstaafu Dk. Salim Ahmed Salim, ambaye mwaka 1970 akiwa Balozi wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa alifanya juhudi kubwa kukusanya maoni na msimamo wa pamoja wa nchi za Afrika, za Kiarabu na mwisho kundi kubwa la nchi zinazoendelea kuunga mkono Jamhuri ya Watu wa China ipewe kiti katika umoja huo.

> Ni wazi kuwa mradi kama ule wa reli ya upana wa viwango vya kimataifa (SGR) pamoja kuwa haukutokana na mkopo kutoka China, baadaye umekuwa na ukaribu na mradi huo...

Hadi wakati huo kisiwa cha Taiwan kilikuwa kinashikilia kiti hicho, kwa kutambuliwa na Marekani kama serikali halali ya China, na siyo ile ya kikomunisti. Hali hiyo ilikuwa imedumu kwa miaka 21 na ikawa haikubaliki tena, akatokea Dk. Salim akavunja mwiko.

Hali hiyo pia ilionekana wakati Rais Barack Obama, alipoingia madarakani nchini Marekani mapema mwaka 2009, na kiongozi wa kwanza wa Afrika ambaye alipewa nafasi na Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani kuonana na Rais Obama huko Washington alikuwa Rais Jakaya Kikwete. Ilikuwa ni pigo la diplomasia kwa Kenya ambayo ilitazamia kuwa Rais Obama angetanguliza uzalendo, aangalie au akaribishe kwanza 'ndugu zake wa karibu.' Marekani badala yake ikaangalia nchi ipi ambayo 'haina matata' katika masuala ya haki za binadamu, ikitangulie.

Hapo linakuja suala la ziada, kuwa kati ya maeneo hayo matatu, lile la mshikamano wa jadi, mahusiano ya kibiashara, mifumo ya kisiasa na vielelezo vyake kama haki za binadamu au jinsia, Rais Samia akiwa kiongozi mkuu wa nchi wa kwanza mwanamke Tanzania, nini hasa kimetangulizwa na China. Labda kupata jibu inabidi kutazama kama sababu za Rais Xi kuja Tanzania kwanza mwaka 2013 na kumwalika Rais Samia anapoingia madarakani tena, sababu ni zile zile au laa.

Unaweza kusema kuna tofauti, kuwa mwaka 2013 ilikuwa ni kutambua umuhimu wa urafiki wa jadi kati ya Tanzania na China na dhamira ya kuuendeleza, au hata yeye binafsi kuienzi nafasi ya Tanzania kwa China kupewa kiti chake UN.

Safari hii kuna suala la ziada, kuwa China inataka marafiki zake katika Afrika watangulie kulainisha mijadala kuhusu muhula wa tatu, na Tanzania haina tatizo na kuisaidia China kuweka mambo sawa kidiplomasia kwenye muktadha unaopendeza. Ziara ya Rais Samia ni kama kifungua kinywa, na si ajabu baada ya hapo mataifa mengine yakaacha mijadala na kuendelea na mahusiano na China kama kawaida. Suala la kuongeza mihula ni la chama tawala nchini humo, siyo la Umoja wa Mataifa au la kukubaliwa katika mahusiano na nchi nyingine, iwe ni Afrika au Magharibi.

Yako maeneo yenye mitego katika majadiliano ya kibiashara yanayotazamiwa kati ya viongozi hao wawili, kuwa nchi kadhaa za Afrika zinaonyesha kuanza kukwama ulipaji wa madeni ya miradi iliyojengwa na kampuni za China. Mojawapo ni Kenya lakini imekuwa ikihakikisha kuwa hakuna 'stress' katika ulipaji wa deni hadi sasa; Zimbabwe inatajwa pia, na nyingine kadhaa. Katika mazingira hayo ni wazi China itaanza kuangalia kwa makini zaidi matazamio yale ya ulipaji wa madeni ya nchi za Afrika na mwendo wa kuingia katika mikataba mingine mipya.

Aina ya 'karata turufu' ambazo Rais Samia anaweza kuwa nazo katika mkoba wake anaposhuka katika ndege na kuketi na ujumbe wake kwa majadiliano na wakuu wa China ni uwezekano wa Tanzania kuwa na lundo la fedha za kigeni katika miaka ya karibuni pale mradi wa kuchakata gesi asilia na kuisindilia katika mitungi baada ya kuikandamiza kuwa kimiminika ('liquefied natural gas' (LNG) utakapokamilika. Gesi hiyo inaweza kutumika kwa muda mrefu, sehemu kubwa iuzwe nchi za nje. Ni mradi ambao uchambuzi wa faida zake uliofanywa na Benki ya Stanbic (T) unasema kuwa utaingiza kiasi cha dola bilioni saba kwa mwaka katika uchumi kwa jumla, na dola bilioni mbili mapato ya serikali hivyo kulainisha ulipaji deni la taifa.

Ni wazi kuwa mradi kama ule wa reli ya upana wa viwango vya kimataifa (SGR) pamoja na kuwa haukutokana na mkopo kutoka China, baadaye imekuwa na ukaribu na mradi huo. Ni wazi kuwa reli hiyo ikikamilika na kuanza kufanya kazi kama inavyotarajiwa itabadili kwa kina mustakabali wa uwekezaji katika nchi za ukanda huu, pamoja na SGR ya Kenya ambayo inaunganishwa na Uganda.

SGR hiyo inaelekea itaunganishwa na Burundi, DRC na Rwanda, hivyo kuwa ya kimkakati kwa washirika wao wa kibiashara. Nchi hizo ziko Jumuiya ya Afrika Mashariki na DRC pia ni mwanachama lakini pia ni mshirika wa Umoja wa Maendeleo wa Kusini mwa Afrika (SADC), na ukiangalia kwa karibu mradi huo unaweza kuwa mwendelezo wa sera ya 'Belt and Road' ya China.

Hatua nyingine ya utawala wa Rais Samia inayoweza kumweka karibu na Rais Jinping ni jitihada kubwa anayoifanya ya kumaliza migogoro na mapigano ukanda wote huu, ili ushirikiano chanya na maendeleo ya pamoja kiuchumi vipatikane. China imekuwa ikiongeza uwepo wake katika nchi za Afrika kusaidia kuleta amani kwa njia tofauti na Marekani inayolazimisha chaguzi huru bila kujali mazingira au Russia , yenye kampuni ya askari wa kukodiwa wanaohofiwa kwa ukatili kila wanakopelekwa, kwa mfano Afrika Magharibi, wakipewa jina la Wagner.

Hivyo, endapo kuna ushirikiano wa karibu kati ya Tanzania na DRC kwenye masuala ya ulinzi wa eneo la mashariki, si ajabu China iweze kuendana na mahitaji ya DRC ambayo yanafahamika kwa kina na Rais Samia. Walitembeleana na kuwa na mazungumzo ya kina hivi karibuni, na hata Rwanda inaweza ikaanza kuchoshwa na mzozo huo.

# Harakati za wasomi wa vyuo vikuu katika siasa zilianza enzi za uhuru hadi mageuzi

## •Wengine leo ni viongozi vyama vikubwa
## •Wamo John Mnyika, Zitto, Mbatia

**Na Sabato Kasika**

KWA miaka mingi, Tanzania ilikuwa chini ya mfumo wa chama kimoja cha siasa, hadi mwishoni mwa miaka ya 1980 zilipoanzishwa harakati za kuanzishwa mfumo wa vyama vingi ambao ulizaa matunda mwaka 1992.

Unapozungumzia harakati za siasa, huwezi kuwaweka pembeni vijana hasa wasomi, kutokana na ukweli kwamba, kundi hilo wakiwamo chipukizi ndiyo wanaofanya kazi kubwa ya uhamasishaji wa umma kujiunga na chama.

Jukumu hilo lilianzia tangu miaka ya 60 wakati wa kutafuta uhuru na hata baada ya uhuru, kwani baadhi yao walishiriki katika maamuzi mbalimbali yakiwamo ya kisiasa na waliandaliwa kushika nafasi mbalimbali kupitia jumuiya za chama.

Kimsingi, dhana ya wanafunzi kupitia taasisi na vyuo vikuu kufanya harakati za demokrasia na siasa za ndani imekuwapo kwa muda mrefu tangu kipindi kifupi tu baada ya nchi kupata uhuru.

Mfano hai ni vuguvugu la wanafunzi wa baadhi ya vyuo na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakati huo kikiwa kipya miaka 60, huku wasomi nao wakiwa wa kwanza, akiwamo Samwel Sitta sasa ni marehemu, walifanya mgomo, wakipinga ulazima kwa vijana wote wasomi kupitia mafunzo na kutumikia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), kwa miaka miwili, yaani miezi sita ya mafunzo na miezi 18 ya utumishi ndani ya JKT.

Historia inaonyesha kuwa serikali ilichapisha muswada kwa madhumuni ya kuanzisha programu ya JKT, ambapo wasomi hao wenye siasa za mrengo wa kushoto, walimshinikiza Mwalimu Nyerere kama Rais na Mwenyekiti wa TANU achukue hatua, vinginevyo wasingekuwa upande wake.

Halikadhalika kipindi chote kuanzia mwaka 1961 hadi mwishoni mwa 1966, chama tawala na TANU ambacho sasa ni CCM baada ya kuungana na AFRO ya Zanzibar kilikuwa katika mchakato wa kupata itikadi ya nchi.

Mwaka 1975, chama hicho kiliweka mkazo na kufanya vijana wengi wakati huo kwenda JKT wakiwamo, akina Jakaya Kikwete, Edward Lowassa, Ditopole Mzuzuri na wengine wengi.

Vilevile kupitia wadau kama akina Moses Nnauye, vijana wengine waliibuliwa akiwamo John Komba maarufu kwenye bendi ya uhamasishaji ya CCM ya TOT kutoka chuo cha ualimu kwenda jeshini huku vijana wengine wakiandaliwa katika vyuo mbalimbali kuja kushika uongozi.

Miongoni mwao ni Dk. Emmanuel Nchimbi, aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, aliyesomea uongozi Chuo Kikuu cha Mzumbe, huku Mkuu wa Mkoa wa Dar -es -Salaam Amos Makalla akisomea uhasibu.

Kwa ujumla kuimarisha siasa nchini, TANU ilifanikiwa kupenyeza baadhi ya wasomi katika siasa na wengine wakaingia jeshini akiwamo Moses Nnauye na wengine wengi.

**VYAMA VINGI**

Katika kipindi cha mfumo wa vyama vingi vya siasa, vijana wameendelea kuandaliwa katika utaratibu huo huo wa kushiriki katika shughuli mbalimbali za vyama vyao vya siasa walivyomo.

Mwaka 1991, kulifanyika kongamano la kitaifa la mageuzi, jijini Dar es Salaam, huku wahusika wakuu wa kongamano hilo wakiwa ni vijana wakati huo ambao ni Mabere Marando, Ringo Tenga, Ndimara Tegambwage, Prince Bagenda, Mashaka Nindi ambaye sasa ni merehemu.

Aidha, kulikuwa na Watanzania waliokuwa wanajulikana kwa misimamo yao ya kimageuzi tangu miaka ya 1960 ambao nao walialikwa katika kongamano hilo, ili kutoa hoja zao, baadhi ya waalikwa walikuwa kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni Profesa Mwesiga Baregu marehemu pia, wanafunzi wakiwa ni James Mbatia, Anthony Komu, Idrissa Al Nuru.

Mbatia alikuja kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha NCCR- Mageuzi, hadi hivi karibuni chama chake kilipoingia katika mgogoro wa kiuongozi na kusababisha afukuzwe uanachama japo suala hilo linaendelea kushughulikiwa katika ngazi mbalimbali za kisheria.

Yeye na wenzake ndiyo ambao baadaye waliwahamasisha vijana wengine wasomi kama John Mnyika ambaye kwa sasa ni Katibu Mkuu wa CHADEMA, Zitto Kabwe Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo. Wengine ni Komu aliyeendesha kampeni za ubunge CHADEMA na NCCR-Mageuzi.

Wote hao na wengine ambao sikuwataja, wametokea vyuo vikuu, hivyo ni wazi vyuo vikuu ni chimbuko la mageuzi ya kisiasa kutokana na ukweli kuwa wasomi wake walioshika nafasi mbalimbali za kisiasa wametokea vyuoni.



Emmanuel Nchimbi ni kiongozi wa UVCCM ni tunda la michakato ya demokrasia kwenye vyuo vikuu. **PICHA: MAKTABA.**

# Miaka miwili ya Dk. Mwinyi Zanzibar yang'ara kidemokrasia na kiuchumi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

NI MIAKA miwili ya Rais wa Zanzibar Dk Hussein Ali Mwinyi, kushika usukani baada ya kushinda uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 na kula kiapo cha utii kuingoza Zanzibar ,Novemba 3 mwaka huo , akitimiza mwaka wa pili kesho Alhamisi.

Ndani ya miaka miwili ya uongozi wake, mafanikio makubwa yamepatikana katika kujenga misingi imara ya demokrasia, utawala bora, kuboresha mikakati ya kifedha na ukusanyaji mapato lakini pia kuwekeza zaidi na kuimarisha uchumi ukiwamo wa rasilimali za baharini.

Dk Mwinyi anaeleza kuwa amedhamiria kujenga misingi bora ya kifedha ambayo itawawezesha wananchi kufanya shughuli zao vizuri za kibiashara na kuongeza kipato cha Wazanzibari na kubadili hali ya maisha ya kila raia visiwani hapa.

Akizungumzia mafanikio ya miaka miwili ya Dk Mwinyi kwenye sekta ya fedha na kibiashara, Mkurugenzi Mwendashaji wa Shirika la Bima (ZIC) Zanzibar Arafat Ali Haji, anasema moja ya maono ya Dk Mwinyi ni taasisi za kiserikali ambazo zipo kwa ajili ya kufanya biashara kuendeshwa katika mifumo ya kibiashara tofauti na ilivyozoeleka zamani.

Mkurugenzi huyo anaeleza hayo wakati akizungumza na Nipashe na kusema katika kutimiza ajenda yake hiyo mashirika yote ya serikali amejaribu kuyabadilisha kwa kuweka wakuu wa taasisi hizo kutoka sekta binafsi za kibiashara ili kuleta mabadiliko.

Anasema lengo ni kuleta mabadiliko ya kiufanisi ambayo yanatokana na utendaji unaoendana na matakwa na mahitaji ya biashara ili mashirika hayo yawe na tija na kuwa sehemu ya kuchangia pato la serikali na maendeleo ya nchi yao.

Mkurugenzi huyo anasema wakati Dk Mwinyi anatimiza miaka miwili, shirika la bima limeongezewa ufanisi na pia amelibadilisha kiutendaji na kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuondokana na utaratibu wa kufanya biashara na kufikiria badala ya kuwafuata wateja walipo ili kutambua mahitaji yao.

Anasema hali hiyo inaongeza imani kwa wateja na kuliamini shirika hilo na kuongeza viwango vya biashara ambavyo walikuwa wakifanya na shirika hilo akisema:"Ndani ya mwaka mmoja shirika hilo limeingia makubaliano na kampuni binafsi katika kukuza biashara, ikiwemo kumuwezesha mwananchi kununua bima yake kupitia simu ya mkononi."

Anaeleza kuwa lengo la kufanyakazi pamoja na taasisi za kibenki , kuongeza mapato ya shirika hilo na kupunguza utegemezi wa kupata biashara kutoka sehemu moja na kwamba kutokana na wingi wa wawekezaji wanaofika Zanzibar, shirika hilo limejipanga kutoa huduma kwao kwa sababu uwekezaji unahitaji kupata uhakika wa usalama wa mitaji .



Mkurugenzi Mwendeshaji wa ZIC Zanzibar , Arafat Ali Haji, akielezea mafanikio ya miaka 2 ya Rais Mwinyi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

"Uhakika huo ataupata endapo atawekeza katika majengo na kuyakatia bima ,inapotekea ajali kufidiwa gharama zake bila ya kupata athari kubwa kwa sababu ikitokea mtaji wa mwekezaji umepotea hata Watanzania walioajiriwa wanaweza kukosa ajira na itakuwa na athari kwa ukuaji wa uchumi wa visiwa vya Zanzibar"anasema Haji.

**UTALII KUPAA**

Aidha, anasema ndani ya miaka miwili ya Rais Dk Mwinyi utalii umekua kwa kasi ambapo uwanja wa ndege kwa mara ya kwanza umekuwa na kiwango kikubwa cha uingiaji wa wageni wanaozuru visiwa hivi na kwamba shirika hilo limeanzisha bidhaa ambazo zitawapa unafuu watalii watakapokuwa Zanzibar na akikata bima ya afya au ya safari shirika hilo linamuhakikishia atakapopata dharura yoyote iwe ya kiafya, msiba au kupoteza vitu vyake litamhakikishia usalama wa mali zake.

Kadhalika, makampuni yanayotoa huduma za utalii nayo hawajayaacha kwa sababu ZIC ina bidhaa ambazo inawasadia kutoa huduma na inapotokea dharura shirika hilo lipo katika kuwahakikishia usalama wageni wanapowatembeza.

Anasema hatua hiyo inawahakikishia watalii wanaofika Zanzibar kuwa salama na kuwapa imani wanatembelea eneo sahihi hasa ikizingatiwa kuwa utalii ni sehemu kubwa ya ajira kwa wazanzibari na watanzania.

Haji anasema katika kuunga mkono jitihada za Dk Mwinyi, shirika hilo la bima kwa kutumia uweledi wao litahakikisha watalii wanabaki salama na idadi yao kuongezeka ili kuongeza ukusanyaji wa kodi na kasi ya uchumi wa Zanzibar.

"Kasi ya idadi ya watalii wanaofika Zanzibar ni kubwa hivyo wameanza kuwajengea uwezo watendaji wa shirika la bima ili kuwa na uwezo wa kutambua ni bima gani makampuni ya ndege yanahitaji ili kukidhi mahitaji ya ndege zinazofanya kazi za kusafirisha abiria na watalii" anasema.

Aidha anasema kuwa kulingana na idadi ya wazanzibari bado idadi ya ukataji wa bima ni ndogo na wengi wanakata bima kwa kutii sheria na sio kuona kuwa ni jambo la msingi katika maisha yao.

Anasema shirika hilo kipindi cha nyuma kabla ya uongozi wa Dk Mwinyi lilikuwa likikusanya kati ya bilioni 20 kwa mwaka na kwa mwaka 2021 limekusanya bilioni 21 ambapo katika makusanyo hayo bilioni tano zililipa madai ya wateja wao walioapata ajali.

Shirika hilo pia limekua sehemu la kutoa gawio kwa serikali na hivi karibuni wanatarajia kupeleka shilingi bilioni moja, anaeleza Haji akitaja mipango ya shirika hilo kuwa ni kuwekeza katika majengo ya kibiashara ili kuongeza thamani ya shirika na ukubwa wa mtaji kwa kutoa huduma kubwa zaidi.

Akizungumzia changamoto ya urasimu wa ulipaji wa fidia kwa wateja wa bima, Mkurugenzi huyo anasema utaratibu wa sasa umebadilika na ndani ya siku 10 wateja wao wanauhakika wa kulipwa fidia baada ya kupata majanga na kulipwa kinachostahiki.

Anasema katika kulitekeleza hilo pia wanakumbana na changamoto ya madai hewa ambayo yanatengenezwa kwa lengo la kujipatia fedha na kuongeza:"Ili madai ya mteja wetu aliepata majanga au ajali aweze kulipwa lazima awe na vielelezo ambavyo vinahitajika kutoka jeshi la polisi."

Mkurugenzi huyo anasema, wakati Dk Mwinyi anatekeleza sera ya uchumi wa buluu shirika hilo la bima linatarajia kutoa bima kwa wavuvi ili wanapopata ajali wakiwa baharini wafidiwe akiwataka Wazanzibari kuendelea kumuunga mkono Dk Mwinyi ili kumaliza kipindi chake cha kwanza cha uongozi akiwa ameviimarisha visiwa vyote kiuchumi.



Rais Mwinyi.

# Congo hakukaliki, wakati M23 ikisonga mbele kibabe

## •Miji ya Kiwanja, Rutshuru yatekwa, raia wakimbia

**Na Mwandishi Wetu**

YAMKANI si shwari tena, mvutano unaongezeka kati ya DRC na Rwanda huku waasi wa M23 wakielezwa kuwa wanazidi kupata nguvu na kuongeza mashambulizi , tena wakiua na kuteka miji.

Katika shambulizi la kivita la hivi karibuni waasi wa M23 wamepata mafanikio mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, na kuzusha hofu ya kuzorota zaidi kwa usalama na amani kwenye ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Umoja wa Afrika (AU) umetoa wito wa kusitishwa kwa mapigano na mazungumzo kuanza mara moja ili kuhakikisha amani inakuwepo kwenye eneo hilo.

Umoja wa Afrika mwanzoni mwa wiki hii umetoa wito wa kusitishwa kwa mapigano DRC, baada ya waasi wa M23 kuteka maeneo ya kimkakati mashariki mwa nchi hiyo, hali inayozua taharuki na kuongeza hofu zaidi kwa raia ambao wanateseka kutokana na vita hivyo vinavyohusishwa na nchi majirani wa Congo.

Itakumbukwa kuwa Julai mwaka huu Kundi la Machi 23 maarufu M23, lilikataa makubaliano ya kusitisha mapigano yaliyotiwa saini kati ya Congo na Rwanda, Julai 7, 2022 likiuita mkataba wa makubaliano hayo, kati ya DRC na Rwanda "usio na maana" 'irrelevant' na kuzusha upya vita. Lilijinasibu kuwa litajadiliana na Kinshasa pekee na si taifa jingine.

Hadi sasa waasi wamejiimarisha na kudhibiti maeneo kadhaa kwa kuteka miji ya Kiwanja na Rutshuru Jumamosi iliyopita na kuukata mji mkuu wa Kivu Kaskazini wa Goma kutoka kwenye mawasiliano na jimbo hilo la Mashariki ya DRC.

Umoja wa Afrika umetoa wito wa kusitishwa kwa mapigano mara moja na kutaka pande zote zinazohasimiana "kuheshimu sheria za kimataifa, usalama wa raia na utulivu katika mipaka ya nchi zote za eneo hilo," inasema taarifa ya pamoja ya umoja huo.

Katika kukabiliana na uhasama DRC ilimfukuza Balozi wa Rwanda nchini humo Vincent Karenga, pamoja na kumrudisha nyumbani balozi wa Congo mjini Kigali, Congo inaishutumu nchi jirani ya Rwanda kwa kuunga mkono M23, lakini serikali ya Rwanda imekanusha vikali madai hayo.

### MAZUNGUMZO KUANZA

Mamlaka za kikanda za Afrika zinazidi kuwa na wasiwasi kufuatia hatua hiyo ya DRC huenda ikazidisha mivutano ya kikanda. Kwa mujibu wa mashirika ya habari, maelfu ya waandamanaji wanaoipinga Rwanda waliandamana katika mji wa Goma, mashariki mwa DRC, wakidai silaha za kupigana nayo.



Idadi ya Wakongo wanaotafuta hifadhi nchini Uganda, inaelezwa kuongezeka kila mara. **PICHA:MTANDAO**

AU inaweka matumaini ya kumaliza tatizo kuelekea kwenye mazungumzo ya tatu ya amani kati ya Congo yaliyopangwa kufanyika jijini Nairobi kuanzia Ijumaa Novemba 4 hadi 13 , katika taarifa yake Umoja wa Afrika umeeleza kuunga mkono mazungumzo ya Luanda Angola yanayotoa mwelekeo wa kufikiwa amani ya DRC na M23.

Katika mkutano wa kusaka amani nchini Angola mwezi Julai, Rais wa Rwanda Paul Kagame na Rais wa DRC Felix Tshisekedi (pichani) walikubaliana kupunguza mvutano kwa kurekebisha uhusiano wa kuweka mambo katika hali ya kawaida na kujenga kuaminiana.

Rais wa Angola Joao Lourenco anasema mwanzoni mwa wiki hii kuwa nchi hiyo itamtuma Waziri wa Mambo ya Nje Tete Antonio kwenda DRC, kupatanisha mzozo huo, akionyesha wasiwasi unaosababishwa na kuongezeka kwa mvutano katika eneo hilo na kusababisha ukosefu wa amani , kuua watu na kusababisha usalama kwenye ukanda huo kuzidi kupungua.

Jumatatu wiki hii, Rais wa Rwanda Paul Kagame, ametuma ujumbe kwenye mtandao wa kijamii wa Twitter akieleza kuwa amezungumza na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres kuhusu njia bora za kumaliza mzozo huo.

Idadi inayoongezeka ya Wakongo waliokimbia makazi yao wanaokimbilia Uganda

> "Umoja wa Afrika umetoa wito wa kusitishwa kwa mapigano mara moja na kutaka pande zote zinazohasimiana "kuheshimu sheria za kimataifa, usalama wa raia na utulivu katika mipaka ya nchi zote za eneo hilo," inasema taarifa ya pamoja ya umoja huo.

Maendeleo ya M23 wikendi hii yanawakilisha kuongezeka maradufu kwa eneo lililo chini ya udhibiti wake.

Vikosi vya UN vya kulinda amani DRC -MONUSCO, vimelalamikia wanajeshi wake wanne kujeruhiwa kwa risasi mwishoni mwa wiki, ikiitoa taarifa za kulaani "vitendo vya uhasama vya M23" na kuonya juu ya madhara makubwa kwa raia wa Congo.

Hivi sasa, Wakongo kutoka maeneo yaliyoathiriwa na vita hivyo wanakimbilia Uganda, mashirika ya kutoa misaada ya kibinadamu yakieleza kuwa takriban watu 10,000, wengi wao wakiwa wanawake na watoto, wamevuka mpaka wa Busanza kuelekea magharibi mwa Uganda tangu mwishoni mwa wiki vurumai zilipoanza tena.

Hivi karibuni Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA) imesema takriban wakimbizi 23,000 wameikimbia DRC tangu mapigano kati ya wanajeshi wa serikali na waasi wa M23yalipozuka tena na kutishia usalama.

### M23 NI NANI?

Waasi wa M23 ni akina nani ni swali linaloulizwa kila mara . Na jibu linalotolewa ni kwamba ni kundi la waasi lilianzishwa mwaka wa 2012 linaloongozwa na Watutsi wengi kutoka Congo. Lilipata umaarufu mwaka huo baada ya kuteka mji wa Goma, jiji kubwa zaidi mashariki mwa DRC, kabla ya kusambaratishwa na mashambulizi ya pamoja ya Congo na Umoja wa Mataifa.

Baada ya juhudi za kuleta amani zilizoanza baada ya makubaliano ya amani mwaka 2013, wapiganaji wengi wa M23 walijiunga na jeshi la taifa la DRC. Lakini M23 walianza tena mapigano mwishoni mwa mwaka jana (2021), wakishutumu serikali kushindwa kutimiza ahadi zake chini ya makubaliano ya amani yaliyofikiwa mwaka huo.

### KILIO CONGO

Juni mwaka huu Rais Felix Tshisekedi anailaumu Rwanda kwa kuendesha "vita ya kiuchumi" , akisema inajaribu kuinyakua ardhi ya Congo ili kujipatia rasimali kubwa ya madini.

Anasisitiza kuwa kinachozorotesha hali ya usalama mashariki mwa Congo ni Rwanda inayojaribu kudhibiti sehemu ya ardhi ya Congo yenye utajiri wa madini ya dhahabu na kobalti kwa manufaa yake, akiita vita ya kiuchumi ya kuwania rasimali zake inayofanywa na Rwanda inayatumia magenge yake ya kigaidi.

Miezi kadhaa iliyopita waasi wa M23 waliukamata mji wa kimkakati wa Bunagana ulio kwenye mpaka baina ya Congo na Uganda lakini pia inadaiwa kuwa malengo ya waasi hao ni kuzingira mji wa Goma, ili baadaye waweze kuukamata kwa vile Goma yenye wakazi wapatao 1,000,000 ni makao makuu ya mkoa wa Kivu Kaskazini, na ni kituo kikuu cha biashara kwenye mpaka wa Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

LULA DA SILVA VS JAIR BOLSONARO

# Brazil wanapopindua meza kumtoa Jair Ikulu na kumwingiza mfungwa Lula

## • Atamba walijaribu kunizika lakini ni mzima

**Na Gaudensia Mngumi**

WABRAZILI wamepindua meza kibabe, kwa kumtimua Rais Jair Bolsonaro Ikulu na kumrejesha kiongozi wa zamani Luis Inacio Da Sliva au Lula, aliyekuwa gerezani ndiyo habari ya mjini kweye taifa hilo tajiri wa rasilimali lililopo Amerika ya Kusini.

Ni rasmi kuwa Lula da Silva ameshinda urais wa Brazil, katika duru ya pili ya uchaguzi baada ya kumuangusha mpinzani wake Jair Bolsonaro na kutoa mwito wa amani na umoja baada ya kampeni kali za uchaguzi huo.

Mandhari ya "kurudi tena" ilitawala kampeni za uchaguzi wa urais nchini Brazili. Wengi wakidhani nchi hiyo itakuja kuona ujio wa mara nyingine wa Luiz Inacio Lula da Silva, akimbwaga Bolsonaro, ambaye miaka michache iliyopita, alimtoa ikulu na hilo limetokea.

Lula katika uchaguzi wa urais wa 2018 aling'olewa, leo amerudi tena licha ya kwamba serikali yake inadaiwa kushindwa katika sera zake za kiuchumi, iligubikwa na usimamizi duni wa mali za umma, kukwama vita ya ufisadi na ajenda ya mabadiliko ya hali ya tabianchi hasa kuhusu kuzuia ukataji miti na uharibifu mkubwa wa misitu mikubwa duniani ya Amazon, inayoitwa mapafu ya dunia.

Miongoni mwa wabaya wa Lula, ambao walimchomea utambi lakini safari hii wameshindwa na watakutana naye bungeni ni pamoja na Jaji wa zamani Sergio Moro, ambaye aliongoza uchunguzi dhidi ya ufisadi ulioshuhudia Lula akifungwa jela, katika hukumu ya kukaa gerezani miaka 22.

Mwingine ni Damares Alves, mtetezi mkuu wa nadharia na"itikadi ya kijinsia", ambayo inadai maadili ya familia yako chini ya tishio; na waziri wa zamani wa afya Eduardo Pazuello, ambaye alisimamia vibaya fedha za COVID-19, wote walikuwa mawaziri katika serikali ya Bolsonaro, aliyeonyeshwa mlango.

Uchaguzi huo haukushuhudia uhamishaji mkubwa wa kura kutoka kwa maskini kwenda kwa Lula na chama chake, kama ilivyotarajiwa kwa kuzingatia sera zake za kuunga mkono maskini katika mihula yake miwili ya kwanza aliyoongoza 2003 hadi 2010. Katika kipindi hicho, nchi hiyo ilipata ukuaji wa kasi wa kiuchumi pamoja na hatua zilizofanikiwa za mgawanyo wa mapato, jambo ambalo lilichangia kuungwa mkono mkubwa miongoni mwa Wabrazili maskini.

Mwanasiasa huyo wa mrengo wa kushoto anayetambulika zaidi kwa jina la Lula alizaliwa Oktoba 27, 1945, anakaribia miaka 80 amembwaga Bolsonaro kwa ushindi japo si mkubwa sana wa asilimia 50.9 dhidi ya asilimia 49.17 za Bolsonaro.





Jair Bolsonaro enzi za ushindi wake hapo zamani. Lula da Silva amepindua meza na kumfurumusha ikulu mwezi uliopita **PICHA: MITANDAO**

Lula anasema kwenye hotuba yake baada ya ushindi huo mjini Sao Paulo kwamba anaona ushindi ndilo chaguo la watu wa Brazil na kwamba si ushindi wake pake yake ama chama chake cha Wafanyakazi bali ni ushindi wa vuguvugu la kidemokrasia iliyo kwenye vyama vya siasa na maslahi binafsi na itikadi.

"Ninajiona kama raia wa Brazil ambaye anakabiliwa na mzigo wa kuzijenga upya siasa za Brazil. Kwa sababu wapinzani wangu walijaribu kunizika lakini nikiwa mzima.

Na leo niko hapa, niko tayari kuitawala nchi na kuitoa kwenye hali ngumu sana. Lakini nina imani kwamba kwa msaada wa watu tutapata suluhu ya kuliondoa taifa hapa lilipo na kurejea kwenye demokrasia na amani ili tuweze kuwasaidia wazazi wetu, familia na kuujenga ulimwengu ambao watu wa Brazil wanautaka.Anasema Lula da Silva.

Aidha, anatoa wito wa amani na umoja na kuapa kupambana na njaa na kuulinda msitu wa mvua wa Amazon katika utawala wake, bila kuweka kando mikakati ya kurejesha sera muhimu za kiuchumi na kuboresha hali ya maisha.

**WABABE WAMPONGEZA**

Rais wa Marekani Joe Biden na Emmanuel Macron wa Ufaransa pamoja na viongozi wengine duniani wamempongeza Lula kwa ushindi huo. Mkuu wa Mahusiano ya Nje wa Umoja wa Ulaya, Joseph Borrell pia amempongeza Lula na hasa mahakama ya juu ya uchaguzi nchini Brazil kwa kutekeleza mamlaka yake ya kusimamia mchakato wa uchaguzi kwa haki na uwazi.

Kabla ya kuingia kwenye siasa, Lula alikuwa kiongozi wa vyama vya wafanyakazi na kwa mara ya kwanza aliiongoza Brazil kati ya mwaka 2003 hadi 2010. Kurejea kwake kunaashiria kishindo cha kiongozi huyo aliyehukumiwa kifungo cha miaka 10 jela mwezi Julai, 2017 kufuatia madai kadhaa ya ufisadi na utakatishaji fedha na kifungo hicho kilimzuia kushiriki kwa namna yoyote kwenye uchaguzi wa mwaka 2018 dhidi ya Bolsonaro.

Ushindi wa mrengo wa kushoto unaifanya Brazil kujiunga kwenye wimbi la kuibuka kwa serikali za mrengo huo lililoanza miaka ya 2000 kuanzia enzi ya Hugo Chavez wa Venezuela na Evo Morales wa Bolivia. Rais wa Colombia Gustavo Petro, pia anampongeza Lula kupitia twitter huku rais wa Bolivia Luis Arce akimpongeza na kusema ushindi wa Lula utaimarisha demokrasia na utangamano ndani ya Amerika ya Kusini. Rais wa Venezuela Nicolas Maduro aliandika kwenye mtandao demokrasia imeshinda leo.

Bolsonaro anakuwa rais wa kwanza wa Brazil ambaye hakufanikiwa kushinda kwenye duru ya pili ya uchaguzi tangu taifa hilo liliporejea kwenye demokrasia mwaka 1985 na bado hajasikika iwapo atakubali ama kuyakataa matokeo hayo. Haipo wazi iwapo Bolsonaro atakayakubali matokeo ama la kwa kuwa huko nyuma aliwahi kunukuliwa akisema hatayakubali matokeo iwapo atashindwa kutokana na udanganyifu.

**LULA GEREZANI**

Lula alifungwa jela mwaka wa 2018, akikaa gerezani kwa siku 580 au takribani mwaka mmoja na nusu, alitupwa jela kwa miaka 22 baada ya kupatikana na hatia ya kula rushwa kutoka kwa kampuni ya uhandisi ili kuyapa kandarasi za kazi za serikali.Alihukumiwa kifungo cha miaka 22 kwa makosa ya rushwa, hukumu iliyokomesha maisha ya mbabe huyo ambaye wakati mmoja alikuwa simba wa Amerika Kusini aliyekuwa natisha.

Wiki ya kwanza ya Novemba 2019, ilishuhudia rais wa zamani wa Brazil Luiz Inacio Lula da Silva akitoka gerezani baada ya kuachiliwa kwa amri ya jaji. Katika hotuba yake ya kwanza kwa wafuasi waliomsubiri aachiliwe huru, Lula aliahidi kupigana ili kuthibitisha kuwa hana hatia na kuchukia kile alichokiita "upande mbovu wa mfumo wa mahakama" kwa "kufanya kazi ya kuunyanyasa mrengo wa kushoto au wajamaa wasio na itikadi kali.

Kiongozi huyo alizaliwa Oktoba 27, 1945 katika mji mdogo katika jimbo la kaskazini-mashariki la Pernambuco, na kujiunga na vuguvugu la vyama vya wafanyakazi hadi kuwa mmoja wa viongozi wake, bado hajapoa kwenye siasa

***MITANDAO***

JUKWAA LA VIONGOZI

GIORGIA MELONI

# Waziri Mkuu mwenye mengi, akianzia kazi baa hadi uyaya

• Kuipambazua upya Italia, hataki ndoa jinsia moja, itikadi kali

**Na Gaudensia Mngumi**



NCHINI Italia, muungano wa kihafidhina wa mrengo wa kulia (wenye siasa kali) ndiyo washindi katika uchaguzi uliofanyika miezi michache iliyopita na kuleta mabadiliko ya kiuongozi na kwa mara ya kwanza, tangu Vita vya Pili vya Dunia, nchi hiyo inaongozwa na mwanamama.

Mambo yalianza hivi, katika majira ya baridi mwaka 2019, klabu za usiku kote Italia zilikuwa zikivuma kwa mpigo wa muziki unaoendeshwa na mdundo wenye maneno machache, unaorudiwarudiwa kwa utenzi wa mtu kujizungumzia: "Mimi ni Giorgia. Mimi ni mwanamke, mimi ni mama, mimi ni Mwitaliano, mimi ni Mkristo."Yote hayo yalifanywa kumkejeli.

Ilikuwa mstari au mashairi ya kuvutia uliotolewa na Giorgia Meloni, kiongozi wa Fratelli d'Italia (Ndugu wa Italia), chama kidogo cha mrengo wa kulia, akizungumza wakati wa hotuba aliyoitoa Oktoba mwaka 2019

'Remix' hiyo ya vilabu vya usiku ilikuwa ikimdhihaki Giorgia, lakini miaka mitatu baadaye, ujumbe wake wa kihafidhina na wa kitaifa umekuwa maarufu na sasa ni mwanasiasa mwenye umri wa miaka 45 mwanamama na Waziri Mkuu wa Italia baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika Septemba 25.

### KILICHOMPAISHA

Giorgia ambaye anajulikana kwa uthubutu wake na mwenye lafudhi nzito anapoongea Kiitaliano, amesimamia kupanda kwa kasi kwa chama chake kutoka asilimia 4 ya kuungwa mkono mwaka wa 2018 hadi kilipofikisha asilimia 25 iliyokuwa inatarajiwa kabla ya uchaguzi wa Septemba mwaka huu.

Mtazamo wake wa kutokubaliana na mambo yasiyo na tija kwa taifa, umewagusa Waitaliano waliochanganyikiwa na changamoto nyingi ikiwamo ugonjwa wa COVID-19 , baada ya serikali saba katika miaka 11 ya misukosuko, ndiyo maana wapiga kura wakamuona Giorgia kama chaguo pekee la kisiasa ambalo halijajaribiwa.

Uamuzi wake wa kusimama kidete na upinzani kwa kukataa kuiunga mkono serikali inayoondoka ya Waziri Mkuu Mario Draghi, tofauti na washirika wake wa muungano wa kisiasa Matteo Salvini na gwiji wa kisiasa Silvio Berlusconi - umempatia umaarufu mkubwa zaidi na kuimarisha hadhi yake popote nje na ndani ya Italia.

Lakini maoni yake yenye msimamo mkali kuhusu uhamiaji na uhifadhi wa "familia ya Kikristo" akikataa ushoga na kubadilisha jinsi yamezua hofu ya kurudi kwenye sera zenye utata.

Wakosoaji wanasema matamshi yake yanatishia haki za kiraia na yatafungua njia kwa maoni ya mrengo mkali kuchukua nafasi kuu katika mazungumzo ya kisiasa ya nchi.

### KUANZA SIASA

Giorgia aliyezaliwa mwaka wa 1977, alikuwa na umri wa miaka 15 alipogonga mlango wa tawi la vijana la Movimento Sociale Italiano (MSI), chama kilichoanzishwa baada ya Vita vya Pili vya Dunia na wafuasi wa zamani wa dikteta wa Benito Mussolini.

Akiwa katika mtaa wanapoishi tabaka la wafanyakazi wa Garbatella huko Roma, Giorgia alipata "familia ya pili", anayoipenda kama alivyoeleza katika wasifu wake wenye mada: Io sono Giorgia Kiitaliano [Mimi ni Giorgia].

Alipojiunga na mrengo wa vijana wa chama cha Kifashisti mamboleo cha Italian Social Movement ili kudhihirisha msimamo wake dhidi ya ugaidi wa mrengo mkali wa kushoto ambao uliikumba Italia wakati huo au miaka ya 1980.

Baadaye aliongoza tawi la wanafunzi la Muungano wa Kitaifa wa siasa kali za mrengo wa kulia, akachaguliwa katika Baraza la Manaibu wa Bunge la Italia mwaka wa 2006, na kuwa waziri mwenye umri mdogo zaidi wa Italia miaka miwili baadaye.

Akiwa na umri wa miaka 31, Giorgia alipewa wizara ya vijana katika serikali ya Silvio Berlusconi. Miaka 10 iliyopita, alianzisha chama cha Ndugu wa Italia, ambacho amekiongoza tangu mwaka 2014.

Mnamo mwaka 2020, Meloni alichukua pia uenyekiti wa chama cha Wahafidhina na Wanamageuzi wa Ulaya ambacho kinajumuisha, miongoni mwa wengine, chama tawala cha Poland, PiS.

Mamake Giorgia alimpata mtoto wake huyo ambaye sasa ni Waziri Mkuu akiwa na miaka 23, mwaka mmoja na nusu baada ya kujifungua binti yake wa kwanza, Arianna, mzazi huyo alihangaika na kazi nyingi ili apate riziki, hukuGiorgia pia akifuata nyayo alipokuwa kijana , alifanyakazi ya uhudumu wa baa katika klabu maarufu ya Piper hadi kuwa mlezi wa watoto kwenye 'day care' na hakukata tamaa.

Baba yake, mhasibu kutoka sehemu wanakoishi matajiri kaskazini mwa Roma, alimtelekeza akiwa bado mdogo, akikimbilia mojawapo ya Visiwa vya Canary, akiwa na miaka 11, Giorgia aliamua kuachana naye kwa vile alihisi hamthamini.

Alipata funzo kuwa baadaye analazimika kuishi kila mara kulingana na matarajio ya watu wengine na kujithibitisha hasa katika mazingira yanayotawaliwa na wanaume na mfumo dume unaokwaza.

Akiwa mwanachama wa MSI's Youth Front, Giorgia alifaulu katika kukusanya na kuratibu mashirika ya wanafunzi wakati ambapo MSI ilikuwa chama pekee, chenye nguvu kubwa, cha mrengo wa kulia katika vyuo vikuu ambavyo kwa kawaida vilitawaliwa na utamaduni wa siasa za mrengo wa kushoto.

### KINACHOMPA NGUVU

Kufikia mwaka wa 2012 Italia ilikuwa katikati ya mdororo mkubwa wa uchumi uliosababishwa na mzozo wa madeni katika kanda inayotumia sarafu ya Yuro, Giorgia aliamua kuanzisha upatu wa kisiasa, kufadhili ushirikiano wa chama cha Brothers of Italy.

Wakijiweka kwenye mrengo wa kulia na wenye nembo iliyobeba logo ya rangi tatu za MSI, chama kipya kiliungana chini ya ajenda ya utaifa, ulinzi na wenye kutilia shaka sana Yuro, kikionyesha wasiwasi wa kupinga masoko ya fedha ya kimataifa, wahamiaji na ndoa za mashoga.

"Tunasema ndiyo kwa familia asilia, mke, mume na watoto hapana kwa watetezi wa ushoga, usagaji na wanaobadili jinsia (LGBT), ndiyo kwa utambulisho wa kijinsia, hapana kwa itikadi ya kijinsia, tena ndio kwa utamaduni wa maisha, hapana siyo shimo la kifo," Giorgia anasema katika hotuba ya Juni wakati wa mkutano wa hadhara wa huko Hispania, chama cha kulia Vox huko Marbella.

"Hapana kwa vurugu za Uislamu wenye itikadi kali, ndiyo kwa mipaka salama, hapana kwa uhamiaji mkubwa," anunguruma mbele ya umati wa watu waliokuwa wakishangilia ambao ulimpa shangwe.

Anataka pia kujadili upya mikataba ya Umoja wa Ulaya, na chama chake kinapinga utoaji mimba na ndoa za jinsia moja. Kwa upande wa sera ya uchumi na uhusiano wa kimataifa, anaonekana kutokuwa na uzoefu.

Ametumia muda mwingi wa maisha yake ya kisiasa kama mbunge na ofisa wa chama, hivyo bado yuko darasani lakini anaendelea kuleta Italia mpya.

***MITANDAO.***

UKAME

# Wadau wanapokumbusha ukaribu serikali, wananchi

**INATOKA UK. 13**

Bisimba, anasema kuna haja ya kufikiria vyanzo vingine vya maji, kwa ajili ya kunusuru Watanzania unapotokea ukame kama huu wa sasa.

"Tunaona nchi za wenzetu zimefikia hadi kuchuja maji ya bahari na kuondoa chumvi ili yatumike kwa kunywa, hivyo nasi tuangalie uwezekano huo, wataalam wetu watusaidie katika hilo," anasema Dk Kijo-Bisimba na kuongeza kuwa ni wakati wa watendaji wakuu wa sekta ya maji mijini RUWASA, mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira mijini, sekta za kilimo na umwagiliaji, mifugo na uvuvi kutoa matamko na maelekezo ya mikakati na jinsi serikali ilivyo karibu kusaidiana na wananchi kushughulikia ukame.

Anasema ukame ni janga la asili ambalo haliepukiki, lakini anafafanua kuwa ni muhimu kuwa na hatua za kukabiliana nao, huku akitolea mfano mkakati uloanzishwa na Rais wa awamu ya tatu hayati Benjamin Mkapa, aliyeanzisha utaratibu wa kupanda miti nchi nzima Januari mosi ya kila mwaka.

"Nakumbuka kwa wakazi wa Dar es Salaam, mkuu wa mkoa wa wakati huo Yusuph Makamba alivyohamasisha watu kupanga miti. Ni vyema pia wananchi wakapanda miti inayovuta na kuhifadhi maji. Serikali na wadau wakatoa mbegu na kazi hiyo ikasimamiwa na kufanyika kwa weledi," anakumbusha mwanasheria mbobevu.

Anaeleza kuwa Makamba alihamasisha upandaji wa miti ya matunda na kulifanya jijini kuwa la kijani. Hata hivyo, anaongeza kuwa kasi ya ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa  na uchomaji misiti inazidi kuongezeka jambo ambalo pia serikali inatakiwa kulikemea na kulisimamia zaidi.

"Wakati hayo yakiendelea, hakuna mkakati wa kudumu kumaliza tatizo, hata Mlima Kilimanjaro ambao ni chanzo cha maji cha mto Rau na Njoro unaungua moto kila mara na sasa mito hiyo imeharibikana kukauka," anasema.



Waziri wa Maji, Juma Aweso (mwenye kipaza sauti). **PICHA: MAKTABA**

Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) inaitaja baadhi ya miti inayovuta maji na kulinda vyanzo vyake kuwa ni midodoma, mizambarau, mikuyu , mikangazi, mikungu na miembe.

**LIWE FUNDISHO**

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania TGNP, Lilian Liundi, akizungumzia hali ya ukame inayotishia kuzikumba nchi mbalimbali za Afrika ikiwamo Tanzania, anasema ni muda wa kujifunza akitaka liwe ni funzo la kuwafanya viongozi, wanasiasa na wananchi kuwa na tahadhari ya muda mrefu na muda mfupi ya kukabili ukame huo.

"Kuna umuhimu wa kujiandaa kukabiliana na majanga, ndiyo maana kuna sera au sheria ya majanga yenye lengo la kujiandaa na kuwa tayari pale yanapotokea, ili kuhakikisha hayaleti madhara makubwa kwa wananchi," anasema Lilian

Anakumbusha kuwapo kwa utaratibu wa kuwa na mabwawa mengi, kwa ajili ya kuvuna maji ya kutosha wakati wa mvua , kuweka miundombinu ya kuzuia maji ya mito yote kuishia baharini ili hata ukame unapotokea usilete madhara makubwa hasa kwenye maji.

"Ikumbukwe kuwa ukame unasababisha wanawake na wasichana kutumia muda mwingi kutafuta maji, lakini pia unasababisha umaskini, kwani unaongeze watu gharama za maisha, unaleta mikasa kama kushambuliwa na wanyama usiku kwenye safari ya maji, unyanyasaji wa kijinsia, unakwamisha wasichana kusoma kwa kuwa ndiyo wanaoteka maji ... " anasema.

Akizungumzia gharama anasema ukame unasababisha maji kupanda bei, hali ambayo inawafanya baadhi ya watu kushindwa kuzimudu gharama hizo kutokana na umaskini wa kipato na wakati mwingine ni chanzo cha magonjwa kwa watu wengi mijini na vijijini wanaoweza kuambukizwa maradhi yanayotokana na maji au kukosa maji kama homa ya matumbo, kipindupindu, maradhi ya macho, ngozi kuhara damu na kuharisha.

"Mamlaka ya Hali ya Hewa iwe inatoa taarifa zake mapema za kuonyesha hali halisi ya msimu wa mvua, ili Watanzania waweze kujiandaa badala ya kusubiri tatizo litokee ndipo wanatoa tangazo.Wanasiasa na viongozi nao wawe karibu na wananchi kwenye kusaidia kutatua matatizo ya uhaba wa maji na malisho au chakula kwa binadamu na mifugo".

---

Dondoo: Kulia


1. wingi wa neno jibu
6. Ubinadamu
8. kitu cha thamani kubwa
10.toa fedha kupata kinachouzwa
11.shauku ya jambo
12.tafuna kitu kigumu
14.kasirika ghafla
16.yenye bei ndogo 18.kibua
19.New Delhi ni mji mkuu
21.mmea wenye mizizi inayofanana na viazi vyeupe
22.mwanzo 23.chukuliwa 24.ugwe

Chini:

1. jina la jadi la watawala wa kichaga 2. kata shauri
3. mahali pasipo na mimea na pia penye uhaba wa maji 4. nyanyua
5. sehemu ya vitu au watu
7. uchepe, ukora 9. wekea ahadi mtu kuwa atatimiza jambo fulani
13.uvunjaji wa kanuni za nchi
15.sarenda 16.fanywa tena
17.vazi la mwanaume la kitambaa la kichwani 20.Sadiki 22.toka

**CHEMSHABONGO NA -00 19 00-**


Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

ALFABETI
MAPATO
KARAKANA
BANDAMA
UNABII
MLANGO
GHANA
GUNA
ADUI
DHAKA
NAFUU
AMANI
MKOA
EBOLA

ABA
ABU
NAI
AMA
ATIA
GIZA




Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| F | A | N | A | K | A | | U | M | A |
| A | M | A | L | I | | | | W | |
| R | I | K | A | B | U | | K | A | A |
| A | N | A | S | A | | K | I | N | U |
| O | I | L | I | | M | | F | A | A |
| | | A | R | U | S | H | A | | |
| M | | | I | G | A | | R | A | I |
| I | | U | | A | F | Y | A | | S |
| K | U | R | A | N | I | | N | | H |
| O | | D | | D | R | O | G | B | A |
| A | | U | H | A | I | | A | | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | A | B | U | B | U | | | M |
| U | M | A | T | I | | | | K |
| K | A | R | A | B | A | T | I | A |
| U | L | A | F | I | | O | | A |
| | I | | I | | A | K | A | |
| U | | M | T | I | H | A | N | I |
| M | A | L | I | | A | | U | |
| I | G | A | | A | | T | A | I |
| M | A | J | O | S | H | O | | L |
| I | | I | | I | | A | W | A |



## UVCCM Mbeya yajitosa usafi kwenye masoko

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya Mjini, umejitosa kufanya usafi kwenye masoko mbalimbali ya Jiji la Mbeya ili kuwasaidia wafanyabiashara pamoja na wateja wao kuepuka magonjwa ya mlipuko.

Vijana hao juzi waliungana na wafanyabiashara wa masoko mbalimbali likiwamo Mwanjelwa na Soweto ambako walifanya usafi kwa kukusanya taka zilizokuwa zinazagaa ovyo pamoja na kuzibua mitaro iliyoziba kutokana na mrundikano wa taka.

Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Mbeya Mjini, Clemency Mwandemba, alisema waliamua kufanya usafi huo ili maeneo ya masoko hayo kuwa safi wafanyabiashara na wateja wao wawe salama.

Alisema kwenye usafi huo waliungana na vijana wengine wanaofanya kazi kwenye masoko husika na wananchi wengine waliokuwa wanapita walihamasika.

"Sisi kama vijana tumeamua kufanya usafi huu ili kuwakumbusha wafanyabiashara hawa wajibu wao, lakini tumefanya hivi ili kuepusha magonjwa ya mlipuko ambayo yanasikika kwenye baadhi ya mataifa.

Ofisa Afya wa Jiji la Mbeya, Odas Aron, ambaye aliambatana na vijana hao kwenye usafi huo aliwataka wananchi kufanya usafi kwenye maeneo yao ili kuepuka magonjwa ya mlipuko ambayo alisema yanasumbua mataifa jirani.

Alisema kwa sasa Taifa la Uganda linateseka na ugonjwa wa ebola huku Malawi ikihangaika na mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu.

"Tujaribu kupambana kwa kila namna kuhakikisha tunayaepuka magonjwa haya, tufuate taratibu tunazoelekezwa na wataalamu hasa kufanya usafi kwenye maeneo yetu," alisema Aron.

Baadhi ya wafanyabiashara waliwashukuru vijana hao kwa kujitolea kufanya usafi kwenye masoko hayo wakieleza kuwa wamepata somo la kuhakikisha maeneo yao yanakuwa safi.

# Serikali yaagiza kituo cha afya kifunguliwe kabla Novemba 30

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imeagiza Kituo cha Afya cha Ifupa, Kata ya Ilungu Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kufunguliwa kabla ya Novemba 30, mwaka huu, ili wanachuo wa eneo hilo waanze kupata huduma.

Kituo hicho kilianza kujengwa kwa nguvu za wananchi wa baadhi ya vijiji vya kata hiyo kwa kuchangishana fedha na vitu vingine kabla ya serikali na wadau mbalimbali kuwaunga mkono ili kuwapunguzia tatizo la kusafiri umbali mrefu kwenda kutafuta matibabu.

Kituo hicho ni ambacho aliyekuwa Mwenyekiti wa Kampuni ya IPP, Hayati Dk. Reginald Mengi alichangia Sh. milioni 25 kwa ajili ya kuwaunga mkono wananchi hao baada ya kuwaona kupitia vyombo vya habari wakichangishana.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alifanya ziara katika kituo hicho kwa ajili ya kukagua ujenzi wa baadhi ya majengo na kujiridhisha kwamba ujenzi umekamilika ndipo akaagiza kifunguliwe haraka.

Homera alimwagiza Mganga Mkuu wa halmashauri hiyo kupeleka watumishi katika kituo hicho ili wananchi waanze kupata huduma haraka na zipatikane.

"Hapa nimeona majengo yote muhimu yamekamilika mpaka nyumba ya mganga, sasa hakuna sababu wananchi wawe wanapata tabu tena, naagiza Mganga Mkuu ashirikiane na Mkurugenzi wa halmashauri walete watumishi hapa, vifaa viletwe ili wananchi wapate huduma," alisema Homera.

Aliagiza waanze kufungua jengo la wagonjwa wa nje (OPD) kabla ya kuendelea na vitengo vingine huku akisisitiza kituo kutoa huduma za upasuaji.

Aliwapongeza wananchi wa kata hiyo kwa kujitolea kufanya shughuli za maendeleo na kuwataka wananchi wa maeneo mengine ya mkoa huo kuiga mfano huo. Baadhi ya wananchi wa kata hiyo waliishukuru serikali na wadau mbalimbali kwa kuwaunga mkono kwenye ujenzi wa kituo hicho kutokana na awali kasi kuwa ndogo kwa kutegemea kuchangishana.

Mmoja wa wananchi hao, Rozina Juma, miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya Ujenzi wa kituo hicho, alisema waliamua kuchangishana fedha baada ya kuona wanapata shida ya kutembea umbali mrefu kwenda kupata huduma.

Alisema walikuwa wanakwenda kupata matibabu wilayani Rungwe mjini umbali wa zaidi ya kilomita 50 na wanawake na watoto ndio waliokuwa wanapata shida zaidi.

Alisema wajawazito walilazimika kusafirishwa kwa kutumia pikipiki na kuwasababishia matatizo ikiwamo vifo na watoto wao.

"Tunakushukuru Mkuu wa Mkoa kwa maagizo yako, sisi wanawake tumepata shida kwa muda mrefu sana na ndio maana tulikuwa mstari wa mbele kwenye kuchangia ujenzi, wewe umepita kwenye hiyo barabara yetu umeona, hebu fikiria mjamzito anasafirishwa kwa pikipiki umbali wote huo usalama wake na mtoto unakuwa wapi?" Alihoji Rozina.

Naye Joseph Ngole, alisema wananchi wa eneo hilo walikuwa wana kiu kubwa ya kuwa na kituo cha afya kutokana na zahanati iliyoko kijijini hapo kutokidhi mahitaji ya eneo hilo.

Aliwaomba wadau wa maendeleo kuendelea kuwaunga mkono kwa kuwa wanaendelea na ujenzi wa baadhi ya miundombinu ambayo bado.



Dereva wa bajaji akiwa ameisheheni magunia ya viazi mviringo akitoka kwenye mashamba ya Kawetere jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kampuni ya meli kupunguza nauli ya kusafirisha mizigo

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

KAMPUNI ya Huduma za Meli nchini, imesema inakusudia kupunguza nauli ya kusafirisha mizigo kwa kutumia meli tatu za Ziwa Nyasa ili kuhamasisha wananchi wengi zaidi kutumia usafiri huo na kuongeza ufanisi wa vyombo hivyo.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Zakaria Mbilinyi, aliyasema hayo juzi wilayani hapo wakati wa kikao cha kukusanya maoni ya wadau wa usafirishaji wa majini kuhusu mapendekezo ya nauli mpya za usafirishaji wa abiria na mizigo.

Alisema meli tatu zilizojengwa na serikali kwa gharama kubwa zimekaa muda mrefu bila kuleta tija na kuamua kuja na mapendekezo ya kupunguza nauli za usafirishaji wa mizigo ili kuhamasisha watu wengi zaidi kuzitumia.

Awali, nauli ya kusafirisha tani moja ya mizigo kutoka Bandari ya Kiwira kwenda Mbamba Bay ambako ni zaidi ya kilomita 200 ilikuwa Sh. 53,000, lakini kwa sasa wanataka watoze Sh. 50,000 na kwenda Bandari za Malawi wanapendekeza nauli iwe Sh. 35,000 ama Dola za Marekani 15.

Vile vile, alisema kwa mizigo midogo wanakusudia kupunguza nauli mpaka Sh. 45,000 kwa tani moja inaposafirishwa kwenda umbali wa kuanzia kilomita 100 tofauti na awali kulikuwa hakuna tofauti ya mizigo hiyo.

Pia wanakusudia kusafirisha vifaa kama pikipiki na baiskeli kwa Sh. 11,000 lengo likiwa ni kuboresha huduma za usafiri wa majini na kuwafanya wananchi wauone kuwa nafuu zaidi.

"Tunataka hizi meli zetu zipate mizigo mingi zaidi na wananchi wautumie zaidi kwa sababu ni salama na ni nafuu zaidi kuliko usafiri mwingine na hii itatusaidia kuwa na ufanisi wa meli zetu," alisema Mbilinyi.

Alisisitiza kuwa meli tatu za MV-Mbeya II, MV-Njombe na MV- Ruvuma zitakuwa zinafanya kazi kwenye pande zote za Ziwa Nyasa ambazo ni upande wa Tanzania na Malawi.

Ofisa Masoko wa Kampuni ya Meli, Ojenia Punjila, alisema waliamua kuja na mapendekezo ya nauli mpya kutokana na zilizoko kutofanyiwa marekebisho kwa muda mrefu na kutoendana na hali halisi ya sasa.

Alisema mapendekezo hayo ya nauli mpya yamezingatia gharama za uendeshaji wa meli hizo ikiwamo kuwahudumia watumishi, ununuzi wa mafuta pamoja matengenezo ya meli zinapokuwa zimeharibika.

Kadhalika, nauli zinazotumika kwa sasa ni zilizopitishwa mwaka 2011 na kwa muda wa miaka mitano walikuwa wamesimamisha huduma kwenye ziwa hilo baada ya meli zilizokuwapo kuharibika.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Kaimu Mkeenge, alisema walipokea mapendekezo ya mabadiliko ya nauli hizo kutoka kwenye kampuni hiyo ambayo ilikabidhiwa jukumu la kuziendesha meli hizo na kuamua kusikiliza maoni ya watumiaji kabla ya kuridhia. Alisema vikao vya kupokea maoni hayo vitafanyika katika maeneo yote ambayo meli hizo zinafanya kazi lengo ni kuzifanya kufanya kazi kwa faida na zitumike kuinua uchumi wa taifa.

Alisema baada ya kupokea maoni kwa upande wa Mbeya, wanaenda Mbamba Bay ambako pia watazungumza na wadau ili waje na mapendekezo ya mwisho ya nauli ambazo zitakuwa zinatumika.

"Sisi kama wadhibiti kabla ya kupitisha mapendekezo ya mmiliki wa chombo tunapokea kwanza maoni ya watumiaji, lengo ni kwamba hatutaki mwenye chombo aumie wala watumiaji wa chombo chenyewe," alisema Mkeenge.

Alisema wakati wa kupitisha nauli hizo maoni ya wadau yatazingatiwa ili kuhakikisha hakuna upande unaoumia na hakuna unaomnyonya mwenzake.





# Rais TCCIA asimamishwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HALMASHAURI Kuu ya Chemba ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) Taifa imemsimamisha kwa muda usiojulikana rais wa chemba hiyo, Paul Koyi katika wadhifa wake ili kupisha uchunguzi wa tuhuma mbalimbali zinazomkabili.

Mwenyekiti wa kikao cha dharura cha Halmashauri Kuu ya TCCIA, Charles Chenza, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapo, alisema kikao hicho kimeitishwa baada ya kutoridhishwa na utendaji kazi wa rais wa Chemba hiyo, Koyi.

Alisema kuwa pamoja na kutoonyesha ufanisi wa kiutendaji, pia anazo tuhuma nyingi ambazo anatakiwa azijibu kabla ya kuendelea na nafasi hiyo.

Alisema tuhuma hizo ni pamoja na kushindwa kufanya kazi na wajumbe wa bodi kama katiba inavyomtaka huku akituhumiwa kupoka madaraka ya bodi hiyo kwa kufanya uamuzi mwenyewe.

Pia kukiuka maagizo ya Halmashauri Kuu ya TCCIA Taifa katika kutekeleza mchakato wa ajira ya Mkurugenzi Mtendaji iliyotolewa Januari 15, mwaka huu katika Hoteli ya Morena jijini Dodoma.

"Tuhuma nyingine ni kuiingilia utendaji wa kila siku wa Mtendaji Mkuu wa Chemba, kusimamisha watumishi wa Chemba bila kufuata sheria ya ajira na uhusiano kazini, matumizi mabaya ya fedha za taasisi, ikiwa ni pamoja na kujipangia safari nyingi za nje ya nchi hata zisizo na tija kwa taasisi," alisema Chenza.

Alisema tuhuma nyingine ni kupoka madaraka ya idara ya ununuzi ya chemba na kutofuata taratibu za ununuzi.

Vilevile, alidai rais huyo ameshindwa kutoa fursa mbalimbali za uwekezaji kwa wadau wa sekta binafsi, fursa ambazo zinazotokana na ziara mbalimbali za viongozi wa kitaifa ambapo rais wa chemba anaongozana nao kama mwakilishi wa sekta binafsi.

"Kutokana na tuhuma hizi, Halmashauri Kuu ya TCCIA, imeamua kumsimamisha kwa muda usiojulikana ndugu Paul Koyi katika wadhifa wake wa urais wa chemba ili kupisha uchunguzi," alisema.

Aliongeza kuwa Halmashauri Kuu ya TCCIA imeunda tume huru ya uchunguzi inayojumuisha wajumbe toka serikalini na sekta binafsi ili kufanya uchunguzi wa kina wa tuhuma hizo na kutoa ripoti kwa Halmashauri Kuu ya Taifa ndani ya siku 30 kuanzia juzi.

Chenza alisema halmashauri kuu inamtaka Koyi kutofika katika ofisi za chemba kwa kipindi chote ambacho uchunguzi unaendelea isipokuwa pale tu atakapohitajika na tume ya uchunguzi. Halmashauri Kuu ya TCCIA Taifa imemchagua ndugu Swallah Swallah ambaye kwa sasa ni makamu wa rais (kilimo) kukaimu nafasi ya rais wa chemba mpaka hapo uchunguzi utakapokamilika na mkutano mkuu kuamua vinginevyo.

Alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia uamuzi huo uliochukulia dhidi yake, Rais wa TCCIA, Koyi, alidai tuhuma zinazoelekezwa dhidi yake hazina ukweli na tayari ameshazitolea ufafanuzi kwa waandishi wa habari.

"Tayari nimeshalitolea ufafanuzi kwa waandishi wa habari asubuhi lakini ukweli ni kwamba hicho kikao chao kilikuwa batili kwa mujibu wa Katiba ya TCCIA," Koyi alisema.



Baadhi ya wabunge wakiwasili katika viwanja vya Bunge kwa ajili ya kuanza kwa kikao cha kwanza cha mkutano wa tisa jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Kamati yataka mwongozo wa matumizi ya kawaida

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Utawala Bora na Serikali za Mitaa (USEMI) imeitaka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuja na mwongozo maalum utakaobainisha utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya kawaida ya mapato ya ndani.

Jijini Dodoma juzi, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jaffari Chaurembo, alitoa agizo hilo wakati wa kikao cha kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka 2021/22 katika Halmashauri za Rungwe, Misenyi, Longido, Kakonko na Mkinga.

"Kuna halmashauri inakusanya mapato Sh. bilioni nne, fedha iliyotengwa katika kitengo cha afya ni Sh. milioni 10. Nyingine inakusanya Sh. bilioni mbili na imetenga zaidi ya Sh. milioni 82 kitengo hicho hicho cha afya. Ipo haja TAMISEMI kuandaa fomula ya matumizi ya kawaida ili idara zote ziwe na fomula moja," Chaurembo aliagiza.

Alisema kutokuwapo mwongozo au fomula kunaathiri utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo, akisisitiza fomula maalum itarahisisha utekelezaji wa shughuli hizo.

"Baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya kawaida katika Halmashauri ya Kakonko, ninaitaka halmashauri hii kuwa wabunifu na kuiga mfano kutoka kwa halmashauri nyingine katika kuibua vyanzo vya mapato ili kuondokana na dhana ya kuwa halmashauri hiyo ni moja ya halmashauri zinazokusanya mapato madogo nchini," aliagiza.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angellah Kairuki, aliihakikishia kamati hiyo kuwa ofisi hiyo itaandaa mwongozo wa utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya kawaida kwa kuzingatia mapendekezo ya kamati, idadi ya watumishi pamoja na jiografia ya halmashauri husika.

# Waziri: Tutazingatia maelekezoya Bunge Bandari ya Bagamoyo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, ameihakikishia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuwa wizara itayafanyia kazi maelekezo, miongozo na maoni yaliyotolewa katika uanzishaji, ujenzi na uendelezaji wa Mradi wa Bandari ya Bagamoyo na Eneo Maalum la Uwekezaji (EPZ) kwa ufanisi na kwa wakati.

Dk. Kijaji alitoa kauli hiyo juzi alipozungumzia maoni na mapendekezo ya wajumbe wa kamati hiyo wakati wa uwasilishaji wa Taarifa ya Mchakato wa Uanzishwaji, Ujenzi na Uendelezaji wa Mradi wa Bandari ya Bagamoyo na EPZ katika ukumbi wa Bunge jijini hapo.

Aliwaambia wajumbe wa kamati hiyo kuwa serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kutekeleza jitihada mbalimbali zinazolenga kuendeleza uwekezaji, viwanda na biashara ukiwamo mradi huo wa kielelezo wa Bagamoyo ili kujenga uchumi shirikishi na kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025.

Wajumbe wa Kamati hiyo wakiongozwa na Mwenyekiti wake Daniel Sillo, walitoa maoni na mapendekezo mbalimbali yanayolenga kuboresha utekelezaji wa mchakato wa uanzishaji, ujenzi na uendelezaji wa Mradi wa Bandari ya Bagamoyo ambao ni muhimu katika kukuza biashara na ujenzi wa uchumi wa taifa kwa haraka na kwa kuzingatia wawekezaji sahihi wenye uwezo wa kuwekeza nchini.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA), Charles Itembe, alisema lengo la uendelezaji wa mradi huo ni ujenzi wa bandari ya kiwango cha kimataifa kama kitovu cha usafirishaji na lango la biashara ya kimataifa inayofungamana na eneo la viwanda kwa ajili ya uzalishaji na uongezaji thamani mazao mbalimbali yanayozalishwa nchini.

Alisema mradi huo unaotekelezwa Bagamoyo mkoani Pwani, una faida kubwa kwa taifa ikiwamo kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, kukuza teknolojia, ujuzi na ajira, kukuza biashara ya usafiri baharini na faida kwa kampuni wazawa, fedha za kigeni na kuongeza Pato la Taifa.



# Mji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kujengwa Fumba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZANZIBAR inatarajiwa kuwa na mji wa Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari (TEHAMA) utakaojengwa Fumba Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na kuwa na uwekezaji tofauti.

Hayo yalisema juzi mjini humo na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar, Mhandisi Shukuru Suleiman, wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya hafla ya kuitambulisha Kampuni ya Mawasiliano ya Threefold kutoka nchini Ubelgiji.

Alisema tayari Serikali ya Zanzibar imesharidhia ujenzi huo na inatarajia kutoa hekta 100 ya ardhi Fumba kwa ajili ya mji huo.

Alisema kujengwa kwa mji huo kutoa fursa kwa vijana kupata mafunzo mbalimbali ya kukuza uelewa wao kuhusu Teknolojia ya Mawasiliano (ICT) na watawalenga vijana kutoka vyuo vikuu kutokana na wengi wao kumaliza chuo bila ya kuwa na ujuzi kwa kutoendelezwa.

Alisema wengi waliofanikiwa duniani katika teknolojia ya TEHAMA wameendelezwa baada ya kumaliza elimu yao ya juu na kutoa mfano mvumbuzi wa Facebook ambaye kwa sasa ni tajiri mkubwa kutokana na nchi yake kumwendeleza.

"Kuna mambo mengi yanafanyika ambayo yanasababisha mabadiliko ya dunia...tunataka vitu kama hivyo kuwaendeleza vijana ili kufanikiwa," alisema Mhandisi Shukuru.

Kadhalika, alisema ushiriki wa wanawake katika teknolojia ya TEHAMA upo nyuma ikilinganishwa na wanaume na kujengwa kwa mji huo itakuwa fursa nzuri kwao kujifunza.

Alisema mji huo pia utasaidia kuifanya Zanzibar kukua kibiashara kwa sababu kutakuwa na uwezo wa kuagiza kitu chochote kutoka Zanzibar bila ya mnunuzi kufika.

"Hata katika masuala ya utalii yataimarika kwa sababu mtalii anayetaka kufanya utalii Zanzibar atakuwa na uwezo wa kufanya utalii huko huko aliko bila ya kufika Zanzibar," alisema.

Mmiliki wa kampuni hiyo ya mawasiliano ya intaneti ya Three Fold, Uristof Spieceleer, alisema mji huo wa utaiwezesha Zanzibar kuwa na huduma bora za mawasiliano.

Alisema Zanzibar wakati inaingia katika mageuzi makubwa ya uwekezaji na huduma za utalii, mawasiliano ya uhakika yanahitajika ambayo yatarahisisha upatikanaji wa huduma bora.

Alisema tayari wameshapata baraka zote kutoka serikali ya Zanzibar ya ujenzi wa kituo hicho ambacho kitakuwa cha kisasa kwa huduma za TEHAMA.

Vile vile, alisema mafanikio mengi yatakayopatikana ni kupungua kwa gharama za mawasiliano ya intaneti ili wananchi wote wa mjini na vijijini wafaidike.



Mkuu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) Zanzibar, Azan Hassan Msingiri (katikati), akionyesha vitango bahari kwa Waziri wa Uchumi wa Buluu, Masoud Suleiman Makame (wa pili kushoto), wakati kikosi hicho kilipozindua mradi wa ufugaji wa vitango bahari katika kambi ya KMKM huko Kibwengo Mkoa wa Kaskazini Unguja juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi aeleza umuhimu mabunge Afrika kukutana

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema mikutano ya Chama cha Wanasheria wa Mabunge ya Afrika ni majukwaa muhimu katika kuwaunganisha wajumbe na kupata fursa ya kujadili masuala muhimu ya kisheria.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana katika ufunguzi wa Mkutano wa sita wa Chama cha Wanasheria wa Mabunge ya Afrika, uliofanyika Mbeni, Mkoa Mjini Magharibi.

Alisema katika kuleta ufanisi na maslahi mapana katika shughuli zinazofanywa na mabunge, kuna mambo mengi yanayowaunganisha wanasheria wa Mabunge ya Afrika, ikiwamo suala la mila na tamaduni za kiafrika na mikutano hiyo hujenga uhalali wa kuwa na taasisi ya pamoja.

Aliwataka washiriki kulitumia vyema jukwaa hilo kujifunza na kubadilishana uzoefu miongoni mwao, badala ya kutegemea uzoefu kutoka nchi za kimagharibi.

"Pamoja na hatua kubwa za kimaendeleo walizofikia, ni wazi yapo mambo mengi kwao yasioendana na mazingira yetu, zikiwamo mila na tamaduni zetu," alisema.

Alisema mkutano huo ni muhimu kwa mabunge na serikali katika nchi za Kiafrika, kwa kuzingatia kuwa wanasheria hao wanahusika moja kwa moja na utekelezaji wa shughuli zinazofanywa, ikiwamo suala la utungaji wa sheria.

Aliwataka wajumbe hao kutumia nafasi zao kushauri mambo watakayohisi ni muhimu katika kukiimarisha chama hicho.

Dk. Mwinyi alisema mabunge mengi barani Afrika kama ilivyo kwa mengine duniani hujumuisha wabunge wenye mitazamo tofauti ya kisiasa na kutanabaisha wajibu walionao katika kuitambua hali hiyo na kuiheshimu katika utendaji wa majukumu yao.

"Mnapaswa kutoa ushauri kwa wateja wenu wote kwa misingi ya usawa bila ya kusukumwa na itikadi za kisiasa, mfanye kazi kwa kuzingatia utaalamu mlionao kwa misingi ya taaluma zenu na kuweka mbele maslahi ya umma na ustawi wa Bara la Afrika," alisema.

Rais Dk. Mwinyi alibainisha furaha aliyonayo kutokana na jukwaa hilo kusheheni wanasheria wa Afrika, likiakisi mikakati ya Umoja wa Afrika, ikiwamo Agenda ya 2063, inayosisitiza umoja miongoni mwa nchi za Afrika.

Alisema ni jambo jema kwa chama hicho kuwa na Kanuni za Nairobi "Nairobi Principles" kwa mantiki ya kuwa zimezingatia umuhimu wa kuwajengea wanasheria wa Mabunge ya Afrika weledi, ushirikiano, umoja na kuimarisha utendaji.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa kuzitumia kanuni hizo ili kupata matokeo mazuri yatakayoweza kuyasaidia mabunge na Serikali katika Bara hilo la Afrika. Katika hatua nyingine, Rais Dk. Mwinyi alilipongeza Bunge la Afrika (Pan African Parliament) kwa kuunga mkono juhudi za wanasheria wa Mabunge ya Afrika, ambayo kimsingi yanasimamia Ajenda ya Umoja wa Afrika, yenye azma ya kuwaunganisha Waafrika.

Aliwataka wajumbe kutembelea maeneo ya vivutio vya utalii hapa Zanzibar na kuwa mabalozi wa kuwasimulia wengine pale watakaporejea nyumbani, akibainisha Zanzibar kuwa na vivutio vingi vya utalii, ikihusisha maeneo ya kihistoria, utamaduni, fukwe, wanyama pamoja na mazingira yenye kuvutia.

Naye Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid, alisema kuna umuhimu kwa kujenga utamaduni kwa wanasheria wa Mabunge ya Afrika kutembeleana, huku akabainisha uwapo wa fursa kwa wajumbe hao kuja nchini kujifunza katika Baraza la Wawakilishi.


Alisema Baraza la Wawakilishi lipo tayari kuendeleza ushirikiano na Mabunge ya Afrika pamoja na kusaidia harakati za Chama cha Wanasheria wa Mabunge ya Afrika kwa mustakabali wa maendeleo ya chama hicho.

Spika Maulid Alisema Mabaraza ya Wawakilishi pamoja na Mabunge wamekuwa wakitegemea mchango wa wanasheria na kubainisha imani yake kuwa mkutano huo utatumika kuwajengea uwezo wanasheria hao, kupata uzoefu pamoja na kujiamini.

Rais wa Chama cha Wanasheria wa Mabunge Afrika, Mussa Kombo Bakar, alisema Kongamano hilo la sita la Chama cha Wanasheria wa Mabunge ya Afrika limewashirikisha wajumbe kutoka nchi mbalimbali za Afrika, ikiwamo Tanzania, Zanzibar, Kenya, Uganda, Ghana, Libya, Nigeria, Afrika Kusini pamoja na Msumbiji.

Alizitaja nchi zingine kuwa ni pamoja Syshelles, Sierra Leone, Eswatini, Zimbabwe, Zambia, Malawi, Mabunge ya Kikanda ECOWAS, EALA pamoja na Provinces za Kenya na Afrika Kusini.

Katika hafla hiyo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Mwinyi alipata fursa ya kuzindua Jarida na Tovuti ya Chama cha Wanasheria wa Mabunge Afrika pamoja na Kukabidhi Cheti cha Usajili wa chama hicho.





# Serikali yaonya uvamizi wa maeneo ya hifadhi

**Na Alphonce Kabilondo,**
GEITA

MSHAURI wa Jeshi la Akiba mkoani Geita ametoa onyo kwa wananchi wanaoendelea kukiuka kanuni na sheria za mazingira kwa kuendesha shughuli binafsi ndani ya maeneo ya hifadhi na kuwataka kuondoka mara moja.

Kanali Johnson Kikoti alitoa onyo hilo juzi kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Geita katika hotuba yake aliyoisoma wakati akihitimisha mazoezi ya kijeshi yaliyopewa jina la Timua Vumbi.

Mazoezi hayo ya kijeshi yalifanyika ndani ya Hifadhi ya Msitu wa Geita, eneo la Samina wilayani Geita ili kuwajengea uwezo askari wa Jeshi la Wananchi na Jeshi la Akiba chini ya uratibu wa kikosi cha JWTZ 23, Biharamulo, Kagera.

Kanali Kikoti alisema wananchi wanapaswa kupisha na kuheshimu Hifadhi ya Msitu wa Geita ili kutunza misitu ya asili kwa kuwa wakati mwingine hutumiwa na askari wa JWTZ kwa ajili ya kufanya mazoezi ya kujengea utimamu.

"Ni marufuku kufanya shughuli zozote kibinafsi kwenye eneo hili, hii kazi mliyoiona leo ni endelevu na hatutatoa taarifa tena. Mifugo na watu ni marufuku, hakuna kukata mkaa, wala magogo, wala kuchoma moto.

"Kwanza, uharibifu wa hifadhi hii unatuharibia sisi wanajeshi kupata maeneo ya kujificha kufanyia shughuli zetu, pia sisi wenyewe kupata maeneo ya kufanyia mazoezi. Pili, tunahatarisha maisha ya vizazi vijavyo na kusababisha ukosefu wa mvua," alionya.

Kamanda wa Kikosi cha JWTZ 23 Biharamulo, Kagera, Meja Raphael Paschal alisema mazoezi hayo ya 'Timua Vumbi' yamefanyika kwa wiki mbili kwa lengo la kujenga utimamu, kuangalia uwezo wa dhana na uwezo wa kumudu vikundi.

Meneja wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wilayani Geita, Almas Mggalu alisema kuwa zaidi ya asilimia 50 ya eneo la Hifadhi ya Msitu Geita ambao una ukubwa wa hekta 50,800, limeharibiwa na shughuli za binadamu.



Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Idara ya Maendeleo ya Mtoto, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Aurelia Msanga, akitoa mafunzo maalum kwa maofisa ustawi wa jamii kuhusu njia za kuwanusuru na ukatili watoto walioko shuleni na mtaani yaliyoandaliwa na Shirika la Plan International jijini Mwanza jana. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Diwani acharuka TARURA kutowagusa wananchi

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

DIWANI wa Ibinzamata, Manispaa ya Shinyanga, Ezekiel Sabo, amelalamikia kitendo cha Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) kutekeleza miradi ya barabara ambayo siyo kipaumbele cha wananchi na kuziacha barabara ambazo wananchi wana uhitaji nazo.

Alitoa malalamiko hayo juzi wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani cha kawaida cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/23, wakati taasisi za serikali zilipokuwa zikiwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi kwenye baraza hilo.

Alieleza kusikitishwa TARURA kutekeleza ujenzi wa miradi ya barabara ambayo siyo kipaumbele cha wananchi katika kata yake ya Ibinzamata na kuiacha barabara ambayo ni kipaumbele chao.

"Haiwezekani mamlaka zinafika kwenye kata yangu bila kutoa taarifa, bila hata kuwasiliana na uongozi wa eneo husika na wanafika na kuanza kutekeleza miradi wanayoitaka bila kuuliza hitaji la wananchi. Hiyo siyo sawa kabisa," alilalama.

Wakati wa kikao hicho, baadhi ya madiwani pia waliilalamikia TARURA kwa kufanya kazi bila kutoa taarifa kwa madiwani pamoja na uongozi wa maeneo husika, ambao ndiyo wasimamizi wakuu wa miradi kwenye maeneo yao.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, alitoa maelekezo kwa TARURA kuwa wanapokuwa wakitaka kutekeleza miradi yao, washirikiane na viongozi wa eneo husika wakiwamo madiwani ili kutekeleza barabara ambazo ni kipaumbele cha wananchi kwa maendeleo yao.

Kaimu Meneja wa TARURA Manispaa ya Shinyanga, Yohana Wiliamu, alikiri kuwa katika baadhi ya kata hawakutoa taarifa wakati wa utekelezaji wa miradi ya barabara ikiwamo Ibinzamata na kubainisha kuwa walipitiwa huku akiomba radhi na kuahidi hali hiyo kutokujirudia.

Alisema asilimia 27 ya barabara kwa Manispaa ya Shinyanga zina hali mbaya na kubainisha kuwa katika mwaka wa fedha 2022/23 zimetengwa Sh. bilioni 2.4 kwa ajili ya matengenezo ya ujenzi wa barabara.

# Bilioni 4.6/- kupeleka huduma ya maji vijijini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Kahama mkoani Shinyanga umetenga Sh. bilioni 4.6 kwa ajili ya kupeleka huduma ya majisafi na salama katika vijiji visivyokuwa na huduma hiyo vilivyoko Halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama.

Kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 3.754 zitatumika katika ujenzi wa miradi ya maji ya bomba na Sh. milioni 251.6 zitatumika pia katika uchimbaji wa visima virefu na fedha zimetengwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23.

Kaimu Meneja wa RUWASA wilayani Kahama, Paschal Mnyeti, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji.

Aliema licha ya kupeleka huduma ya majisafi na salama, wananchi wanaendelea kutumia maji machafu yanayowasababishia kupata magonjwa ya mlipuko.

Alisema mwaka wa fedha 2021/22 miradi minne ya maji imeshatekelezwa yenye thamani ya Sh. milioni 920.18 katika maeneo mbalimbali katika Kata za Nyankende, Kisuke Halmashauri ya Ushetu, Mwaluguru (Msalala) na Mhongolo (Manispaa ya Kahama).

Mnyeti alisema vikwazo ambavyo vimekuwa vikiwakabili ni pamoja na kuwapo miamba kwa baadhi ya maeneo hususani Halmashauri ya Ushetu, hali ambayo inasababisha miradi kushindwa kukamilika kwa wakati na wananchi kuendelea kutumia maji ya kwenye madimbwi.

Vilevile, alisema kuna mwitikio mdogo wa wananchi hasa vijana kushiriki katika vibarua vya uchimbaji wa mitaro na ulazaji wa mabomba ya maji.

Salvatory Willison, mkazi wa Segese, Halmashauri ya Msalala, alisema kabla ya utekelezaji wa miradi hiyo, inatakiwa kutoa elimu ya matumizi ya maji na gharama zake ili inapokamilika wananchi watambue mwisho wake watatakiwa kuchangia kiasi gani kwa kila ndoo ya maji.

Omary Athumani, mkazi mwingine wa Segese, aliiomba serikali kuhakikisha inapotekeleza miradi, iangalie uwezo wa kipato kwa mwananchi mmoja mmoja ili kupanga bei stahiki katika kugharamia uendeshahji wa huduma ya maji.

## Waisraeli wapiga kura kwa mara nyingine

**JERUSALEM,** ISRAEL

WAISRAELI wamepiga kura kwa mara ya tano ndani ya kipindi cha miaka minne, katika uchaguzi mkuu ambapo Waziri Mkuu wa zamani Benjamin Netanyahu anafanya jitihada za kurejea tena katika nafasi yake ya awali.

Wachambuzi wanakitathimini kinyang'anyiro hicho kwa kukipa nafasi nzuri chama mrengo wa kulia kuwa kama mtawala katika kile kinachoonekana uwezekano wa serikali ya muungano, baada ya miaka mingi ya mkwamo wa kisiasa, na kwamba hasira za wapiga kura zinaweza kuathiri ushiriki wa zoezi hilo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na DW, uungwaji mkono mkubwa wa kambi ya Uzayuni na mpinzani mwenye msimamo mkali, Itamar Ben-Gvir kumebadilisha mwelekeo wa kampeni.

Ilieleza kuwa Waziri Mkuu aliyedumu kwa muda mrefu zaidi madarani huko Israel, Benjamin Netanyahu anaendelea na mashtaka yanayomkabili mahakamani yanayohusu tuhuma za rushwa, ambayo anakanusha, huku chama chake cha Likud kikitarajiwa kuhitimisha uchaguzi huu kikiwa na wingi wa wabunge.

Muda mfupi baada ya kupiga kura yake mjini Jerusalem, kiongozi huyo wa upinzani alisema ana matumaini kwamba watamaliza siku kwa tabasamu, huku akieleza kuwa hilo lipo katika uamuzi wa watu wenyewe.

"Niwajibu na heshima kubwa kujitokeza kupiga kura. Ni wazi kabisa nasema hili kwa wafuasi wetu, lakini pia kwa ujumla kwa raia wa Israel. Nakwambia wewe nikiwa na mashaka kidogo, lakini Mungu atasaidia, natumaini tutamaliza siku kwa tabasamu, ingawa ni juu yenu, kila mmoja atafanya uamuzi. Ninachotumai tu ni kwamba hamtaipuuza haki yenu ya kidemokrasia kupiga kura kwa zingatio la hatma ya nchi," alisema.

Hata hivyo, wakati vituo vya kupiga kura vikifunguliwa jana, uchunguzi wa maoni wa juma lililopita ulionesha kiongozi huyo wa zamani bado ana upungufu wa viti 61 vinavyohitajika katika kumpa wingi katika bunge la Israel Knesset, lenye wabunge 120, hatua ambayo inaonyesha mashaka ya kuwepo kwa juma zima la matarajio ya mzozo wa kuunda serikali ya muungano na pia uwezekano wa uchaguzi mpya.

Mchakato huo wa upigaji kura ulifanyika baada ya kuvunjika kwa kile kilichoitwa muungano wa mabadiliko, ambao uliviunganisha vyama vinane vilivyotofautiana, na kufanikiwa kumuondoa madarakani Netanyahu mwaka uliopita, na kwamba ulishindwa kufanikisha utulivu wa kisiasa.

Waziri Mkuu wa sasa Yair Lapid bado ana nia kudhibiti wadhifa wake wakati chama chake cha Yesh Atid kikionekana kuwa nyuma kidogo ya Netanyahu cha mrengo wa kulia Likud katika kura ya maoni.

Pia Lapid ambae aliwahi kuwa mtangazaji wa kituo cha televisheni nae alisikika katika kituo cha kupigia kura cha Tel Aviv akiwahimiza wapiga kura kujitokeza vituoni kutimiza wajibu wao. **DW**

# Nigeria yahadharisha Ebola kutoka Uganda

**ABUJA,** NIGERIA

MAMLAKA ya Nigeria imesema nchi hiyo iko katika hatari kubwa ya kupata virusi vya Ebola kutokana na mlipuko wa ugonjwa huo nchini Uganda.

Kituo cha Kudhibiti Magonjwa cha Nigeria (NCDC) kupitia taarifa yake iliyotoa jana, kilisema kiwango kikubwa cha hatari kwa nchi hiyo kinatokana na kiasi kikubwa cha usafiri wa anga kati ya Nigeria na Uganda na mchanganyiko wa abiria, hasa katika vituo vya usafiri vya kikanda vya Nairobi, Addis, viwanja vya ndege vya Ababa na Kigali.

Aidha, Mamlaka ya afya nchini humo ilisema wako macho, huku hatua kadhaa zikiwekwa ili kuzuia na kupunguza athari za uwezekano wa mlipuko wa Ebola kuingia nchini Nigeria.

"Hatua hizo ni pamoja na kuongezeka kwa ufuatiliaji na uchunguzi wa abiria katika viwanja vya ndege," ilisema.

Nigeria pia ilitoa ushauri wa kusafiri kwa wananchi kwamba wanapaswa kuepuka safari zote isipokuwa muhimu kwenda Uganda kwa sasa.

"Lakini wakati kusafiri kwenda Uganda hakuepukiki, wasafiri wanapaswa kuepuka kuwasiliana na watu ambao ni wazi kuwa wagonjwa au wanaoshukiwa kuwa na Ebola," ilishauri.

NCDC ilisema abiria wanaotoka au wanaopitia Uganda wanafuatiliwa kwa siku 21 kuanzia siku walipofika Nigeria.

Pia ilieleza kuwa maofisa wa kushughulikia majanga wako katika hali ya tahadhari tayari kupelekwa iwapo kutatokea mlipuko.

Hata hivyo Uganda imethibitisha zaidi ya visa 100 vya ugonjwa na vifo 30 tangu mlipuko huo uanze Septemba, ikielezwa kuwa kumekuwa na hofu kwamba virusi hivyo vinaweza kuenea katika nchi zingine. **BBC**




Waandamanaji mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) waliotembea hadi kwenye mpaka wa nchi hiyo na Rwanda wakidai kwamba mataifa hayo yanawaunga mkono waasi wa M23, walibeba mabango yenye picha ya rais wa Rwanda Paul Kagame na mwenzake wa Uganda Yoweri Museveni, pamoja na jeneza, juzi. **PICHA: VOA.**

# Korea Kaskazini yaitishia Marekani

**PYONGYANG,** KOREA KASKAZINI

KOREA Kaskazini imeitishia Marekani kuwa itachukua hatua kali za ufuatiliaji ikiwa haitaacha kufanya mazoezi yao makubwa zaidi ya kijeshi na Korea Kusini.

Washington na Seoul siku ya Jumatatu zilianza moja ya mazoezi yao makubwa zaidi ya kijeshi ya anga, ambayo yanatarajiwa kukamilika Ijumaa.

Kwa mujibu wa ripoti iliyochapishwa jana na BBC, Korea Kaskazini pia imerusha mfululizo wa makombora katika wiki za hivi karibuni kujibu mazoezi mbalimbali, huku ikielezwa kuwa suala hilo lilikuja kufuatia ripoti za kijasusi kwamba Pyongyang inajiandaa kwa jaribio la kwanza la silaha za nyuklia tangu 2017.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Korea Kaskazini ilisema "Ikiwa Marekani itaendelea na uchochezi wa kijeshi, Korea Kaskazini itazingatia hatua zenye nguvu zaidi za majibu, pia kama Washington haitaki maendeleo yoyote makubwa ambayo hayafai kwa maslahi yake ya usalama, inapaswa kuacha mazoezi ya vita yasiyo na maana na yasiyofaa mara moja," Pia ilieleza kuwa kama hilo halitazingatiwa, italazimika kuchukua lawama kwa matokeo yote, na kwamba mazoezi ya sasa ya kijeshi, yanayoitwa 'Vigilant Storm' yanahusisha mamia ya ndege zinazofanya mashambulizi ya kejeli saa 24 kwa siku.

Ilielezwa kuwa mwezi Oktoba, Washington ilipeleka shehena yake ya nyuklia ya 'USS Ronald Reagan' karibu na Peninsula ya Korea katika hatua ambayo ilionekana kuwa onyo kwa Kaskazini.

Seoul ilisema kutumwa huko kulionyesha azimio la Muungano wa Korea Kusini na Marekani kujibu vikali chokochoko zozote za Korea Kaskazini.

Pyongyang ilisema mwezi Oktoba kwamba kurusha makombora yake ni mwigizo wa shambulio la nyuklia Kusini. Walidai kuwa walifanikiwa kuiga kugonga vituo vya kijeshi vya Korea Kusini, bandari na viwanja vya ndege, na kusema kwamba makombora hayo yalitengenezwa kubeba silaha za kimkakati za nyuklia.

**BBC**



# GIGY MONEY:
## MASHA LOVE VUJISHA ZAIDI

**Na Mwandishi Wetu**

MDADA mwenye mambo mengi kwenye muziki wa Bongo Fleva, Gigy Money, amesema kitendo cha Masha Love kuposti video yake ya faragha na Jimmy Mafufu, anakiunga mkono kwa asilimia mia kwani ni funzo.

Gigy amezungumza hayo alipokuwa kwenye hafla ya uzinduzi wa albamu fupi ya Mbosso na kupata nafasi ya kuzungumza na wanahabari.

"Amefanya poa sana ikiwezekana avujishe nyingine. Haya mambo ya sijui mwanaume kakuweka ndani uone kakupa heshima wakati kuna mwanamke mwingie nje halafu amchukulie poa inahusu?" alihoji Gigy.

Hivi karibuni, Masha Love alivujisha video zinazomwonyesha akiwa faragha na Mafufu baada ya kudaiwa kukataa ujauzito wake.

Hata hivyo, Mafufu ameendelea kukanusha kuwa na uhusiano na Masha huku akizikana video hizo.

# DAVIDO AFIWA NA MTOTO WAKE KWENYE BWAWA

**LAGOS, Nigeria**



MTOTO wa mwanamuziki maarufu wa Nigeria, Davido Adeleke (Ifeanyi Davido), amefariki dunia wakati akiogelea kwenye bwawa la nyumbani kwao (swimming pool).

Davido alipata mtoto huyo na mpenzi wake wa muda mrefu, Chioma Rowland.

Ifeanyi mwenye umri wa miaka mitatu, alifariki dunia baada ya kuzama kwenye bwawa hilo lililoko nyumbani kwao maeneo ya Banana Island nchini Nigeria.

Habari ya kifo cha mtoto huyo imekuwa kubwa kwenye vyombo vya habari vya kimataifa kwa kumiminika kwa pole nyingi kutoka kwa mastaa wakubwa duniani ambao ni marafiki wa Davido.

Ifeanyi alifariki dunia Jumatatu, Oktoba 31, 2022 ambapo taarifa zaidi zinaeleza kuwa, mtoto huyo kipenzi cha Davido, alizama kwenye maji kwa muda mrefu bila wazazi wake kushtukia.

Wanafamilia waligundua kifo hicho baada ya kuanza kujiuliza mtoto wao yupo wapi ndipo baadaye wakamkuta akielea kwenye maji.

Davido anakuwa msanii wa pili nchini humo kumpoteza mtoto kwa kuzama kwenye maji, kwani mwaka 2018 mtoto wa msanii D'Banj naye alipoteza maisha katika tukio kama hilo.

# HARMONIZE
## AMCHOKONOA DIAMOND

**Na Mwandishi Wetu**



WIMBO mpya wa msanii wa Bongo Fleva, Harmonize wa 'Ma Way' umeonekana kumpiga vijembe vya wazi bosi wake wa zamani, Diamond Platnumz.

Wimbo huo upo kwenye albamu yake mpya na ya tatu aliyoiachia mwishoni mwa wiki inayojulikana kwa jina la Made For Us yenye mkusanyiko wa nyimbo 14.

Katika wimbo huo wa 'My Way', ambao kwa sasa umekuwa gumzo kubwa kwenye mitandao ya kijamii, pamoja na kuzungumzia mahusiano yake ya nyuma ya kimapenzi, lakini amemtaja wazi wazi Diamond.

Ndani ya wimbo huo, amezungumzia maisha yake namna ambavyo anataka kuishi kwa njia yake pasipo na mtu yeyote kumratibia mambo yake na kutupa bomu kwa Diamond.

Harmonize amesikika akiimba kwamba hata hakutaka kuzua vita vya kimaneno na aliyekuwa babake katika muziki Diamond, lakini aliingiwa na shinikizo tu la kuhofia kupitwa kimuziki.

"Hata huyo ndugu yenu mimi sikutaka vita, mbona sikugombana na Madam Ritha, ni presha tu kuhofia nampita," ameimba Harmonize.

SHUTI LA MBALI...



Kiungo mkabaji wa Simba Queens, Vivian Aquino, akiachia shuti wakati wakiwa mazoezini na wachezaji wenzake jana nchini Morocco kujianda na mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake dhidi ya Determine Girls kutoka Liberia utakaochezwa katika Uwanja wa Prince Heritier Moulay El Hassan nchini humo leo. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# KOMBE LA FA KUANZA JUMAMOSI

**Na Adam Fungamwango**

MICHUANO ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF), maarufu FA Cup, msimu wa 2022/23 utaanza rasmi Jumamosi ijayo kwa mechi kadhaa za hatua za awali, ikiwa ni safari ya kuanza kusaka timu itakayoiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa jana na TFF, jumla ya timu nne zitafungua dimba Jumamosi na kuendelea tena Jumapili kwa mechi zingine mbili.

Ratiba inaonyesha kuwa Kigoma Kwanza itaanza kufungua dimba kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika kwa kucheza dhidi ya Kakubilo ya Geita, huku kwenye Uwanja wa Halmashauri Simiyu, timu ya Lamadi ya huko, itaikaribisha Buhare FC kutoka Mara.

Michuano hiyo inayoendeshwa kwa mtindo wa mtoano, itaendelea tena Jumapili ya Novemba 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Shule ya Minaki, ambapo Kibadeni FC ya Pwani itavaana na Tandika United ya Dar es Salaam, huku Misitu FC ya Tanga ikiwa uwanja wa nyumbani, Mwakwani jijini Tanga kucheza dhidi ya Kawele SC ya Kilimanjaro.

Washindi wa michezo hiyo watatinga kwenye hatua ya raundi ya kwanza ambayo ratiba yake itapangwa baadaye.

Yanga ndiyo mabingwa wa kombe hilo msimu uliopita ambalo ililipata Julai 2, mwaka huu kwa kuifunga Coastal Union kwa mikwaju ya penalti 4-1, baada ya kutoka sare ndani ya dakika 90 za mchezo, mechi hiyo ikipigwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.




**Invitation To Tender**

**Tanzania Teachers' Union**
**Tender; TTU/2022/2023/T-SHIRT/C**
**For**
**Supply of May Day T-shirts and Caps**

***Date 2/11/2022***

1. This Invitation for Tenders follows the Tanzania Teachers' Union Financial Regulation 3rd Edition of 2018.
2. Tanzania Teachers' Union has set aside funds for the operation of Tanzania Teachers' Union during the financial year 2022. It is intended that part of the proceeds of the fund will be used to cover eligible payment under the contract for the Supply of May Day T-shirts and caps.
3. Tanzania Teachers' Union now invites sealed Tenders from eligible Suppliers for carrying out the Supply of May Day T-shirts and Caps 2023.
4. Tendering will be conducted through the National Competitive Tendering procedures specified in Tanzania Teachers' Union Financial Regulation 3rd Edition of 2018.
5. A complete set of Tendering Documents in English and additional sets may be purchased by interested Tenderers through and upon payment of a nonrefundable participation fee of 500,000 TZS. Payment is performed through bank via account Mwalimu commercial bank (MCB) 0351083201 Tanzania Teachers' Union or NMB 20101300312 and collect set of Tendering Documents physically at Tanzania Teachers' Union Head quarter office, Jamhuri Stadium from 8:00 AM to 10:00 PM (Monday to Friday).
6. All Tenders must be accompanied by a Tender Securing Declaration in the format provided in the Tendering Documents.
7. All Tenders must be physically submitted in the proper format, at or before 16/11/2022, 09:59AM. Tenders will be opened promptly thereafter in public and in the presence of Tenderers' representatives who choose to attend in the opening at the TTU Head quarter office, ground floor meeting room, BOX 3077, Jamhuri Stadium, Dodoma.

GENERAL SECRETARY
P.O.BOX 3077
DODOMA, JAMHURI STADIUM

TANZANIA TEACHERS UNION (TTU) HEADQUARTERS DODOMA

1712912

# Mwambusi alia kukosa 3 Azam

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Ihefu FC, Juma Mwambusi, ameonyesha kusikitishwa na kukosa pointi tatu dhidi ya Azam FC juzi baada ya timu yake kukubali kipigo cha bao 1-0 kwenye Uwanja wa Azam Complex, akisema ni mechi ambayo walipaswa kushinda.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kumalizika, Mwambusi alisema walitawala kila kitu, wakati wakiwa wote 11 na hata baada ya kucheza pungufu, lakini umakini wa wachezaji wake uliwagharimu kwani mpaka mapumziko timu yake ilitakiwa iwe na mabao matatu.

"Nasikitika, tumepoteza mechi ambayo tulitakiwa kushinda, tulicheza dakika nyingi tukikiwa pungufu, nawapongeza tu Azam kwa bao walilolipata, lakini walikuwa kwenye mazingira magumu, tumetawala mechi, tumefanya mashambulizi, ila umakini unakosekama.

"Nafasi tatu za wazi tumepata, lakini umakini umekosemana, na hili itabidi tulifanyie kazi sana kwenye uwanja wa mazoezi, siyo kitu kizuri na tupo sehemu mbaya. Ligi ni ngumu na ina timu chache," alisema kocha Mwambusi.

# Zimamoto yaitaka nafasi ya Malindi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Zimamoto SC, imesema mipango yake ni kuhakikisha michezo minne iliyobaki ya mzunguko wa kwanza inashinda ili wakae kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo wakati wa mapumziko ya kupisha usajili wa dirisha dogo.

Zimamoto ipo nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi kuu Zanzibar ikiwa na alama 20 wakati timu ya Malindi inaongoza ligi hiyo ikiwa na alama 21, zote zikiwa tayari zimecheza michezo 10 kila moja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Zimamoto, Mohamed Ali Hilali, alisema malengo ya kushinda michezo minne iliyosalia kabla ya mapumziko ya usajili wa dirisha dogo yatatimia iwapo wachezaji wataendelea kujituma kama ilivyo sasa.

Alisema timu hiyo inajiandaa na mchezo wao wa 11 dhidi ya Maafande wa Polisi utakaochezwa Jumapili wiki hii, huku akieleza ni moja kati ya mechi ngumu kwao bila kuangalia nafasi iliyopo Polisi kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Katika michezo minne, tunahitaji kushinda kwa kuanza na Polisi na kila mtu anaijua timu ya Polisi muda wowote inaweza kubadilika na kutibua mipango yako hata kama ipo chini kwenye msimamo wa ligi, hivyo tunapaswa kucheza kwa umakini," alisema.

## ZISIKUPITE

### GUNDOGAN AITIA HOFU CITY

KLABU ya Manchester City wanahofia, Ilkay Gundogan, ataondoka katika klabu hiyo kwa uhamisho wa bila malipo msimu ujao. Kiungo huyo wa kati wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 32, bado hajakubali mkataba mpya, na mkataba wake wa sasa unamalizika Juni. (***Football Insider***)

### RASHFORD KUBAKIZWA UNITED

MANCHESTER United wanataka kupata hatima ya Marcus Rashford Old Trafford kabla ya mwisho wa mwaka ili kumzuia kunyakuliwa. Mshambuliaji huyo wa Kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 25, atakuwa huru kufanya mazungumzo na klabu nyingine Januari isipokuwa iwapo atatia saini mkataba mpya au kipengele cha chaguo la mwaka mmoja katika mkataba wake. (***Daily Mail***)

### UNITED YAWINDA NYOTA

KLABU ya Manchester United ina nia ya kumsajili beki wa kulia wa England, Max Aarons mwenye umri wa miaka 22, kutoka Norwich ili kumpa changamoto mchezaji wa kimataifa wa Ureno, Diogo Dalot (23), huku Mholanzi wa Bayer Leverkusen, Jeremie Frimpong mwenye umri wa miaka 21, akiwa chaguo lingine. (***Sun***)

### DANILO ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL wameripotiwa kutuma maskauti kumtazama kiungo wa kati wa Palmeiras na Brazil Danilo wiki iliyopita, huku 'Washikabunduki' hao wakiwa na nia ya kumleta mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 Januari. (***Sun***)

### TORRES AWANIWA ARSENAL

ARSENAL pia wameripotiwa kufanya mazungumzo na winga wa Uruguay, Facundo Torres mwenye umri wa miaka 22, kutoka Orlando City. (***Evening Standard***)

### GAKPO KUNG'OLEWA PSV

KLABU ya Manchester United bado ina nia ya kumsajili winga wa PSV, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 23, Mholanzi huyo alikaribia kusajiliwa na 'Mashetani Wekundu' hao msimu wa majira ya joto. (***GiveMeSport***)

### SEMEDO KUMRITHI JAMES

CHELSEA wanafikiria kumnunua mlinzi wa Wolves na Ureno, Nelson Semedo mwenye umri wa miaka 28, kuchukua nafasi ya mchezaji wao wa Kimataifa wa England, ambaye ni majeruhi, Reece James, 22. (***Express***)

### SALIBA MKATABA MPYA

ARSENAL wamempa mkataba mpya mlinzi wa Ufaransa, William Saliba mwenye umri wa miaka 21. (***Athletic***)

### ZERBI AWANIWA BRIGHTON

KOCHA wa Brighton, Roberto de Zerbi, anapanga kumsajili mlinzi wa kati wa Ukraine na Shakhtar Donetsk, Mykola Matviyenko mwenye umri wa miaka 26, ambaye thamani yake ni pauni milioni 17.2. (***Athletic***)

### GOMES ANAITAKA LIVERPOOL

KIUNGO wa kati wa Flamengo na Brazil, Joao Gomes, amesema Liverpool ni timu ambayo angeichezea, ingawa Real Madrid pia wanaripotiwa kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. (***ESPN***)

### JONES AGOMBEWA WEST HAM

KLABU ya West Ham inamfuatilia, Isaiah Jones wa Middlesbrough, huku winga huyo wa England mwenye umri wa miaka 23, akiivutia pia Crystal Palace. (***GiveMeSport***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BRUYNE: KOMBE LA DUNIA 2022 LA MWISHO KWANGU

### ●●● Nina miaka 31 na sijui nini kitatokea katika miaka minne, muda haujulikani, hakuna...

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Kati wa Manchester City, Kevin De Bruyne, amekiri kwamba, Kombe la Dunia la mwaka huu nchini Qatar, linaweza kuwa la mwisho kwake.

De Bruyne ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 31, anabaki kuwa mmoja wa watu wenye vipaji vya hali ya juu duniani na ni sehemu ya timu ya Ubelgiji ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikitajwa kama mshindi wa baadaye wa Kombe la Dunia.

Alikuwa sehemu ya kikosi kilichotinga robo fainali mwaka 2014, kabla ya kushika nafasi ya tatu miaka minne baadaye.

De Bruyne amekiri kwamba ana nia ya kuchukua kwamba, michuano hii inaweza kuwa ya mwisho kwake kwani hana uhakika kama atapata nafasi nyingine ya kushinda Kombe la Dunia.

"Familia yangu inaingia kwenye hatua za makundi," alianza.

**"Nina umri wa miaka 31, na sijui nini kitatokea katika miaka minne. Hii ni mara ya kwanza kwa watoto wangu kuja kwenye Kombe la Dunia.**

"Ndiyo maana wanakuja. Itakuwa maalum, tukio ambalo sitaki wakose. Wao wana miaka sita, minne na miwili. Wakubwa wawili kati yao wanafuata mpira kidogo, lakini binti hapana. Lakini anaweza kwenda na kufurahia jua na kucheza kwenye bwawa.

"Nina furaha. Itakuwa ya tatu na daima ni maalum. Matukio haya ni mazuri kwani kila mtu anayatazama. Ni kubwa lakini hakuna maana ya kusisitiza juu yake. Ni mara yangu ya tatu, ninaelewa kinachokuja na siwezi kusema kwa ajili ya mtu mwingine ambaye atakuwa hapo kwa mara ya kwanza.

"Muda haujulikani. Hakuna maana ya kuwa na wasiwasi juu yake au kufikiria juu yake. Unaichukua inapokuja na ujaribu na kucheza vizuri iwezekanavyo. Hatuzungumzii juu yake na wenzi wa timu. Ratiba ina shughuli nyingi sana."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,046,4

MECHI KALI

JUVENTUS
VERSUS
PARIS ST GERMAIN

1 | 4.46
X | 3.80
2 | 1.69

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# POGBA RASMI KUKOSA KOMBE LA DUNIA QATAR




**PARIS, Ufaransa**

WAKALA wa kiungo, Paul Pogba, alithibitisha kuwa Mfaransa huyo hatapona jeraha lake la hivi punde kwa wakati kuelekea Kombe la Dunia.

Mchezaji huyo wa Juventus alipata jeraha la goti mapema msimu huu wa majira ya joto kwa mara ya pili katika klabu yake hiyo mpya.

Ilitarajiwa kwamba angerejea hivi karibuni, lakini jeraha la paja alilolipata akiwa mazoezini limechelewesha kurejea kwake kwa mara nyingine.

Sasa, akizungumza na Telefoot, wakala wake, Rafaela Pimenta amethibitisha kuwa Pogba hatarejea kwa wakati wa Kombe la Dunia.

"Paul angependa kurejea haraka iwezekanavyo, lakini lazima awe mvumilivu, afanye kazi kwa bidii katika nyakati hizi ngumu na ajitoe vema ili kurejea uwanjani kwa ajili ya mashabiki na timu yake haraka iwezekanavyo," alisema.

Pimenta alithibitisha kuwa Pogba atahitaji muda zaidi kupona jeraha lake la paja, ambalo linatarajiwa kumweka nje ya uwanja kwa wiki tatu zaidi.

Ufaransa tayari watamkosa mshirika wa Pogba, N'Golo Kante, baada ya Mfaransa huyo kupata jeraha la misuli ya paja ambalo litamfanya kuwa nje hadi pale michuano hiyo itakapokamilika.

Kocha Didier Deschamps hivi majuzi alisisitiza kwamba hatakuwa tayari kumwita mchezaji yeyote ambaye hatakuwa fiti, akikiri kwamba beki wa kati wa Manchester United, Raphael Varane yuko hatarini kukosa kucheza kutokana na jeraha.

"Sijawahi kupeleka mchezaji aliyejeruhiwa kwenye mashindano makubwa," alisema.

# Ibrahimovic aikejeli Ligi Kuu Ufaransa

**MILAN, Italia**


ZLATAN Ibrahimovic ameelekeza mashambulizi mapya katika soka ya Ufaransa, akidai kuwa haina umuhimu tangu alipoondoka pale Paris Saint-Germain.

Ibrahimovic alifurahia maisha mazuri akiwa PSG, akifunga mabao 156 katika mechi 180 pekee kabla ya kuondoka na kujiunga na Manchester United mwaka 2016.

Tangu wakati huo amefurahia vipindi vya mafanikio huko LA Galaxy na AC Milan, huku PSG sasa ikijivunia wachezaji watatu wa mbele Neymar, Kylian Mbappe na Lionel Messi.

Hata hivyo, pamoja na nguvu zote hizo za nyota hao, Ibrahimovic kama kawaida yake ameitupia vijembe.

"Tangu nilipoondoka Ufaransa, kila kitu kinakwenda chini," aliiambia Canal+.




"Ufaransa inanihitaji. Siihitaji Ufaransa. Hata ukiwa na Mbappe, Neymar na Messi, haikusaidii. Kwa nini? Kwa sababu huna Mungu (Mimi)."

Ibrahimovic, ambaye sasa ana umri wa miaka 41, aliisaidia Milan kunyakua taji lake la kwanza la Serie A ndani ya miaka 11 msimu uliopita, ingawa tangu wakati huo amefanyiwa upasuaji wa goti ambao litamweka nje ya uwanja hadi 2023.

Hata hivyo, amesema hana nia ya kustaafu, na kuongeza: "Nikirudi, nitasikilizwa na wanaweza kujitegemea.

"Sitastaafu, narudi na sitakata tamaa, nikiona mchezaji ana nguvu zaidi yangu nitaacha, lakini sijamwona bado."

## HABARI MICHEZO


433,814/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/11/22 | 18:00 | Blackpool vs Luton Town | 2.83 | 3.23 | 2.48 |
| 02. 05/11/22 | 18:00 | QPR vs West Bromwich | 2.44 | 3.29 | 2.84 |
| 03. 05/11/22 | 18:00 | Nottingham vs Brentford | 2.73 | 3.28 | 2.54 |
| 04. 05/11/22 | 19:00 | AC Ajaccio vs Strasbourg | 2.73 | 3.08 | 2.63 |
| 05. 05/11/22 | 20:00 | Galatasaray vs Besiktas | 2.43 | 3.33 | 2.83 |
| 06. 05/11/22 | 20:30 | Everton vs Leicester | 2.33 | 3.27 | 3.03 |
| 07. 05/11/22 | 21:00 | PAU FC vs Amiens | 2.79 | 3.14 | 2.64 |
| 08. 05/11/22 | 21:00 | Bastia vs Paris FC | 2.49 | 3.11 | 3.01 |
| 09. 05/11/22 | 21:00 | Dijon vs Guingamp | 2.50 | 3.16 | 2.96 |
| 10. 05/11/22 | 22:30 | Arminia Bielefeld vs Kaiserslautern | 2.68 | 3.28 | 2.58 |
| 11. 06/11/22 | 14:30 | Bologna vs Torino | 2.84 | 3.14 | 2.54 |
| 12. 06/11/22 | 15:00 | Chelsea vs Arsenal | 2.63 | 3.28 | 2.63 |
| 13. 06/11/22 | 15:30 | KAA Gent vs Brugge | 2.54 | 3.59 | 2.54 |
| 14. 06/11/22 | 15:30 | Eintracht Braunschweig vs Greuther Furth | 2.54 | 3.28 | 2.73 |
| 15. 06/11/22 | 17:00 | Clermont Foot vs Montpellier | 2.31 | 3.52 | 2.83 |
| 16. 06/11/22 | 19:05 | Lille vs Rennes | 2.48 | 3.48 | 2.63 |
| 17. 06/11/22 | 19:30 | Tottenham vs Liverpool | 2.88 | 3.53 | 2.30 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 02/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 1452 | Dinamo Minsk vs Energetik Bgu Minsk | 1.75 | 3.45 | 4.18 |
| 15:30 | 5762 | FC Stk 1914 Samorin vs MSK Zilina B | 1.62 | 3.99 | 4.28 |
| 16:05 | 4017 | AL Etihad vs Al Nahda (Oman) | 5.44 | 3.01 | 1.71 |
| 16:30 | 1574 | FC Olimpik vs Metallurg Bekabad | 2.20 | 2.82 | 3.45 |
| 16:30 | 1665 | Neftchi Fargona vs Otmk Olmaliq | 3.55 | 2.97 | 2.07 |
| 16:30 | 2247 | Club A Bizertin vs Esperance Tunis | 8.18 | 3.41 | 1.46 |
| 16:30 | 2863 | Mantova vs Renate | 5.05 | 3.59 | 1.60 |
| 16:30 | 3041 | Feralpisalo vs Juventus U23 | 1.86 | 3.31 | 3.85 |
| 16:30 | 3054 | Viterbo Calcio vs FC Giugliano 1928 | 3.51 | 3.21 | 1.99 |
| 16:30 | 3979 | CS Chebba vs ES Hammam Sousse | 2.49 | 2.58 | 3.22 |
| 16:30 | 4720 | Crotone vs Monopoli | 1.64 | 3.54 | 4.84 |
| 16:30 | 4783 | Pakhtakor vs Sogdiyona Jizzax | 1.46 | 3.88 | 6.41 |
| 16:30 | 5056 | Pescara Calcio vs Gubbio | 2.19 | 3.11 | 3.11 |
| 16:30 | 5904 | Qizilqum vs Kokand 1912 | 1.87 | 2.92 | 4.48 |
| 17:00 | 3509 | CD Lunda Sul vs Primeiro De Agosto | 3.55 | 2.82 | 2.16 |
| 17:30 | 4191 | Al Jahra vs Al Salmiyah | 2.92 | 3.27 | 2.21 |
| 18:00 | 2143 | AL Khlood vs Jeddah Club | 2.00 | 2.97 | 3.80 |
| 18:00 | 2564 | Lucchese vs Olbia Calcio | 1.57 | 3.66 | 5.27 |
| 18:00 | 3383 | Al Seeb vs Al Suwaiq | 1.61 | 3.37 | 5.47 |
| 18:00 | 4163 | El Daklyeh vs Al Ahly Cairo | 5.78 | 3.69 | 1.58 |
| 18:00 | 5191 | Petro Luanda vs Inter Luanda | 1.59 | 3.55 | 5.25 |
| 18:20 | 5572 | Ohud Medina vs Alshoulla | 2.30 | 2.82 | 3.21 |
| 18:30 | 3185 | AL Musanaa vs Rustaq Club | 2.54 | 2.78 | 2.88 |
| 19:00 | 3038 | AS Kigali vs Musanze | 1.49 | 3.73 | 6.20 |
| 19:45 | 3785 | Najran SC vs Al Faisaly (KSA) | 4.57 | 3.11 | 1.79 |
| 19:50 | 1793 | Al Fehaheel vs AL Sahel | 2.17 | 3.36 | 2.92 |
| 20:00 | 1749 | Enppi Club vs Zamalek | 6.74 | 3.87 | 1.50 |
| 20:45 | 2975 | Shakhtar Donetsk vs RB Leipzig | 4.85 | 4.06 | 1.59 |
| 20:45 | 4611 | Real Madrid vs Celtic | 1.22 | 6.38 | 9.96 |
| 21:00 | 1447 | CA Tigre vs Racing Club | 3.55 | 3.25 | 2.08 |
| 21:00 | 2868 | Villarreal B vs Real Oviedo | 2.77 | 2.97 | 2.62 |
| 21:00 | 4523 | Eibar vs Lugo | 1.54 | 3.81 | 5.93 |
| 22:00 | 2505 | Atletico Pr vs Goias | 1.49 | 3.85 | 5.85 |
| 22:00 | 3188 | Charlton vs Brighton U23 | 1.54 | 4.17 | 4.75 |
| 22:00 | 5096 | America Mineiro MG vs Internacional | 2.58 | 2.96 | 2.67 |
| 22:30 | 4411 | Santiago Wanderers vs CD Santa Cruz | 1.90 | 3.31 | 3.70 |
| 22:45 | 1060 | Birmingham vs Millwall | 2.48 | 3.08 | 2.83 |
| 22:45 | 1085 | Wigan vs Stoke City | 2.67 | 3.16 | 2.57 |
| 22:45 | 2508 | Cardiff vs Watford | 2.88 | 3.13 | 2.42 |
| 22:45 | 2885 | Burnley vs Rotherham | 1.43 | 4.35 | 6.73 |
| 22:45 | 3606 | Huddersfield vs Sunderland | 2.62 | 3.16 | 2.62 |
| 22:45 | 5794 | Norwich City vs QPR | 1.94 | 3.42 | 3.67 |
| 23:00 | 1741 | Mirandes vs Tenerife | 2.68 | 3.07 | 2.63 |
| 23:00 | 2238 | Juventus vs Paris St Germain | 4.46 | 3.80 | 1.69 |
| 23:00 | 2531 | Maccabi Haifa vs Benfica | 4.47 | 4.07 | 1.64 |
| 23:00 | 3816 | AC Milan vs RB Salzburg | 1.48 | 4.34 | 5.73 |
| 23:00 | 3964 | Chelsea vs Dinamo Zagreb | 1.29 | 5.34 | 8.30 |
| 23:00 | 4162 | Copenhagen vs Borussia Dortmund | 4.36 | 3.96 | 1.67 |
| 23:00 | 4800 | Manchester City vs Sevilla FC | 1.25 | 5.69 | 9.79 |
| 23:00 | 4884 | FBC Melgar vs Sporting Cristal | 1.88 | 3.21 | 3.90 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MGUNDA AANIKA TAREHE YA MWELEKEO MSIMAMO SIMBA

**Na Hadija Mngwai**

KAIMU Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amesema anasubiria hadi mzunguko wa kwanza utakapofika tamati ndipo anaweze kuona mwelekeo wa timu yake hiyo katika msimamo wa Ligi Kuu Bara.

Simba ipo nafasi ya pili ya msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa imecheza mechi nane na kuna pointi 17 huku Yanga ikiongoza ikiwa na alama 20 ikiwa na idadi sawa ya michezo na watani wao hao.

Akizungumza na Nipashe jana, Mgunda alisema kwa sasa ni mapema mno kuweza kuzungumzia mwelekeo wa timu yake kwenye ligi, hivyo anasubiria hadi mzunguko wa kwanza utakapomalizika.

"Kikosi changu nilikipa mapumziko ya siku moja na kesho (leo), kinarudi kambini kwa ajili ya kuendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo unaofuata.



"Kwa sasa ni mapema mno kuweza kuzungumzia mwelekeo wa timu kwenye msimamo wa Ligi Kuu, tukimaliza raundi ya kwanza ndio nitakuwa na neno la kusema kulingana na tutakapofikia.

"Tunachotakiwa kukifanya kwa sasa ni kupambana ili tuweze kumaliza vizuri mzunguko wa kwanza," alisema Mngunda.

Mwishoni mwa wiki Simba iliibuka na ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Mtibwa Sugar, ikiwa ni baada ya kupoteza mechi yake ya kwanza Ligi Kuu msimu huu dhidi ya Azam FC katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kwa sasa Simba imeingia kambini kujiwinda na mechi ijayo ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Singida Big Stars itakayopigwa Uwanja wa Liti mkoani Singida Jumatano ijayo.

## Simba Queens majaribuni tena

INATOKA UK. 32

ma.

Simba Queens itamaliza mechi zake za hatua ya makundi Jumamosi kwa kuwavaa Green Buffalo, mechi ambayo itachezwa katika mji wa kitalii wa Marrakech, umbali wa zaidi ya kilomita 300 kutoka hapa Rabat.

Katika mechi za juzi usiku, TP Mazembe Queens ilianza vema michuano hiyo kwa kuifunga Wadi Degla ya Misri bao 1-0 wakati kinara wa Kundi B ni Mamelodi Sundowns Queens ambao iliwafunga Bayelsa Queens kutoka Nigeria mabao 2-1.

# Yanga, Watunisia dk. 90 za jasho leo

INATOKA UK. 32

Jumapili dhidi ya Geita Gold FC, lakini Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), hawakujibu maombi na kulazimika kucheza.

Nabi alisema kutokana na mchezo dhidi ya Geita Gold, wachezaji wawili waliumia na kwamba hawatakuwapo katika kikosi cha mchezo wa leo dhidi ya Club Africain.

"Naogopa kutaja majina ya wachezaji hao na hata wale watakaokosa kwa sababu ndani ya kikosi changu kuna mchezaji mkubwa na tegemeo tunaweza kumkosa katika mechi ya leo," alisema.

Kwa upande wa mwakilishi wa wachezaji wa Yanga, Yusuf Athumani, alisema wamejiandaa vizuri na wako tayari kwa ajili ya kutafuta ushindi katika mchezo huo wa nyumbani.

"Tumejiandaa vizuri na tutapambana katika mchezo wa kesho ili tusonge mbele katika hatua inayofuata," alisema Athumani.

Kocha wa Club Africain, Mfaransa Bertrand Marchand, alisema anafurahi kuwasili kwa mara ya pili baada ya wiki tatu kutoka hapa nchini na wamerejea kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri.

Alisema wamejiandaa vizuri kuja kupata matokeo mazuri na wanafahamu ubora wa Yanga, na ana imani utakuwa mchezo mzuri na ushindani mkubwa.

"Tumejiandaa vizuri, wachezaji wote wako tayari kwa ajili ya mechi ya kesho (leo), tutacheza kwa tahadhari na umakini mkubwa kwa sababu wapinzani wetu ni wazuri," alisema Bertrand.

Alisema kuna baadhi ya wachezaji kama Mayele (Fiston)ambaye alitaka kumsajili msimu uliopita, Tuisila Kisinda na Juses Moloko ambao amewajua wakicheza katika Klabu ya AS Vita ya DR Congo.

"Yanga wana wachezaji wazuri sana, na baadhi yao wanatumikia mataifa yao, utakuwa mchezo mzuri na ushindani mkubwa, hatujali Yanga wanapata matokeo kipindi gani kwa sababu katika mpira matokeo yanapatika kipindi chochote," alisema Kocha huyo.

Nahodha wa Club Africain, Nader Ghandri, alisema ni mechi muhimu sana kwao na wiki mbili wamejiandaa kwa ajili ya mchezo huo ili kupata ushindi.

"Tumejiandaa vizuri kuelekea mchezo wa kesho (leo), tunajua Yanga wana mashabiki wengi, hata kwetu tuna mashabiki wengi zaidi na tunahitaji ushundi ili kuwafurahisha mashabiki wetu.

"Tumekuja kivingine kwa kufanyia kazi makosa yaliyojitokeza na kujipanga kwa mechi yetu dhidi ya Yanga, ukizingatia mechi ya Kipanga tulitoka nao suluhu na kushinda nyumbani," alisema Ghandri.

# Michezo

Jumatano Novemba 2, 2022

Nipashe




UKURASA 29

## Bruyne: Kombe la Dunia 2022 la mwisho kwangu

# YANGA SC, WATUNISIA DK. 90 ZA JASHO LEO

●●●Nabi ataja wakuchungwa na mipira iliyokufa, wenyewe wasema wanamjua sana Mayele...

**Na Saada Akida**

WAWAKILISHI wa Tanzania wanaosaka nafasi ya kushiriki hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, Yanga leo watakuwa na shughuli pevu ya kusaka ushindi dhidi ya wapinzani wao, Club Africain kwenye mechi itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kuelekea mchezo huo wa kwanza kabla ya kurudiana Jumatano ijayo nchini Tunisia, Kocha Mkuu wa Yanga, Mtunisia Nasreddine Nabi, amemtaja beki wa Club Africain, Nader Ghandri kuwa anapaswa kuchungwa zaidi, lakini wapinzani wao nao wakawataja Fiston Mayele, Tuisila Kisinda na Jesus Moloko kuwa wanawafahamu vizuri.

Akizungumza na Nipashe jana, Nabi alisema wachezaji wake wana ari ya kutaka kufanya vizuri katika mechi hiyo ya leo na kwamba anaamini watajituma ipasavyo kupata matokeo mazuri ili kupata nafasi ya kusonga mbele ya hatua inayofuata.

Nabi alisema wanatakiwa kuchunga wachezaji wote kwa sababu wengi wao wapo katika kikosi cha timu ya Taifa ya Tunisia na nyota wa kuchungwa sana ni Ghandri.

"Tunatakiwa kuwa makini kuhakikisha hatuwapi nafasi kwenye mipira ya kufa kwa sababu wachezaji wao ni wazuri sana katika mipira hiyo," alisema Nabi.

Alisema Club Africain ni timu kongwe kwa Tunisia na wakubwa katika historia ya soka, lakini wachezaji wake wapo tayari kupambana kupata matokeo mazuri zaidi nyumbani na hata ugenini.

Nabi alisema presha haiko benchi la ufundi wala kwa wachezaji kwa kuwa katika soka hakuna hofu, ni mchezo unaohitaji kujiandaa vizuri na kupata matokeo yenye mabao mengi kwa ajili ya kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kusonga mbele.

"Kuhusu mfumo inategemea na aina ya wachezaji wangu, nitaendelea kutumia mfumo wa mshambuliaji mmoja kulingana na nyota niliokuwa nao, si kwa sababu ya timu ya nyumbani, nitafurahi kuwatoa au kusonga mbele bali kikubwa naomba Mungu atusaidie tufuzu ikiwa ni shukran kwa mashabiki wa Yanga," alisema Nabi.

Alisema anahitaji kuwapa furaha Wanayanga ikiwamo kupata ushindi na ataumia zaidi hasa atakapotolewa katika michuano hiyo.

Nabi alisema walikuwa na muda mfupi wa maandalizi na kikubwa wameangalia zaidi wapinzani wao wanavyocheza huku baada ya mechi ya Geita Gold akiwapa muda wachezaji wake kupumzika kwa sababu ya mfululizo wa ratiba za mechi za Ligi Kuu.

Alisema awali waliomba kusogezewa mechi waliyocheza

INAENDELEA UK. 31




Mayele

## Simba Queens majaribuni tena

**Na Somoe Ng'itu, RABAT**

HAWAPONI, hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, kuelekea mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake dhidi ya Determine Girls kutoka Liberia itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Prince Heritier Moulay El Hassan, Morocco.

Mechi hiyo itachezwa kuanzia saa 11:00 jioni kwa saa za Morocco sawa na saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania na baadaye saa 2:00 kwa hapa wenyeji ASFAR FC walioifunga Simba Queens bao 1-0 mchezo wa kwanza, watawakaribisha Green Buffalo kutoka Zambia.

Simba Queens ambao ni Mabingwa wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), wanahitaji kushinda mechi ya leo ili kurejesha matumaini ya kusonga mbele katika michuano hii ya kimataifa ambayo inafanyika kwa mara ya pili barani Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lukula, alisema wamejipanga kuhakikisha hawarudii makosa yaliyojitokeza katika mechi iliyopita na anaamini wachezaji wake wanaweza kusaka matokeo chanya.

Lukula alisema hajakata tamaa ya kusonga mbele na endapo watapata ushindi katika mchezo wa leo, mipango na mikakati yake itatimia.

"Ninawaamini wachezaji wangu, ninaamini watalipiza kisasi, tunachohitaji kesho (leo) ni ushindi, haijalishi mabao mangapi, halafu ndio tutaanza mipango ya kuwakabili Green Buffalo, kazi kubwa ni kuwamaliza hawa Determine Girls kutoka Liberia," alisema Lukula.

Kocha huyo aliongeza kuwa licha ya wapinzani wao kufungwa idadi kubwa ya mabao katika mchezo wao wa kwanza, kikosi chake kitaingia uwanjani kikiwaheshimu kwa sababu katika michuano hii hakuna timu ndogo.

Nahodha wa Simba Queens, Oppa Clement, aliliambia gazeti hili kuwa wachezaji wote wamejiandaa kupambana kuhakikisha wanapata ushindi katika mechi ya leo.

"Tunajua kesho (leo) ndio fainali yetu, tutafanya kile ambacho sisi pia tunakihitaji, tunaamini malengo yetu yatatimia, bado nafasi tunayo na kilichobakia ni kuomba tuamke salama," Clement alise-

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >